

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 27 Juni, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Kikao cha Kumi na Moja cha Mkutano wetu wa nane.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 85

Wabunge Kulipwa Pensheni

MHE. NASSIB SELEMAN OMAR aiuliza:-

Wabunge wa Tanzania huwa na maisha magumu sana pale wanapomaliza vipindi vyao vya Ubunge na Wabunge wa nchi jirani kama Kenya hulipwa pensheni pindi wanapomaliza kipindi chao cha Ubunge.

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha sheria itakayowawezesha Wabunge nchini kulipwa penshnsni baada ya kumaliza vipindi vyao vya Ubunge?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kiinua mgongo cha Wabunge ili kiendane na hali halisi ya maisha ya sasa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nassir Suleiman Omar, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa masharti ya kazi ya Mbunge aya ya 25, stahili ya kazi ya Mbunge ni malipo ya kiinua mgongo (*gratuity*) na siyo pensheni. Malipo hayo hutolewa kwa mujibu wa kifungu cha 21(1) – (3) cha Sheria ya Hitimisho la Kazi ya Vingozi wa Kisiasa namba 3 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, pensheni hulipwa kwa Mtumishi wa Umma mwenye masharti ya kazi ya kudumu na malipo ya uzeeni (*Permanent and Pensionable*). Mtumishi mwenye masharti hayo huchangia sehemu ya mshahara wake kila mwezi kwenye Mfuko wa Pensheni husika. Hali hii ni tofauti kwa Waheshimiwa Wabunge kwani hulipwa kiinua mgongo (*gratuity*) kipindi chao cha Ubunge kinapokwisha. Kwa misingi hiyo, Serikali haioni

umuhimu wa kutunga sheria nyingine kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kulipwa pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiongeza mishahara ya Waheshimwa Wabunge sambamba na watumishi wengine wa Umma kila hali ya uchumi inavyoruhusu. Kwa kiinua mgongo hukokotolewa kwa kuzingatia asilimia ya mshahara ni dhahiri kuwa kiinua mgongo nacho kinaongezeka kila mshahara unavyoongezeka.

MHE. NASSIB SELEMAN OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri, lakini vilevile ajue kwamba Bunge la Kenya na Bunge la Zanzibar baada ya kuangalia hali halisi ya maisha ya Wabunge ambao wanaishi baada ya kumaliza muda wao wamebadilisha sheria na sasa hivi wanaanza kuwalipa pensheni, mfano Zanzibar wataanza kuwalipa shilingi 1,000,000/= kila mwezi baada ya wajumbe wake kumalizika vipindi vyao. Tuna taarifa vilevile kwamba Kenya inalipa dola 1,000 kwa mwezi baada ya kumaliza muda wao wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo hii sheria si kama msahafu lakini tunaangalia hali halisi ya Wabunge waliokuwa nayo baada ya kuacha Ubunge. Wengi wa Wabunge wanauza nyanya, wanafanya kazi ambazo ni aibu kwa Bunge hili. Kwa hivyo naitaka Serikali iangalie kwa makini suala hili na sheria ibadilishwe ili Wabunge waweze kupata mafao hayo? Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Majibu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ukizingatia suala hili ni muhimu sana. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli inawezekana wenzetu wa Zanzibar Baraza la Wawakilishi na Kenya wanafanya hivi. Lakini kwa sasa kwa Bunge letu hivi ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unajua kwamba kwanza kwa mujibu wa sheria sisi humu ndani huwa tunaanza kuzungumza kupitia Tume yetu wenyewe. Tume yetu na Wabunge tuliridhia twende kwenye *gratuity*. Sasa kama hili jambo mnafikiri sasa msimamo umebadilika twende kwenye pensheni nashauri sisi Serikali hatutakuwa na pingamizi yoyote ili mradi utaratibu ule ufuatwe. Kwamba Tume yetu ipendekeze, tuzungumze na Serikali na kwa sababu ndani ya Tume kuna Serikali tuzungumze tuone tuchanganue uzuri na ubaya wa kupata pensheni na namna ya kufanya ili kama ikibidi sheria hii irekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama Serikali hatuna pingamizi na hili lakini tuzungumze kupitia utaratibu wetu tuliojiwekea. (*Makofi*)

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa muda mrefu sasa Wabunge wa Viti Maalum wamekuwa wakiomba Serikali iweze kuwapatia fedha za kuhudumia mikoa ambayo wanaiwakilisha. Lakini kilio hiki kimekuwa cha

muda mrefu Ofisi ya Waziri Mkuu tunaona kwamba haitekelezwi tofauti na Wabunge wenzetu wa Majimbo wamekuwa wakipewa fedha za Maendeleo ya jimbo.

Ukiangalia nchi za jirani Uganda na Kenya Wabunge wanaowakilisha Wilaya wanapewa fedha za kuhudumia hizo Wilaya. Ni lini Serikali itaacha ubaguzi kwa Wabunge wa Viti Maalum na kuwezesha fedha kwa ajili ya kuhudumia mikoa? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali inatoa fedha na bahati nzuri mwenyewe amekiri kwamba zinatolewa kwa sheria ya Wabunge wa Majimbo, sio wa Mikoa. Hakuna Mbunge wa Mkoa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hiyo *terminology* tumejitungia kienyeji hapa. Lakini ninyi ni Wabunge wa Viti Maalum sio Wabunge wa Mikoa. Kwa hiyo, sheria inasema kwamba wale wenye Majimbo waliochaguliwa moja kwa moja na wananchi ndio wanaopewa fedha hizi kwa ajili ya kuhudumia yale Majimbo.

Kwa sasa sheria iko hivyo na hao uliowatolea mfano katika uchaguzi wa Uganda kuna Wabunge wa Majimbo lakini vimetengwa Viti Maalum kwa maana ya kwamba wanawake watagombea majimbo yanayoitwa Wilaya, wanagombea na wanachaguliwa.

Kwa hiyo kule kuna Majimbo yanaitwa Wilaya, kuna Majimbo yanaitwa Majimbo. Kwa hiyo wale wamechaguliwa *Direct* kama walivyo Wabunge wa

Majimbo. Kwa hiyo, ni vitu viwili tofauti. Hili tulishasema linazungumzika lakini tujenge hoja kwa sasa sheria inasema ni Wabunge wa Majimbo. *(Makofi)*

Na. 86

Kijiji cha Mlowo Kupewa Hadhi Kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Kijiji cha Mlowo chenye idadi ya watu karibu 30,000 kimsingi ni mji tayari, na kimekua sana kiasi cha kusababisha uongozi wa kijiji hicho kushindwa kukabiliana na changamoto za kukua kwake kama vile, huduma za jamii, miundombinu na shughuli za kibiashara kwa ujumla:-

Je, ni lini sasa kijiji hicho kitapandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA
MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zamb, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Kijiji cha Mlowo kina idadi ya watu inayofikia 30,000 kiasi cha kuleta changamoto

katika utoaji wa huduma kwa wananchi wake. Aidha, zipo taratibu na vigezo vinavyozingatiwa katika uanzishaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo kama ilivyo katika maeneo mengine ya utawala ambapo suala hili linapaswa kuanzia kwa wananchi wenyewe na kujadiliwa katika vikao vilivyowekwa kisheria katika ngazi za Vijiji, Kata (Kamati za Maendeleo za Kata), Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa. Hoja ya msingi hapa ni ushirikishwaji wa wananchi na kupata ridhaa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ni kwamba pendekezo hilo halijajadiliwa katika Kikao cha Baraza la Madiwani na vikao vingine vya kisheria. Hivyo, taratibu hizo za kisheria zikikamilika na kijiji hicho kukidhi vigezo vya kupandishwa hadhi kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlowo, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI haitasita kuridhia pendekezo hilo. Rai yangu ni kwamba sheria na taratibu zizingatiwe katika kushughulikia suala hili. *(Makofi)*

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba tu nitoe masikitiko yangu kwa majibu ya Serikali kwa sababu vikao vyote katika kijiji cha Mlowo vyote vilishakaa mapendekezo yalishaenda Wilayani, kulishakaa *Finance Committee*, Baraza la Madiwani lilishakaa. Sasa nasikitika Mheshimiwa Waziri anaposema kwamba taarifa zilizopo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kwamba jambo hili halijajadiliwa amelipata wapi kwa sababu leo nimezungumza na Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Halmashauri tunathibitishiana kwamba

tulishakaa yeye Waziri taarifa hizi amezipata wapi na kama ni upungufu yuko tayari kukiri hapa?

Swali la pili, kwa kuwa ni kweli mji wa Mlowo una changamoto kubwa na nyingi na hivi karibuni wafanyabiashara wa mji ule walianza kugoma kutoa ushuru kwa sababu kijiji hakiwezi kukabiliana na changamoto zilizopo pale. Je, ni kwa haraka kiasi gani sasa kama taarifa zote hizi zitafikia TAMISEMI ni kwa haraka kiasi gani Serikali itaridhia kijiji cha Mlowo kuwa mji ili kuondokana na adha na kadha zinazowakumba wana-Mlowo sasa hivi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo ninayozungumza hapa siyazungumzi mambo yangu mimi kutoka kichwani ninavyofikiri. Ndugu yangu Zamboni wala asiwe na tatizo na jambo hili. *Regional Commissioner* yupo hapa, RAS yuko hapa na wale wengine wanaohusika wote nimezungumza nao *The bottom line is* hakuna *documents* zilizotoka katika Mkoa ule kuja Makao Makuu ambazo zinaomba kuwa na mamlaka ya mji mdogo wa Mlowo.

Nataka niiseme hii na wale wengine wote ambao wameomba nilikuwa nazungumzia hapa hakuna mgongano wowote katika kuanzisha Mamlaka ya mji mdogo. Anachozungumza Mheshimiwa Zamboni hapa tumeangalia kwa kupitia njia nyingine ambayo sio hii anayozungumza. Kijiji kinachozungumzwa kina watu 30,000, Sheria hii tunayoizungumza hapa ni Sheria Na. 8 ya Mamlaka ya Mji Mdogo inahitaji watu wawe 10,000

tu, kuwe na maduka pale, kuwe na Makao Makuu ya Kata na Tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama *documents* hizi ziko hapa atuletee hapa hili jambo wala sihitaji kwenda ku-*consult* kwa sababu ni suala ambalo linafahamika kisheria na sheria zenyewe ninazo hapa. Nataka nimwambie atuitie huyo mtu aliyetumwa aliyeleta hapa twende tukashughulikie jambo hili. Hili la kwanza na nikikuta kuna mtu wa kwetu amehusika humo ndani kwamba amekaa na hizo *documents* hakuwasilisha kunakohusika kwa kufanyiwa kazi, tutachukua hatua pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hili la wananchi kwamba wamekataa sasa kulipa ushuru na vitu vingine. Namwomba sana Mheshimiwa Mbunge hawataweza kukataa hapa jambo hili wakasema sisi unajua mpaka tuwe Mamlaka ya Mji Mdogo ndipo tutakapolipa ushuru, tutakuwa sasa tunarudi nyuma. Yaani kwa maneno mengine ni kwamba watakuwa hawa-*qualify* kwa sababu moja ya mambo ambayo tunayazungumza katika kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo ni kujenga pia uwezo wa ndani kwa sababu hii Mamlaka ya Mji Mdogo utakuwa na Bajeti yake. Bajeti hiyo itakuwa *an integral part* ya ile Halmashauri mama iliyoko pale.

Ninamwomba sana Ndugu yangu Zamboni twende tukakae na wananchi hawa tukawaambie wakati sisi tunahangaika hapa kama Serikali kuhakikisha kwamba tutakuwa na mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlowo kipindi

hiki cha Mpito kitumike pia kujenga uwezo wa kiuchumi ambao utawezesha Halmashauri hiyo kuanza kazi. Nasema kwamba hakuna tatizo lolote kuanza jambo hili, sisi tuko tayari kuanza mradi tufuate hizi taratibu na vigezo ambavyo nimevisema hapa.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa suala la miji midogo na hasa lile lililotajwa kule katika Wilaya ya Mbozi ni kama suala la uanzishwaji wa Mji Mdogo wa Madaba katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea jimbo la Peramiho. Kwa kuwa mchakato mzima anaousema Waziri wa kisheria Kijiji cha Madaba kimeshatekeleza vikao vyote mpaka *RCC* vimeshamaliza kazi yake. Kwa kuwa sasa ni wakati muafaka wa Naibu Waziri kuwatangazia wananchi wa Madaba kwamba mwakilishi wao Mbunge nimemaliza kazi yangu.

Je, ni lini sasa Serikali itatangaza kwenye gazeti lake Kijiji cha Madaba kwamba sasa ni Mji Mdogo na ili Halmashauri yetu ianze kutenga Bajeti ya Mji Mdogo katika Kijiji kile ili kuondoa wingu la kisiasa linaloonesha kwamba Mbunge hajatimiza wajibu wake? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, hii sasa ni kweli. Yeye Mheshimiwa Jenista Mhagama *documents* zao zipo, tunazo hizo. Ni kweli zimeshakuja. Tulichofanya katika jambo hili na nimpongeze sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa

sababu ni jambo ambalo alikuwa analifuatilia kila wakati. Tulikabana hapa mpaka ikabidi mimi mwenyewe niende Madaba huko nikaangalie lile eneo analolizungumzia kwa sababu hii Halmashauri ya Mji Mdogo inapoanzishwa maana yake ni nini?

Ni kama ile ya Kibaigwa unavyoona inakwenda pale. Unaitazama Kibaigwa unasema Kibaigwa inavyokwenda namna hii kama hatutaweka Mamlaka pale ambayo itakuwa ina-*plan* maana yake ni kwamba utakuwa na ma-*squatter* pale na mji utavurugika pale. Hutajua nguzo za umeme zimepita wapi, hutajua kwamba simu zitapita wapi na bomba za maji zitapita wapi, *drainage system* na vitu vingine vitapita wapi, misikiti na makanisa yatajengwa wapi.

Kwa hiyo tulichofanya hapa kuhusu hili na hii naijibu pamoja na wale wengine na Mheshimiwa Lwanji najua atasimama hapa na kuuliza swali hili. Tulichofanya ni kwamba tumeunda timu hapa ili kwenda sasa kuangalia hicho kinachosemwa kwenye hizo *documents* ni kweli.

Wewe unaweza ukaanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo ukakuta inakwenda mpaka kwenye Kata ya watu wengine au kwenye tarafa ya watu wengine halafu baadaye ukifanya maamuzi kule mbele unasikia mgogoro unaanza tena pale tunataka haki zetu tunaonewa.

Sasa hii yote ni lazima tujiridhishe kwamba mambo haya yamekwenda kama yanavyotakiwa na baada

ya hapo tutashughulikia. Ninamwomba Mheshimiwa Mhagama awe na hakika kwamba jambo hili tunalishughulikia sasa kwa ajili ya kutathmini na kuthibitisha hilo lakini ni kweli kwamba hili tunalo na halina tatizo lolote. *(Makofi)*

Na. 87

Soko la Uhakika Kwa Wakulima wa Choroko Nanyumbu

MHE. DUSTAN D. MKAPA aliuliza:-

Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu ni wakulima hodari wa zao la choroko lakini wanunuzi wa zao hilo walilinunua kwa bei ya chini sana msimu uliopita:-

Je, ni lini Serikali itawahakikishia soko la uhakika wakulima wa zao la choroko Nanyumbu?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nawapongeza wananchi wa Nanyumbu kwa kilimo cha choroko kwa wingi. Wakulima wa zao hili hawapati bei nzuri kutokana na ushindani mdogo katika mfumo wa ununuzi wa zao hilo, hivyo

kusababisha wanunuzi binafsi (walanguzi) kununua choroko moja kwa moja kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza mikakati ambayo imeonesha mafanikio katika kuwahakikishia wakulima bei nzuri ya mazao ya wakulima kwa utaratibu au mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani ambao umepunguza changamoto za bei, ubora wa zao, uhifadhi, upatikanaji wa takwimu sahihi za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa stakabadhi ghalani umeonesha mafanikio katika mazao ya mbegu mafuta ya ufuta mkoani Lindi na alizeti mkoani Singida.

Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ametuhakikishia kuwa Wilaya ya Nanyumbu inazalisha kwa wingi zao la choroko Wizara yangu itafanya utafiti katika mwaka wa fedha 2012/2013 ili kuweza kuliingiza zao la choroko katika mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani kwa vile zao hili linalimwa pia katika maeneo mengine kama vile Singida, Wilaya ya Igunga na Manyara.

Ni mategemeo yangu kwamba matumizi ya mfumo wa stakabadhi kwa zao hili utaongeza ushindani na kuwahakikishia wakulima bei nzuri kuliko ile inayotolewa na walanguzi wa choroko Wilayani Nanyumbu. *(Makofi)*

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini

nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mfumo huu wa stakabadhi ghalani ulileta mushkeri kidogo katika zao la korosho msimu uliopita.

Je, Serikali itawahakikishia wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu kwamba wakulima wa zao la korosho mfumo utakapoanza watalipwa fedha yao yote kwa mkupuo mara moja na baadaye wasubiri malipo ya majaliwa?

Swali la pili, endapo mfumo huu wa stakabadhi ghalani hautaweza kuanza katika msimu ujao. Je, Serikali ina wahakikishiaje wakulima wa zao hili la choroko bei nzuri hapo watakopolima zao hili hapo mwakani.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:
Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge analinganisha kwamba utaratibu au mfumo huu wa stakabadhi ghalani umeleta usumbufu sana katika zao la korosho na anaonyesha wasiwasi kwamba utaratibu huu ukitumika kwenye zao la choroko nao utaleta matatizo yaleyale.

Nataka nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba huu mfumo wa stakabadhi ghalani kusema kweli wakati umeanza tulitegemea kwamba ungefanya vizuri lakini kwa matatizo ambayo yalikuwa yametokana na wale wasimamizi wakuu wenye dhamana na uratibu wa zao hili la korosho hawakuweza kufanya vizuri na Serikali ilibainisha hilo na ilichukua hatua za kuwawajibisha baadhi ya watendaji hao ambao hawakufanya vizuri.

Sasa Mfumo hauna tatizo, mfumo ni mzuri na unawalinda sana wakulima hasa kupambana na walanguzi ambao huwa wanavamia wakati wa mavuno wananunua kwa wingi na baadaye wao ndiyo wanaofaidi wale wakulima wanaolima hawafaidi chochote kwa sababu ya hawa walanguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kwamba walipwe kwa mkupuo kama wakulima wa korosho na hawa wa zao lingine. Kusema kweli Waheshimiwa Wabunge malipo ya mkupuo kwa wananchi kwa ujumla siyo mazuri yanaleta hasara sana kwa sababu unalipwa mkupuo wakati wa mavuno lakini ukikaa baadaye kidogo bei zinakuwa nzuri na zinapanda kwa hiyo wewe utakuwa umeshalipwa kwa mkupuo. Lakini kama unasuburi unaweka kwenye maghala halafu bei ikiwa nzuri unafaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kusema kwamba bei nzuri kwa wakulima wa choroko kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba huu utaratibu wa mfumo wa stakabadhi ghalani ndiyo mfumo pekee ambao naona kwamba unaweza kuwasaidia wakulima wetu kupata bei nzuri kwa kuwa na subira na kuweka mazao ghalani. Bei ikiwa nzuri wanalipwa bei nzuri wakati ukishapita kuliko ule wa mavuno kama nilivyosema kwamba wakati wa mavuno hawa walanguzi wana-*dominate* wanachukua mazao wanaweka bei ikipanda wanauza. Kwa hiyo, wao ndiyo wanaofaidi.

Kwa hiyo mimi nazidi kusesitiza, na Serikali inasisitiza kwamba huu utaratibu wa stakabadhi ghalani ndiyo unaofaa mpaka mpaka sasa. *(Makofi)*

Na. 88

Kuwapatia Umeme Wananchi wa Ikhanoda

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuza:-

Serikali imeshaanza kutekeleza ahadi ya kuwapatia umeme wananchi wa Ikhanoda kwa kuweka nguzo tangu mwaka 2004 na kwamba umeme unaotoka Singida Mjini unapitia katika Mji huo:-

Je, ni lini umeme utawaka katika Kata hiyo yenye wakazi wengi na huduma nyingi muhimu?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kata ya Ikhanoda iliyoko Iramba Mashiriki ni miongoni mwa Kata zenye mwamko mzuri wa maendeleo ya kijamii na hivyo huduma ya umeme itakuwa kichocheo kikubwa cha Maendeleo. Kata hiyo imepitwa na njia ya umeme wa msongo wa KV 33 inaopeleka umeme katika Hospitali ya Iramba. Kata ya Ikhanoda ilikuwa kwenye mpango wa kuwekewa umeme kwenye Bajeti ya mwaka

2004/2005. Hata hivyo kutokana na matatizo ya kiutendaji yaliyotokea katika kipindi hicho mradi huu haukukamilika na hivyo kusababisha kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme Ikhanoda inahitaji *transfoma* moja yenye uwezo wa KVA 200 na njia ndogo ya umeme wa msongo wa KV 0.4 yenye urefu wa kilomita 4. Mradi unakadiriwa kugalimu jumla ya shilingi milioni 102. Mradi huu ulikuwa miongoni mwa miradi iliyopendekezwa na *TANESCO* ili Shirika la Umeme liweze kuutengea fedha za utekelezaji katika kipindi cha Bajeti ya Shirika ya mwaka huu wa 2012, lakini kutokana na uhaba wa fedha katika Shirika kwa sasa mradi huu utatekelezwa na Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, *REA* imetenga fedha kwa ajili ya Miradi huu katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 ili kuhakikisha umeme unawaka katika Kata hiyo. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi miwili baada ya fedha kupatikana.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Lakini kabla sijauliza maswali naomba niweke rekodi vizuri. Kata hii iko Wilaya ya Singida, Jimbo la Singida Kaskazini sio Iramba na umeme huo unaenda Hospitali ya Iyambi sio Hospitali ya Iramba. Iramba ni Wilaya.

Sasa nauliza maswali yangu. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja Waziri wake na Katibu Mkuu kwa muda mfupi waliokaa pale

wamepata pesa za kupeleka kwenye mradi huu. Mradi huu ulitengewa pesa mwaka 2004 na ukaanza kutekelezwa lakini Afisa aliyekuwa anasimamia mradi huu aliyeyuka na vifaa vyote vya mamilioni ya pesa wakati kwenye vitabu anaandika mradi ametekeleza wakati hakutekeleza amekwenda kumwaga nguzo chini akaishia. Lakini Afisa huyu akapewa adhabu ya kufukuzwa kazi tu haya mamilioni hakuyarudisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli tunaitendea haki Serikali kumwacha mtu hivi hivi tu? Naomba nipewe majibu katika hilo. La pili, ipo miradi ya kupelekea umeme Singida ambayo kila Bajeti inatamkwa lakini utekelezaji unakuwa haupo hela zinakosekana kwa mfano kupeleka umeme Sepuka kutoka Singida Mjini, kupeleka umeme Mgongo kutoka Shelui mji mdogo pamoja na kupeleka Londoni kwenye mgodi wa dhahabu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atawathibitishia wananchi hawa kwamba sasa miradi hiyo itatekelezeka kupitia Bajeti hii ya 2012/2013?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mradi huu ulitakiwa utekelezwe katika bajeti ya mwaka wa fedha 2004/2005 na kweli yalitokea matatizo ya kiutendaji watumishi ambao walihusika katika kutekeleza mradi ule walifanya wizi wa vifaa na kwa taarifa ambazo tunazo ni kwamba wamechukuliwa hatua za kinidhamu kwanza kufukuzwa kazi lakini tumeshaagiza *TANESCO* kuchukua hatua zaidi za kinidhamu na hasa

kuwafikisha katika vyombo vya Sheria wote waliohusika na wizi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna miradi mingi ya umeme ambayo inatakiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 na Mheshimiwa Mbunge bahati nzuri ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anafahamu kuna miradi mingi ya vijijini ambayo tunayo katika Wizara ambayo inafadhiliwa na Mradi wa *Electrical Five* ambao unahusisha vijiji vyote na tumeviweka katika awamu.

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika awamu inayofuata maeneo yale ya Londoni na maeneo mengine ambayo ameyataja tutayaweka katika mpango wa utekelezaji.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Shirika la Umeme TANESCO katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu linakabiliwa na tuhuma za rushwa ikiwa ni pamoja na kuweza kung'oa nguzo kwenye maeneo ambayo umeme ulipaswa kupelekwa.

Je, Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari either wewe Naibu Waziri au Waziri mwenyewe baada ya Bunge tuweze kufanya ziara katika Jimbo la Kasulu Mjini ili kuweza kuthibitisha madai haya na malalamiko ambayo yamekuwa yanatolewa na wananchi na hatimaye kuweza kutatua matatizo.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa taarifa

hizi nazipokea sasa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge nitamwomba Mheshimiwa Mbunge tuanane baada ya kikao anifafanulie vizuri na ikiwezekana kunipatia vielelezo kama anavyo na mimi nimhakikishie nitakuwa tayari kufanya ziara eneo la Kasulu na kuangalia matatizo yote yaliyojitokeza ya rushwa.

Na. 89

Kuongeza Nguvu ya Umeme wa Kusukuma Pampu za Maji

MHE. MKIWA ADAM KIWANGA aliuliza:-

Wananchi wa Nyasaka Wilaya ya Ilemela Mkoa wa Mwanza na maeneo jirani wanakabiliwa na shida kubwa ya upatikanaji wa majisafi na salama kwa muda mrefu kutokana na nguvu ndogo ya umeme uliopo ambao unashindwa kusukuma pampu za maji.

Je, Serikali itaongeza lini nguvu ya umeme katika maeneo hayo ili kuziwezesha pampu za maji kufanya kazi kwa ufanisi na hivyo kuondoa tatizo hilo la maji?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Nyasaka, Wilaya

ya Ilemela Jijini Mwanza na maeneo jirani, halitokani na nguvu ndogo ya umeme bali linatokana baadhi ya wakazi kuwa kwenye miinuko hivyo maji, ambayo hutoka kwenye tenki la maji kwa nguvu ya uvutano hushindwa kuyafikia maeneo ya miinuko kutokana na nguvu ndogo ya msukumo. Hivyo, kwa ufumbuzi wa muda mfupi Idara ya Maji inatafuta eneo la kuweka *booster* ili kusukuma maji kwa nguvu na kuyafikia maeneo ya miinuko. Aidha, maeneo haya yana umeme wenye nguvu za kutosha hakujawahi kuwa na nguvu ndogo ya umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania lipo tayari kuunganisha umeme katika *booster* itakayofungwa kwa ajili ya kusukuma maji. Hivi sasa kinachosubiriwa ni malipo ya gharama ya kazi hiyo na maelekezo ya wapi *booster* hiyo ya maji itafungwa ili utaratibu wa kufunga umeme uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ninamwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na viongozi wa umeme ya Nyasaka kutoa ushirikiano kwa Shirika la Umeme *TANESCO* ili kufanikisha kazi hiyo.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Napenda niulize maswali mawili ya nyongeza. Katika Bunge la Tisa niliuliza swali hili katika Idara ya Maji aliyekuwa Waziri wa Maji Mheshimiwa Mwandosya alifanya juhudi na kunipa jibu kwa maandishi kwamba wale watu hawakosi maji kutokana na Idara ya Maji. Wanakosa maji kutokana na *TANESCO*. Sasa basi ninaona kwamba Serikali haifanyi kazi kwa pamoja kama Mawaziri. Ninaiomba Serikali

sasa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Waziri wa Maji washirikiane kwa pamoja ili wananchi hao waweze kupata maji kwani ni muda mrefu kero hii imekuwepo, kuna shule nyingi za *boarding* kuna wakazi wengi mji unapanuka kwenda kule ili waweze kupata maji.

Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema maeneo haya ni maeneo ya miinuko na kwa hiyo hawajafunga booster lakini hata Mkuu wa Mkoa wa Mwanza anakaa mlimani ni eneo la miinuko na yeye anapata maji. Ninaiomba Serikali. Ninaiomba Serikali isiangalie isiangalie nani anakaa wapi kama ni miinuko wananchi wote wa Jiji la Mwanza hawawezi kuyaona maji kama jua ni haki yao ya msingi kupata maji.

NAIBU SPIKA: Yote mawili yalikuwa ni maombi. Hayakuwamaswali. Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Sasa namwita Mheshimiwa Shaffin Amedal Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini.

Na. 90

Vipimo vya DNA Kuwekwa Kwenye Hospitali za Mikoa

MHE. SHAFFIN AHMEDALI SUMAR aliuliza:-

Suala la mimba kwa wanafunzi wa shule za mingi ni janga kubwa na mara nyingi wahusika hujinasua kupelekwa Mahakamani kwa kutokuwepo ushahidi wa kutosha au kuwatisha wazazi na watoto ambao hawana uwezo kifedha.

(a)Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwa na kipimo cha *DNA* kwenye kila hospitali?

(b)Kama mpango huo upo je, ni lini Serikali itakamilisha?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin Ahmadeli Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua janga la wanafunzi kukatishwa masomo kwa kupewa mimba na inajitahidi kutumia mbinu mbalimbali kuwabaini wanaowapa mimba wanafunzi ikiwemo teknolojia mpya ya vinasaba (*DNA*). Aidha, kutokana na gharama kubwa ya kununua na kuendesha mtambo wa *DNA*, ambayo kwa sasa gharama ya mitambo hiyo ni kiasi cha shilingi za Kitanzania kati ya milioni 600 hadi 700 na gharama za uendesaji wa mitambo hiyo ni shilingi milioni 150 kwa mwaka.

Gharama za kusomesha mtaalam mmoja wa kufanya uchunguzi kwa teknolojia ya *DNA* kwa kiwango cha Uzamili ni kati ya shilingi milioni 80 hadi 90 kutegemea na nchi. Kwa sasa kuna mtambo mmoja tu kwa Mkemia Mkuu wa Serikali hivyo kutokana na gharama hizo sio rahisi kuwa na mitambo hiyo kila

Mkoa. Aidha kutokana na gharama za ununuzi na uendeshaji wa mitambo hiyo, kiasi halisi ambacho kinastahili kutozwa kwa huduma ya uchunguzi wa *DNA* kwa sampuli moja ni shilingi 300,000/-. Kwa sasa gharama inayotozwa kwa mwananchi ni kiasi cha shilingi 100,000/- kwa sampuli hii ni kwa sababu Serikali huchangia sehemu ya gharama hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu wa Serikali ni kupeleka huduma karibu na wananchi ambapo hatua ya kwanza itakuwa ni kuimarisha maabara za Kanda za Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kununua na kusimika mitambo mipya na kutoa mafunzo kwa wataalam. Hadi sasa wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali una Kanda nne ambazo ni Dar es Salaam, Kanda ya Ziwa –Mwanza, Kanda ya Kaskazini – Arusha na Nyanda za Juu Kusini – Mbeya.

MHE. SHAFFIN AHMEDALI SUMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kipimo cha *DNA* ni muhimu sana hata kiusalama wa nchi na hata Jeshi la Polisi linaweza likanufaika kwa kutumia kipimo cha *DNA* kukamata wahalifu. Je, bado Serikali inaendelea kusema kwamba mitambo hii ni aghali sana na tunajipanga?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, Ni kweli kabisa mitambo hii ni ghali na ni kweli kabisa na inahitajika katika kila Mkoa, Lakini kutokana na unyeti na hasa unapozungumzia

masuala ya makosa ya jinai lakini kutokana na unyeti ni muhimu kuhakikisha kwamba mitambo hiyo inakuwa katika maeneo ambayo inakuwa ya ubora unaohitajika kwa ajili ya kuchunguza makosa hayo ya jinai.

Lakini vilevile siyo kosa kusafirisha sampuli kutoka eneo moja kufikisha eneo jingine kwa ajili ya kufanya uchunguzi ambao kwa hakika utapunguza gharama za uendeshaji na gharama za uendeshaji wa kesi husika. Kwa hiyo, bado hata nchi zinazoendelea wanasafirisha sampuli na siyo kosa kwa Tanzania kuendelea kusafirisha sampuli katika kipindi ambacho tunaimarisha ofisi za Mkemia Mkuu za Kanda ambazo tayari ujenzi wake umeanza. Kwa mfano Arusha, Mwanza, Mbeya kuna jengo ambalo Halmashauri ya Jiji la Mbeya ambalo limetoa na Bajeti ya mwaka 2013/2014 ukarabati utakuwa umeanza. (*Makofi*)

MHE. SAID MOHAMED MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kutokana na umuhimu wa mtambo huo wa *DNA* na kwa kuwa watu wa Lindi na Mtwara wako mbali sana na Kanda hizo zilizotajwa. Je, Serikali haioni kuw kuna haja kuwa Kanda ya Kusini badala ya sisi kwenda Mbeya kupeleka mtambo huo pale Ligula au Hosptali ya Mkoa wa Lindi?

NAIBU SPIKA: Sijui kwa nini watu wanautaka sana mtambo huu wa *DNA*.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa

Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi Serikali ina mpango wa kuziendeleza Kanda hizi nne baada ya kuwa Kanda ya Dar es Salaam imekamilika na Kanda hizi tatu zinafuata ninaamini muda na wakati utakapokuwa umefika Kanda ile ya Mtwara itapewa kipaumbele.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kwasababu ya muda na swali linalofuata ambalo linaelekezwa katika Wizara ya Maliasili na Utalii na mwuliza swali ni Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini.

Na. 91

Kupanua maeneo ya Hifadhi Kiholela

MHE. MOSHI SELEMANI KAKOSO aliuliza:-

Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa ikipanua maeneo ya Hifadhi kila siku katika maeneo mengi ya Jimbo la Mpanda vijijini kiholela bila bila kushirikisha wananchi wa maeneo hayo:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kuthamini wananchi kuliko wanyama?
- (b) Je, ni lini wananchi wa vijiji vya Kaparamsenga, Kasekese, Kungwi, Itunya (Igalukilo) watarejeshewa maeneo ambayo

yalikuwepo kwa muda mrefu na sasa yamemegwa na WMA?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii haina utaratibu au mpango wowote wa kupanua maeneo ya hifadhi kiholela. Ardhi ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyama Pori (*Wildlife Management Area*) (WMA) humilikiwa na wananchi wa vijiji husika. Wizara yangu inahusika katika kuwawezesha wananchi wa vijiji hivyo kutenga maeneo na kuanzisha WMA kwa kuzingatia Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya vijiji vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inathamini sana wananchi wake na kwa vyoyote vile haiwezi kumthamini mnyama kuliko binadamu. Sambamba na kuthamini wananchi, Serikali ina jukumu la kushirikiana na Wananchi, kuendeleza uhifadhi wa wanyamapori ili kulinda maisha na mali za wananchi pamoja na kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kunufaika na kuwepo kwa wanayamapori. Aidha, ni muhimu kuwalinda wanyamapori ili kizazi cha sasa na kijacho kifaidike nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Kaparamsenga, kasekase, Kungwi, Itunya (Igalukilo) ni miongoni mwa

vijiji wananchama vinavyounda Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori tarajiwa ya Ubende. Namwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Wananchi kukamilisha uanzishwaji wa WMA hiyo ili waweze kufaidika na rasilimali za wanyamapori kama vile uwindaji wa kitalii, utalii wa picha na kadhalika. *(Makofi)*

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa vijiji vya Kabage, Kungwi, Sibwesa, Kasekese na Kaparamsenga havikushirikishwa kwa kina kwa kuwa utaratibu unaotumika na maafisa wa WMA wanaenda wakiwaona watendaji wa vijiji na Mwenyekiti bila kuwashirikisha wananchi. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwenda kushughudia katika vijiji hivyo ili tuambatane naye ili akaone ukweli ulivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Kitongoji cha Igalukilo ni kitongoji ambacho kimekuwepo kisheria toka mwaka 2000 na wananchi wamekuwa wakihusisha katika shughuli za maendeleo kushiriki ikiwepo pia kushiriki uchaguzi na shughuli za kijamii. Leo hii Kitongoji hicho kimeamuliwa kitoke katika eneo hilo, kwa wananchi ambao wanaishi katika kitongoji hicho chenye Kaya takribani mia saba na hamsini na wananchi karibu elfu nne na zaidi wameamuriwa watoke katika eneo hilo. Je, Serikali iko tayari kuwalipa fidia wananchi hao ambao wanatolewa kwa nguvu na kuwafanya kuwa wakimbizi katika eneo husika?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana nzima ya uanzishwaji wa WMA inashirikisha wananchi. Sera ya 2007 lengo lake kubwa lilikuwa ni hilo kwa sababu zamani kulikuwa na sera ya wakoloni ambayo ilikuwa haishirikishi wananchi na ilikuwa inalenga zaidi kulinda wanayama lakini baadaye ikaonekana kuwa ni vizuri wananchi washirikishwe ili kuweza kuweka zile mali ziwe endelevu, kwa wananchi hawa kwa taarifa tulizonazo walishirikishwa kwenye jumuiya ya Ubende Vijiji 10 vilishirikishwa na baada ya kushirikishwa waliunda Kamati ya Wajumbe watatu kutoka kwenye kila kijiji na hivyo kufanya Wajumbe thelathini wa vijiji kumi vya Ubende.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Kata ya Mpimbwe ina vijiji vitano nao walitoa Wajumbe watatu kila kijiji na kufanya jumla ya Wajumbe kumi na tano. Kwa hiyo, inaonyesha kuwa walishirikishwa lakini hatua ya pili ya ushirikishwaji Baraza la Madiwani la Mpanda la tarehe 23 Mei, 2012 liliridhia uanzishwaji wa WMA kwenye vikao vyake. Kwa hiyo, nadhani kwenye baraza ambapo Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe alikuwa na nafasi nzuri sana ya kuona kama wananchi hawakushirikishwa na kutoa maoni yake pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kile kitongoji ambacho watu wameondolewa kwenye eneo hili ni suala kubwa ambalo siwezi kutoa maamuzi yake hapa.

Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge atupe taarifa kwa undani zaidi halafu tutaona namna Serikali jinsi ya kulifuatilia na kulifanyia kazi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge sasa tuhamie Wizara ya Maji naomba nimwite Mheshimiwa Israel Yohana Natse.

Na . 92

Utekelezaji wa Mradi wa Maji Karatu

MHE. CECILIA A. PARESSO (K.n.y. MHE. MCH. ISRAEL NATSE) aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa barua ya Waziri ya tarehe 11 Februari, 2010 kuhusu Mradi wa Maji wa Karatu, upembuzi yakinifu uliofanywa na Mhandisi Mshauri *BELVA CONSULTANT* na *SIR FRIEDRICK SONOW AND PARTNERS* ulishakamilika na kilichotakiwa kufanyika ni kutangaza zabuni ili kupata Mkandarasi kufikia mwezi machi, 2010.

- (a) Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi wa Karatu kuhusu utekelezaji wa Mradi huo?
- (b) Je, ni lini Serikali itaanza utaratibu wa kutoa marejesho ya taarifa kwa wananchi wake kuhusu miradi ya maendeleo inayoendelea katika maeneo yao wakiwa wadau wa kwanza katika maendeleo hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israeli Yohana Natse, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia programme ya Maendeleo ya Sekta ya maji (*WSDP*) ilifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya maji kwa mji wa Karatu Mkoani Arusha, miji ya Katesh na Orkesumet ya Mkoani Manyara chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Maji safi na usafi wa Mazingira Babati. Usanifu na uandaaji wa wa Zabuni ulikamilika mwezi Aprili, 2009 na makisio ya awali ya gharama za mradi yalikuwa shilingi billioni sita.

Matarajio yalikuwa ni kumpata Mkandarasi wa kuanza ujenzi wa mradi wa maji Karatu katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa programu. Kutokana na ufinyu wa Bajeti, mradi huo haukupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza kero ya maji kwa wakazi wa Karatu wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji Karatu, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilitenga shilingi milioni 55 zitakazotumika kuchimba kisima eneo la Bondeni Mjini Karatu. Kisima hicho kinatarajia kuzalisha maji mita za ujazo 20 hadi 30 kwa saa na kuhudumia wakazi 16,800 wa kijiji cha G-Arusha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina taratibu za kutoa marejesho ya taarifa za utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa wananchi wake katika maeneo

yao kila robo mwaka na mwisho wa mwaka. Mamlaka za Maji au Vyombo vya watumia maji katika maeneo husika ni wadau na watoa huduma ambao hushirikiana na Serikali kutoa taarifa hizo.

Watendaji katika ngazi hizo watawajibika kutoa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao. Kwa utaratibu huo na kwa kuwa *Karatu Villages Water Supply. (KAVIWASU)* ndiyo chombo kinachoendesha na kusimamia huduma ya maji katika mji wa Karatu, kinawajibika kutoa taarifa kwa wananchi kwa kushirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya. *(Makofi)*

MHE. CECILIA A.PARESSO: Mheshiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi na nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa lengo la mradi ilikuwa ni kuchimba visima kumi na shilingi milioni hamsini na tano zilizopelekwa zinachimba kisima kimoja bila kujumuisha gharama za umeme, *pipe line na tank.*

(a) Je, Serikali ina dhamira ya kweli na kwa vipi katika kutekeleza au kukamilisha kisima hicho?

(b) Kwa kuwa, mradi huo ulianza mchakacho mwaka 2008 na kufanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2009 na sasa ni miaka mitatu na inaoneka hakuna dhamira ya dhati kutekeleza mradi huo. Je, Serikali ina mkakati gani endelevu kutekeleza mradi huo katika mwaka wa fedha unaoanza julai?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Shilingi milioni hamsini na tano zinazotolewa sasa hivi ndiyo zinazotolewa sasa

hivi ndiyo zinaingizwa kwenye *account* za Halmashauri ya Karatu ili ziweze kusaidia hatua za haraka za kusaidia hatua za haraka za kupatikana maji kwa maana ya kuboresha miundombinu iliyopo ili kuongeza idadi ya visima vya maji.

Lakini kuhusu vile vijiji kumi vilifanyiwa utafiti na ikaonekana kwamba ni visima 8 ndiyo vinaweza kutoa maji. Sasa kutokana na fedha mwaka huu tumeingiza kijiji kimoja cha gatemoock ambacho kimetengewa milioni mia tatu themanini na tano kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

leleweke kuwa vijiji ni vingi kwa hiyo, tuna gawana *resources* kulingana na uwezo uliopo. Upo mkakati wa upelekaji maji vijijini ambapo sasa hivi tumefanikiwa Halmashauri sitini kupata *no objection* kutoka *bank* kwa hiyo, tukishamaliza na wakipata wote zile *no objection* vikiwemo vile vijijini vingine ambavyo vimebaki kwenye Halmashauri hii ya Karatu tutaendelea na awamu ya pili ambayo itaanza 2013/2014 kwa ajili ya kupeleka maji kwenye sehemu zilizobaki. Tunamuomba Mheshimiwa Mbunge watusaidie kupitisha Bajeti hii ya Wizara ya Maji hapo itakaposomwa ili tuweze kutekeleza miradi ya awamu hii na tukitekeleza mwaka ujao tufanye mingine ambayo itakuwa imebaki.

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Jafo swali dogo la nyongeza.

MHE. SULEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Kisarawe tulichimba visima vya

miradi ya *World Bank* na bahati nzuri pale Kihale, Chakenge, Boga na Msanga tulipata maji ya kutosha katika maeneo hayo, lakini visima vile mpaka hivi sasa vimefunikwa bado usambazaji haujafanyika.

Je, nini mpango wa Serikali kuja Wilayani Kisarawe kuja katika vile visima vya *World Bank* ambavyo vina maji kuja kufanya utaratibu wa kuweka miundombinu ili maji yale yaweze kuwafikia wananchi wa Kisarawe ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna visima vingi vimechimbwa siyo Rufiji tu ni karibu Tanzania nzima zaidi ya visima mia tisa hamsini na moja na vipo visima mia sita na zaidi ambayo vimepatikana na maji. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa siwezi kujua idadi ya visima ambavyo kwake tayari Serikali imetoa pesa apitishie Bajeti yetu ili vile ambavyo vimepitishiwa vianze kutekelezwa na wananchi wapate maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leticia Nyerere, swali la mwisho kwenye eneo hili.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niulize swali. Tatizo la maji limekuwa ni janga kubwa katika Mkoa wa Mwanza, asubuhi hii nimepokea ujumbe kutoka kwa wananchi wa Ngudu Mjini, Kilaboya, Ngh'ungumalwa, Mwamashimba, Mwankulwe, Jojilo na Kadhalika naomba nikusomee ujumbe huu: *"Tumechoka na porojo za Serikali kuhusu*

tatizo la maji sisi ni Watanzania kama Watanzania wengine tunataka maji yetu". (Vicheko)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyerere. Ni kwamba tumeshapewa taarifa hizi kupitia Waheshimiwa Wabunge wa Bukwimba kuhusu matatizo ya maji ya mwanzo tutazifuatilia na kuona namna ya kuzitatua.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hili ni swali la mwisho kwa siku ya leo kama mnavyoona muda wetu, linaulizwa na Mheshimiwa Zabreena Hamza Sungura.

Na. 93

Kuimarisha Mazao ya Mawese, Alizeti, Karanga na Pamba

MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA aliuliza:-

Tanzania inatumia takribani tani laki tatu za mafuta ya kula kutoka nje sawa na 55% ya mafuta yote yanayotumika nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha mazao ya mawese, alizeti, karanga na pamba ili kupunguza wimbi la mafuta kutoka nje.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya mafuta ya kula hapa nchini ni wastani wa Tani 330,000 kwa mwaka. Asilimia 60 ya mahitaji hayo yanatoka nje. Mafuta haya ya ndani yanatokana na mbegu za alizeti, pamba, michikichi, karanga, ufuta, soya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mipango na mikakati ya kuendeleza mazao ya mbegu za mafuta ili kuimarisha tija na uzalishaji wa mazao haya ili kupunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi. Kwa sasa uzalishaji wa mbegu za mafuta umeongezeka kutoka wastani wa tani 895,920 mwaka 2005/2006 na hadi tani 2,415,880 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mipango na mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuandaa na kutekeleza mipango ya kuendeleza zao husika kupitia miradi kama vile *ASDP/DADPs*, *DASIP* na miradi ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kama vile *TACARE*, *CARITAS* na *TCRS* kwa zao la michikichi/mawese.

(b) Kuimarisha utafiti wa mazao ya mbegu za mafuta kupitia vituo vya utafiti hapa nchini. Mfano ni kituo cha Naliendele kwa mazao ya karanga na ufuta na llonga kwa zao la Alizeti na kuandaa mikakati na

programu (*Specific Strategies and Programmes*) ya kuendeleza kila zao lenye malengo ya kupimika.

(c) Kutoa ruzuku ya mbegu bora kwa zao la alizeti hususani katika Mkoa wa Singida. Mfano mwaka 2010/2011 shilingi 30 milioni zilitumika kwa ajili ya mbegu za alizeti Mkoani Singida. Matokeo ya Ruzuku hiyo ni kwamba uzalishaji wa alizeti umeongezeka kutoka Tani 68297 kwa mwaka 2007/2008 hadi Tani 82484.9 kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine ni pamoja na kuondoa ushuru wa uingizaji wa mitambo na mashine za kukamulia mafuta ili kuwahakikishia wakulima soko na kuimarisha upatikananji wa mbegu bora kupitia Wakala wa Mbegu wa Taifa. (*Makofi*)

MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, Mkoa wa Kigoma una hekta takribani milioni mbili laki sita na kidogo kwa ajili ya kilimo. Lakini katikahekta hizo ni aslimia ishirini na nne tu ndiyo inayotumika kwa kilimo na kwa kuwa Mkoa wa Kigoma wakazi wake wanategemea asilimia themanini na mbili ya ajira zake kutoka kwenye kilimo. Je, Serikali iko tayari kupima maeneo na kutoa Hati Miliki kwa wananchi ili wawe na sifa za kukopesheka?

(b) Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la uchakachujaji wa mafuta hususani katika mikoa ya Pwani inasemekana kwa wale walaji wa *chips* mafuta

ya *transfoma* yanachanganywa na mafuta ya korie. Je, Serikali sasa iko tayari kuhamasisha mazao haya ya Alizeti, Pamba, Ufuta na Mchikichi katika mikoa ya Pwani ili kukabiliana na uchakachuaji huu wa mafuta ya *transfoma*?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kigoma ina maeneo kama hekta milioni mbili lakini hilo wenyewe watu wa Kigoma kwenye *RCC* yenu mmetenga maeneo hayo kwa ajili ya kulima mazao mbalimbali, moja ninavyofahamu ni kulima kilimo cha miwa.

Sasa hiki kilimo cha mawese kinaweza kikastawi kwa njia ya *contract farming* na kwa maana unavyosema ni kwamba wakulima wadogo wadogo wahusishwe moja kwa moja lakini apatikane mwekezaji ambaye atawapa soko wakulima wadogo wa kulima michikichi hii. Kwa sababu mchikichi mmoja kwa mfano ule mkungu ukiwa kilo thelathini unatoa mafuta kama lita tatu mpaka lita nne.

Kwa hiyo, fikra iliyokuwepo ni kwamba wadau kwa kila kaya mtu ukiwa na michikichi yako minne mitano kwa kila kaya mnaweza mka-*boost demand* ya kuwa na *industrial production* ya mawese pale Kigoma. Kwa hiyo, hili jambo la uwekezaji kwa maana ya kuhamasisha mwekezaji aje kuwekeza kwenye zao la michikichi pale itategemea pia ushirikiano wa sisi viongozi moja kwa moja kuhamasisha wakulima wa zao hili wajue kwamba hata katika mazingira ya kaya unaweza ukawa na michikichi yako

minne, mitano na sisi wote kwa pamoja tukafikisha mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kupima maeneo mimi nadhani liko Wizara ya Ardhi na kwa sababu ni moja wamenisikia na wao watalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili swali la pili la wachakachujaji wa mafuta ya *transfoma* wa mikoa ya Pwani, hili linanipa taabu kidogo kwa sababu mimi mwenyewe ni mwenyeji wa Mkoa wa Pwani na uzoefu wangu nilipokuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini tulishindwa kuthibitisha kama kweli mafuta ya *transfoma* yanatumika kupikia *chips*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba kwa swali ulivyojielekeza kwamba tuangalie namna ya kuhamasisha wawekezaji wa mafuta ili mbegu zetu za mafuta na vyanzo hivi vya rasilimali za hapa nchini zitumike kuzalisha mafuta na kupunguza ile *dependence* ya mafuta kutoka nje. Hili Serikali tunalifanyia kazi na nafikiri kuongezeka kwa mbegu za mafuta kwa miaka hii mitano inathibitisha kwamba tunakwenda vizuri.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana tumefikia mwisho kwa sababu ya muda naomba tuendelee na nianze na matangazo ya wageni waliopo katika ukumbi katika *gallery* mbalimbali.

Kuna wanafunzi hamsini kutoka shule ya sekondari ya Bihawana pamoja na walimu wao, simameni pale

mlipo, karibuni sana wanafunzi hapa Bungeni, Waheshimiwa Wabunge msiojua Bihawana ilipo siyo mbali sana ni umbali usiozidi kilomita ishirini kutoka hapa barabara ya Iringa lakini unachepuka kidogo mkono wa kulia. Karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Pia kuna kikundi cha akina mama 35 kutoka *Redeemed Assemblies of God*, karibuni sana akina mama kutoka Kanisa hili tunawakaribisheni Dodoma lakini kipekee tunawakaribisha kwenye Bunge letu karibuni sana mjisikie mpo nyumbani. Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Godfrey Zambi ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao wanatoka Jimbo la Mbozi Mashariki, karibuni sana popote pale mlipo na niwahakikishie Mheshimiwa Godfrey Zambi yeye ni Kamishna wa Tume ya Huduma za Bunge, lakini vile vile ni Mbunge anayetetea sana maslahi ya Mbozi Mashariki, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mgeni wa mwisho ni Dkt. Salum Ibrahim Mwandu, Mwenyekiti wa Bodi ya Hospitali ya Rufaa ya Morogoro ni mgeni wa Mheshimiwa Stephen Julius Masele, karibu sana Dkt. Mwandu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge matangazo ya kazi ni kama yafuatavyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba wajumbe wa Kamati yake ambayo ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ikutane saa saba mchana leo, Ukumbi Namba 231.

Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Waziri Mkuu imeleta *addendum* ambayo natumaini kila mmoja ameipata mezani kwenu ni vizuri mkaipitia ili katika kujadili hotuba ya Waziri Mkuu basi mkaona marekebisho yaliyofanywa ukurasa wa 75 kuhusiana na aya mbalimbali na mafungu mbalimbali. Ni muhimu sana kwa sababu baadhi yake yanahusu Bunge letu lenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho niwaombe kwamba wengi wetu tunaposafiri kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na tunapotoka Dodoma kwenda Dar es Salaam tunapopita maeneo ya Kongwa pale tunayo *Kongwa Ranch* ni shamba letu wenyewe Watanzania ni shamba la Taifa, tunaomba kuna nyama pale ni *Grade One* kabisa Kongwa *Beef*. Mheshimiwa Mbunge yeyote unapopita chepuka tu dakika mbili, ingia pale pata nyama ambayo ni safi kabisa na ni ya kiwango chake nchi nzima. Tunaomba pia maafisa wa Serikali wanapopita kuboresha shamba letu la Taifa ili liendelee kuwepo. Karibuni sana na bei yake ni bei poa kabisa na unapata kiwango unachohitaji na kipindi hiki cha Bunge kwa sababu tunakuwepo hapa muda mrefu kama utahitaji kiwango kikubwa zaidi cha nyama tuwasiliane tu. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kumalizia ninaomba nichukue dakika yenu moja niwakumbushe kidogo kuhusu masuala yanayohusu utaratibu yanayoendana na Kanuni ya 68 ambayo Wabunge wengi sana tunapenda kuitumia kwa maneno yale matatu ambayo tumeyazoea sana hapa Bungeni. Kwanza ni

kuhusu utaratibu ambao unaweza ukaombwa na Mbunge yeyote wakati mwingi na wakati wowote, lakini jikumbushe kwamba ukitaka kuzungumzia habari ya utaratibu ni lazima ujiandaye kutaja Kanuni na jambo la utaratibu ni lazima lihusiane na jambo fulani ambalo limekiukwa humu ndani. Kwa hiyo unataka kusaidiana na meza kujaribu kuliweka sawa kwa kumtaka Mwenyekiti au Spika akiwa hapa kufafanua endapo jambo hilo linaendana na utaratibu ulioruhusiwa kikanuni.

Ukisimama kuhusu mwongozo inapaswa iwe kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika afafanue kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi, ukisimama kuhusu taarifa mara nyingi kama siyo mara zote utakuwa unampa taarifa Mbunge ambaye wakati huo anaongea na baada ya taarifa yako ninaweza nikampa nafasi aseme kama anaikubali au anaikataa. Lakini katika mambo yote haya ya utaratibu maamuzi ya meza yanakuwa ni ya mwisho.

Maana kuna baadhi ya Wabunge wanapenda tuendeleo kubishana kuhusu mambo ambayo Kanuni imetoa mamlaka kwamba kiti kikishaelekeza basi hatuendelei kubishana tunasonga mbele na mambo mengine. Baada ya matangazo hayo basi namwomba Katibu atuelekeze ni nini kinafuata.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mwongozo ni mmoja tu, Mheshimiwa Kamishna Zambi.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68 (7). Tarehe 22 Juni, 2012 Waziri wa Afya Dkt. Hussein Mwinyi alitoa taarifa hapa Bungeni kuhusiana na madai ya Madaktari na uboreshaji wa maslahi yao karibu katika hospitali zote nchini. Lakini alitoa kauli hiyo pia kufuatia tishio la madaktari nchi nzima kugoma na kwamba walitarajia waanze mgomo tarehe 22 Juni, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru taarifa ya Serikali ilitolewa vizuri, lakini kuanzia Jumamosi iliyopita madaktari bila kujali taarifa ya Serikali wameendelea na mgomo katika hospitali karibu zote za Rufaa nchini.

Leo asubuhi nimeongea na baadhi wa watumishi wa hospitali ya Taifa ya Muhimbili wamenithibitishia kwamba mgomo upo ni madaktari mabingwa wachache tu ambao wanahudumia wagonjwa, nimeongea na Madaktari kule Mbeya wamenithibitishia kwamba mgomo upo na taarifa hii naweza nikakusomea inatoka kwa Daktari mmoja inasema kwamba, mgomo upo na unaendelea tangu Jumamosi, tarehe 23 Juni, 2012 na hii imetoka kwa madaktari wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua suala hili katika taarifa ya Serikali lilishapelekwa mahakamani baada ya pande mbili hizi kushindana. Madaktari hawa bila kujali hatua za Serikali bado wameendeleza mgomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo ninaoumba hapa ni kwamba katika hali kama hii ambapo suala hili lipo Mahakamani, Madaktari wanagoma, wagonjwa na Watanzania wetu wanaendelea kupata taabu, Serikali sasa inachukua hatua gani kwamba hili jambo liko mahakamani maana hatuwezi kunyamaza jambo liko mahakamani Watanzania hawa wanaumia, Serikali sasa inaweza ikatoa taarifa gani ya ziada juu ya jambo hili ingawa tunajua kwamba liko mahakamani hatuwezi kulijadili na mimi nisingeomba Wabunge waniunge mkono kwa maana ya kusimama ili lijadiliwe kwa sababu liko mahakamani. Hatua gani za ziada Serikali inawaambia Watanzania juu ya jambo hili. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu nimekuona.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, pengine kabla hujatoa mwongozo huo kama alivyosema Mheshimiwa Zamboni labda tungetoa maelezo mafupi ili utakapotoa basi uweze kuwa katika picha kamili. Ni kweli kwamba Serikali ilitoa tamko hapa Bungeni, lakini ni kweli vile vile kwamba nilikuwa nimekwishalieleza Bunge lako Tukufu kwamba baada ya kutofautiana katika majadiliano ilibidi turudi kwenye chombo cha kisheria ambako tulikuwa tumeanzia kwenda kutoa taarifa kwamba kuna maeneo hatujaridhiana. Kwa CMA ambacho ni chombo cha kisheria kikaamua kwamba jambo hili ni vizuri sasa liende katika Mahakama Kuu katika *Division* ile ya Kazi. Kwa hiyo, tumekwenda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 22 Juni, 2012
Mahakama ilitoa amri ikiwataka Madaktari wasigome,
wasitishie mgomo na kwamba waende wakatangaze
kwenye vyombo vya habari kwamba sasa mgomo
hautakuwepo.

Mtakumbuka katikati hapo tukawa na *weekend*
tulichofanya Serikalini tukaendelea kuona kama
itatekelezwa, jana tumelazimika tena kurudi
Mahakama Kuu, Mahakama Kuu ikatoa amri ikiagiza
amri iliyotolewa tarehe 22 itekelezwe na wakaagizwa
waede wakatoe taarifa kwenye vyombo vya habari.
Wale mtakaokuwa mmeona jana kwenye runinga
mtakuwa mmeona jambo hili limejitokeza kama taarifa
likieleza jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama
alivyosema Mheshimiwa Zamboni, lakini nataka niwasihi
sana Wabunge kwamba tungeweza kwa kweli
tukachukua hatua stahiki wakati ule ule tulipokuwa
tumedhamiria kufanya hivyo, lakini tulichelea kufanya
hivyo kwa kuheshimu taratibu hizi za kisheria kwa
sababu tulijua Mahakama Kuu inatekeleza wajibu
wake tukafikiri siyo vizuri chombo hiki, Muhimili mmoja
kuonekana kwamba mnataka kuingilia taratibu
ambazo ni za msingi sana. Kwa hiyo, rai ya Serikali
hapa ni Madaktari kuheshimu hiyo amri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana ndani ya
Serikali kwamba tutatoa kauli hapa Bungeni kesho
kueleza sasa Serikali baada ya hatua zote hizi
imeamua kuchukua hatua zipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama ni jitihada kwa kweli tumefanya kubwa sana, lakini tunaona pengine dhamira haipo. Kwa hiyo, tumeona na sisi kesho tuli arifu Bunge lako Tukufu ili waswahili wanasema na litakalokuwa na liwe. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mnyika unapandia hapo, kwa sababu bado tunashughulika na jambo moja *at least* tufike mahali halafu kama kuna jingine basi tutaendelea. (*Makofi*)

Kuhusu suala la madaktari nafikiri ufafanuzi wa Waziri Mkuu unatosha kabisa na kama alivyoomba Mheshimiwa Zambzi kwamba Serikali ije hapa Bungeni itueleze Serikali imesema itakuja kesho. Kwa hiyo hapo hakuna maneno.

Waheshimiwa Wabunge nilitaka tu kusemea kidogo kuhusu ule ufafanuzi wangu wa mwanzo kuhusu matumizi ya mwongozo ambayo Mheshimiwa Zambzi alitumia vizuri tu kwa suala la tarehe 22 Juni, 2012 ambapo Waziri wa Afya Dkt. Hussein Mwinyi alisoma taarifa ya Serikali. Kanuni inasema mwongozo utahusu jambo, ambalo limetolewa Bungeni mapema. Sasa hapa huwa kuna mtihani kidogo mapema maana yake nini. Uli tarajia kanuni iseme mapema siku hiyo lakini ikaishia mapema, ndiyo maana mtu hata akiuliza tarehe 22 atakuwa bado yupo kwenye mapema ile ile, siku zijazo mtatushauri hii kanuni ikae namna gani ili tuibane kidogo au iendelee kuwa imekaa wazi namna hii.

Haya Mheshimiwa Mnyika ulitaka kumpa taarifa sijui nani.

KUHUSU TAARIFA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kumpa taarifa Mheshimiwa Zamboni na Waziri Mkuu. Ningeomba uniruhusu sitasoma lakini niseme tu kwa mujibu wa taarifa zilizomo kwenye vyombo vya habari ni kwamba kesi iliyopo mahakamani imeshtakiwa *MAT* ambacho ni Chama cha Kitaaluma cha Madaktari, lakini Jumuiya ya Madaktari ambayo ndiyo inatoa kauli za mgomo na mambo mengine haijashtakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kutoa taarifa kwamba nimeandikia ofisi yako kuiomba kwamba kwa kuwa ulielekeza Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ikafanye kazi ya kukutana na hizi pande mbili ni vizuri tusipokee taarifa ya upande wa Serikali peke yake, tupokee vile vile taarifa rasmi ya Kamati ya Bunge iliyofanyia kazi suala hili ili tuweze kufanya maamuzi tukiwa na taarifa zilizokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni taarifa hiyo.
(*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate mwongozo wako kuhusiana na hicho ambacho Mheshimiwa Mnyika amesema ni taarifa. Alisimama kwa mujibu wa fasili ya 8, fasili ya 8 inasema: Vile vile Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa na kwa ruhusa ya Spika atatoa taarifa au ufafanuzi kwa Mbunge anayesema ambapo Spika atatamtaka Mbunge anayesema aketi kusikiliza taarifa hiyo.

Mheshimiwa Godfrey Zamboni alikuwa ameketi amemaliza kusema aliyokuwa ameyasema, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa amemaliza kuyasema aliyoyasema ameketi. Haiwezekani ukatoa taarifa wakati aliyekuwa anasema ameshaketi. Naomba mwongozo wako kama tafsiri hiyo na matumizi ya Kanuni ya taarifa kama ilivyotumiwa ni sahihi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mimi ninachoshukuru ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote tunazidi kujifunza kuhusu matumizi ya vipengele mbalimbali. Nawashukuruni nyote, ila niseme kwamba, kuhusu jambo hili Serikali itakuja kesho kutueleza hapa Bungeni nini kinachoendelea. Tupe nafasi Serikali. Tukumbuke kwamba jambo hili lipo Mahakamani, awe anashtakiwa nani, lakini kesho itakuja kutupa maelezo yake Bungeni. Kwa hiyo, naomba tuwe na subira hadi kesho tuweze kuelewa kuhusu jambo hili.

Kuhusu Kamati ya Huduma za Jamii, ilishalishughulikia jambo hili hili na ikatuletea taarifa hapa. Sasa Kamati irudi kufanya nini? Labda pawe na mazingira mapya lakini jambo lenyewe ni mwendelezo

wa jambo hili hili ambalo lilikuwa linaendelea. Tusubiri maelezo ya Serikali kesho, kama kuna kinginecho kitafuata baada ya kuisikiliza Serikali.

MBUNGE FULANI: Anataka posho.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 – Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, naomba tuzingatie muda kwa wale ambao wanapata fursa kwa sababu kama nilivyowaambia wachangiaji wangu ni wengi, kwa hiyo, naomba mjikite moja kwa moja katika hoja na anaanza Mheshimiwa Victor Mwambalaswa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu kwa kutoa mfano kidogo; natoa mfano kutoka katika Biblia, Kitabu Kitakatifu. Bwana Yesu alipoanza kufanya kazi zake na kuonesha utukufu wake na ukuu wake, alizunguka sana Galilaya na Wanafunzi wake, baadaye akapanda mlimani na wanafunzi wake. Huko Mlimani aliwafundisha mambo mengi sana, hata namna ya kuomba aliwafundisha huko mlimani. Sasa

aliposhuka kutoka mlimani mtu wa kwanza aliyekutana naye ni mwenye ukoma, mwenye ukoma akamfuata Bwana Yesu; Bwana Yesu naomba unitakase ukitaka, Bwana Yesu akamgusa akasema nataka na utakasike. Yule mtu ukoma ukapona. Mtu wa pili kuonana naye ndiyo mfano ninaoutaka sasa hapa alionana na Akida, Akida alimfuata Bwana Yesu, Akida wa enzi hizo ni Mkuu wa Wilaya wa enzi hizi au Mkuu wa Mkoa. Huyu Akida akamfuata Bwana Yesu akamsihi Bwana Yesu nakusihhi sana, nina mtumishi wangu anaumwa amepooza siku nyingi naomba uniponye. Mtumishi, Bwana Yesu akamwambia vyema nitakuja nimponye akasema ahaa, mimi sistahili wewe uingie ndani ya gari langu, wewe sema neno moja tu huyu mtu atapona ni kama nilivyo mimi nina maaskari chini yangu, nina watumishi chini yangu, nikisema askari nenda huko anakwenda, nikisema njoo anakuja, nikisema mtumishi fanya hivi anafanya na wewe fanya hivyo tu atapona.

Bwana Yesu alimshangaa sana yuke Akida (Mkuu wa Wilaya), alishangaa sana imani yake. Akasema amini amini, nawaambia wanafunzi wake hakuna mwenye imani kama hii katika Israel yote. Mimi ninamshangaa huyu Akida kwa kuwatumikia wananchi ambao siyo ndugu zake, siyo wajomba zake, siyo dada zake, kuwatumikia huyu ndiyo Kiongozi wa hawa wananchi, huyu ndiyo kiongozi ambaye Mwalimu Nyerere alimtaka awe Kiongozi wa Umma anayewajali wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi ilikuwemo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 – 2010,

kilomita 115 Mbeya – Chunya – Makongorosi. Aliifungua Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2008, mpaka leo kuna madaraja mawili au matatu tu yamejengwa, hakuna hata kilomita ya lami. Sisi Wananchi wa Chunya tunaona kama tunabaguliwa.

Tunadhani kuna matatizo makubwa mawili; la kwanza, labda wanaopanga Miradi hii wanaanzisha Miradi mipya kila mwaka, wakati uwezo ni mdogo. Kwa hiyo, kuimalizia Miradi hii inakuwa vigumu. Tunaiomba Wizara inayohusika, *please, clear the backlog*. Maliza Miradi iliyoanza kwanza halafu ndiyo uanze Miradi mipya, maana mingine inakuwa kama mchezo tu. *(Makofi)*

Sisi Wananchi wa Chunya tunadhani tatizo la pili labda kwa kuwa sisi tuko pembezoni, tuko nyuma, basi fedha ikipatikana inagawiwa Miradi mingine ambayo hata imeanza kujengwa nyuma yetu. Kwa hiyo, tunaomba Viongozi wanaohusika hapo wawe kama Akida huyu, wawatumikie wananchi ambao siyo ndugu zao hata wa Chunya, watumikieni wajengeeni barabara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Chunya wana uchungu sana na barabara hii. Naomba uniruhusu nilie kidogo kuonesha uchungu wao ulivyo.

WABUNGE FULANI: Ahaaa!

NAIBU SPIKA: Hapana Mheshimiwa Mbunge, Kanuni inakukataza usilie. *(Makofi)*

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nafuata Kanuni. Ninayotaka kusema, nataka Wizara inayohusika itupe maelezo ya kutosha kuonesha kwamba barabara hii itaisha kabla ya kipindi hiki cha Ilani cha kutoka mwaka 2010 - 2015. Kama hawatatoa maelezo ya kutosha, sitaunga mkono Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008 Serikali iliamua kwa makusudi mazuri sana kupima ardhi kwa wananchi ili wananchi wapate hati za kimila, waweze kumiliki ardhi na waweze kukopesheka. Sasa walikuja Chunya wamepima kuanzia mwaka 2008/2009 mpaka leo hii hakuna hata hati moja iliyotoka Chunya, yale yale ya Akida! Wilaya zingine kama Mbozi kuna hati 25,000 zimepelekwa, Chunya hata hati moja hakuna. Wanasema sijui Afisa Ardhi Mteule, mara kaenda Dar es Salaam hayupo, mara amekwenda huku; jamani Chunya mbona mnatufanya hivi kwa nini? Naomba Wizara inayohusika itupe maelezo ya kutosha kwa nini Chunya hata hati moja ya kimila haijatoka mpaka leo licha ya kwamba walianza kupima mwaka 2008? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado naongelea Chunya tu, ukisoma *Volume III* ya Bajeti ya Serikali, yale makadirio ya Mkoa, Chunya katika Mkoa wa Mbeya asilimia 46 ambayo ni sawa sawa na 50 kieneo, ndiyo Wilaya ya Chunya. Asilimia 46 kieneo Mkoa wa Mbeya ni Wilaya moja ya Chunya, lakini wameona kutoa fedha za Utawala hata za mafuta Chunya ipo chini kuliko Wilaya zingine; utakuta Chunya milioni 15, lleje

milioni 20, Kyela milioni 20, wakati ukubwa wa Chunya ni asilimia 50 ya Mkoa wa Mbeya. Katika hili sisemi kwamba bajeti ijayo namwomba Mheshimiwa Waziri ufanye marekebisho, *total* ibaki ile ile lakini mwenye eneo kubwa la kiutawala apate hela ya mafuta nyingi ya kutosha kuliko mwenye eneo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nipo Chunya; mwaka 1995, Serikali ilipiga marufuku kilimo cha pamba Chunya kwa sababu ya mdudu funza mwekundu, wakasema Wizara ya Kilimo inafanya utafiti kumwangamiza huyu funza mwekundu. Tangu mwaka 1995 na sasa ni 2012 Wananchi wa Wilaya ya Chunya wamepewa mazao mengine mbadala ya kulima ufuta na alizeti, lakini siyo kama walivyozoea kulima pamba na pamba ya Chunya ni nzuri sana. Wenzetu wa Zambia, Zimbabwe na Msumbiji wanalima, Chunya tunasema utafiti unaendelea. Jamani utafiti gani huu au ni ile ile tu ya Chunya? Naomba Waziri anayehusika atupe maelezo ya kutosha kwamba sasa Chunya tutaanza lini kulima pamba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, sasa hivi huu ni Msimu wa Zao la Tumbuku. Makampuni ya ununuzi yameanza yananutua tumbaku huku, lakini nimepata taarifa kuna masoko mengine makampuni ya tumbaku yameanza kuwalalia wakulima. Kilimo cha Tumbaku kinaanza mwezi wa nane mpaka wa nne, wakulima wanatabika sana. Anapokuja mtu kuwalalia wakulima wamwogope Mungu. Nimepata taarifa kwenye Masoko ya Matwiga na Masoko ya Mamba kuwa, Makampuni haya ya Tumbaku yanawalalia

wakulima wangu. Nawaombeni sana, Serikali iingilie kati na makampuni yamwogope Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee la mwisho kuhusu Matumizi ya Serikali. Nimefurahishwa sana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, ameamua kuanza kubana Matumizi ya Serikali hasa katika magari. Kwanza, nilifurahi sana pale ambapo Mheshimiwa Waziri nadhani alinunuliwa VX akaikataa akaamua kuchukua GX, anaonesha kwa matendo kwamba mimi nataka kupunguza Matumizi ya Serikali; safi sana. Nilimwambia ningemletea debe la asali, sijamletea lakini nitamletea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya Serikali kutamka hadharani kwamba matumizi ya magari Wizarani itakuwa kati ya CC 3000 kwa Viongozi Wakubwa na CC 2000 na CC 1500 kwa Viongozi wengine, naona kama vile *Land Cruiser Prado* ndiyo hiyo CC 3000, ni *four-wheel drive*, ni *comfortable*. Kwa hiyo, Viongozi wakubwa kwenye Wizara watumie gari hilo. Haya magari mengine yaliyopo, kila Wizara sasa ichukue hatua madhubuti ya kupiga mnada ili tununue magari ya CC 3000 au CC 1500. Wenzetu wamefanya, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya, Serikali ya Kenya ilifanya, sasa hivi Viongozi wote wanatumie *Volkswagen Passat*. Serikali ya Malawi imefanya, Serikali ya Zambia wamefanya wanatumia Prado ya Mkonga na Serikali ya Rwanda imefanya jamani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulizoea kwamba, Tanzania ndiyo ya kuigwa kila jambo, ilikuwa

Tanzania ndio ya kuigwa, siku hizi sisi ndiyo wa kuiga. Sasa tunasema Malawi wamefanya na Msumbiji wamefanya. Naomba kila Waziri apunguze matumizi katika Wizara yake kwa kupiga mnada magari haya na kununua magari ambayo yamesomwa kwenye Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo imetokea tabia fulani hapa kwa Viongozi kujiuzia magari ya Serikali. Sheria inasema unanunua kwa *tender*, hata ku-*dispose* kwa *tender*. Siyo kujiuzia, tena Mkuu wa Mkoa alikuwa anatumia gari, sijui muda wake umeisha anajiuzia yeye mwenyewe, *that is wrong*, siyo vizuri. Naomba Mawaziri wote mnapo-*tender* hili acheni *Government Procurement Agency* ifanye mnada kwa niaba yenu halafu mnunue magari mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Idara moja tu katika Serikali; Idara ya Usalama wa Taifa, wao magari yote ambayo yamekwishakutumika wanaweka mahali ili baadaye wapige mnada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja hii mpaka nitakapopata majibu ya Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, ahadi ya debe la asali itabidi ipitie kwangu, utekelezaji wake.

MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie angalau kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Muumini wa Utawala Bora. Ninapoona Utawala Bora haufuatwi inaniumiza sana. Tuna utaratibu wa kuajiri na kufukuza na kuna mamlaka zinazohusika katika kazi hizo. Mawaziri ambao kazi yao ni Sera (*Policy*), wanapoingilia kufukuza wafanyakazi siyo sawa. Kwa hiyo, ni vizuri utaratibu wa Wafanyakazi wa Serikali ufuatwe kama ilivyokuwa tangu zamani. (*Makofi*)

Mimi nakumbuka zamani wakati wa Awamu ya Kwanza, iliwahi kutokea wafanyakazi wakaanza kufukuzwa kwenye *radio*, unatoka unafukuzwa kwenye *radio* watoto wanakuja unaambiwa umeshafukuzwa kazi; kwa kweli tuliyumba na tukaacha mtindo ule. Katika Utawala Bora, kuendesha Serikali kwenye magazeti siyo sawa. Kwa hiyo, ningepomba hilo lifuatiliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mimi natoka Moshi, Moshi ni Mji wa zamani sana, ulikuwa unaunganishwa na reli ya kutoka Tanga kuja Moshi na hii reli ilikuwa ya kwanza katika *East Africa* iliyojengwa na Wajerumani waliokuja Afrika. Reli ile imeachwa kabisa imekufa. Tunang'ang'ania kwenda kujenga reli zingine. Tunajua kujenga upya, lakini hatujui kukarabati vile tulivyonavyo. Kwa kweli ni mwendo mbaya ambao hautatupeleka mahali pazuri, tutakuja kukuta tunaingia kwenye matatizo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Moshi ni Mji wa Watalii, tunapokea Watalii siyo chini ya 50,000 kwa mwaka, wanaokuja kupanda Mlima wa Kilimanjaro, lakini Mji huu hauna maendeleo yoyote. Mji wa Moshi karibu utakuwa kama *Host Town*, hauvutii tena kama ulivyokuwa unavutia zamani. Kimaendeleo, umerudi nyuma kuliko Miji mingine ya Tanzania. Tunaona unazidi kuharibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia hili labda nimzungumzie na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi. Ule Mji sasa unajengwa ovyo, kila mtu anajenga bila kufuata utaratibu. Tulikuwa na utaratibu wa kusema kuna *Master Plan* ya Mji wetu, ilikuwa katikati ya Mji lazima zijengwe nyumba za ghorofa hakuna kujenga nyumba ndogo ndogo. Sasa hivi Mkurugenzi anaachia hata maamuzi ya Baraza hayafuatwi na Mkurugenzi. Tumechoka na Mkurugenzi huyu. Watu wa Moshi wamechoka na Mkurugenzi ambaye hafuati utaratibu, hatimizi matakwa ya Baraza, anafanya anavyotaka na vyombo vyote vinavyohusika nimeshajaribu kuwaambia. Nilifika mpaka TAKUKURU kwa sababu kuna maneno ya kwamba hizi zinajengwa kwa rushwa. Kwa sababu kama kuna sheria na sheria haifuatwi hivi nini kinatumika; ni lazima kuna rushwa. Hata TAKUKURU hawachukui hatua. Mji unaharibika ule. Tumejaribu kuzuia kwa nguvu zetu zote ili pawe na amani kwa sababu Mji ukiingia vurugu na ule ni Mji wa Watalii, tuta-*disturb* watalii wetu na itakuwa ni jambo baya. Kwa hiyo, tumejaribu kuzuia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba na Serikali nayo ione, huyu Mkurugenzi atatuletea vurugu, maana leo nalisema hapa baadaye zisije zikatokea vurugu mkasema Ndesamburo hakusema. Nimesema na naomba Serikali isikie huyu Mkurugenzi hatufai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wafanyakazi wa Serikali wana-*retire* wakifika miaka 60, huyu Mkurugenzi kaongezewa miaka miwili baada ya ku-*retire*; hivi maana yake nini? Vijana ambao wako tayari wanaweza kufanya kazi zile wanaachwa na huku Serikali inatoa kauli inasema wanaopewa *contract* baada ya ku-*retire* ni wenye kazi maalum! Hebu niambieni, Mkurugenzi wa Halmashauri unatakiwa utaalam gani mpaka anaongezewa? Ameongezewa miaka miwili, jamani hii ni hatari, huku tunatoa kauli hii, huku tunafanya mambo mengine tofauti. Tunaomba yule Mkurugenzi tafadhali aondolewe Moshi. Tunaambiwa eti anaweza kuwadhibiti Wapinzani, hivi kweli hiyo ndiyo sababu ya kumweka Mkurugenzi alete vurugu katika Mji kwa kuwa anadhibiti Wapinzani? Sasa wakileta vurugu akishindwa itakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mlima wa Kilimanjaro ni kielelezo kizuri cha nchi yetu ya Tanzania, ndiyo mlima mrefu kuliko yote Afrika na ndiyo kivutio kikubwa cha utalii. Tunaingiza fedha za utalii kwa kutumia Mlima ule. Ule Mlima unaharibika, mazingira yake ni mabaya kabisa, miti inakatwa, moto unachomwa; hii ni hatari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati tumepata Mkuu wa Mkoa Mpya, kijana shupavu, ameweza

kuhamasisha sasa tunapanda miti mingi. Tungeomba katika fedha za utalii, wale wanaopanda sehemu moja iachwe kwa zile Halmashauri zinazozunguka ili ziweze kusaidia kuboresha angalau kutia maji katika ile miti inayopandwa iweze kuendelea. Kwa hiyo, tungeomba sana *KINAPA* au *TANAPA*, katika fedha za watalii wanaoingia, wanaopanda ule Mlima, hatujataka fedha zaidi, fedha zile za watalii wanaopanda Mlima sehemu fulani iachwe ili iboreshe mazingira ya ule Mlima. Hilo tunaomba sana lifanyiwe kazi. Tulishalipitia hilo mpaka kwenye *RCC* yetu ya Kilimanjaro ili hizi fedha ziweze kusaidia kuboresha mazingira ya ule Mlima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia haya mazingira, labda nigusie sehemu nyingine; nilitumia helikopta nikatembea sehemu fulani za Tanzania. Ukitumia helikopta unaiona nchi, unaona mazingira ya watu, ukitumia barabara huwezi kuona na ukitumia ndege ya juu huwezi kuona. Nimeona mambo ya ajabu; katika nchi yetu kuna watu mpaka sasa wanakaa porini kabisa hakuna barabara wala kitu chochote. Watu hawa hata hatuwajui. Nimekwenda mpaka *Sukuma Land* ile inakuwa jangwa kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kila mwaka tunapanda miti; tunapanda wapi? Kama tusipofanya mkakati maalum, nchi yetu inarudia kuwa jangwa. Kwa kweli nchi hii inarudia kuwa jangwa na mimi ningepomba Viongozi, hebu nendeni na helikopta, msiende na magari, ndiyo mnaweza kuona vichaka

vya watu, mnaweza kuona jinsi Watanzania walivyo na mnaweza kuona matatizo. Maendeleo ya nchi twende pamoja. Nakumbuka wakati wa Vijiji vya Ujamaa, nadhani tatizo lilikuwa neno ujamaa, tunahitaji kuanza ile *operation* mara nyingine lakini tusitumie ujamaa, tuseme ni Vijiji. Maana watu wanasema ukisema ujamaa, ujamaa labda hata na mkee wangu atakuwa wa jamaa.

Kwa hiyo, watu wanaogopa, lakini tungetafuta njia nyingine, tukusanye hawa Watanzania walioko porini. Kuna Watanzania hawajui hospitali, hawajui shule, hata makaburi sikuyaona; ni hatari. Tukisema miaka hamsini tumeendelea wakati wenzetu wanakaa porini kama wanyama, kwa kweli ni hatari. Mimi ningepomba wakati mnaposema tunakwenda kuangalia Watanzania katika Tanzania, hebu tumieni helikopta mpite, maana inapita hapa juu kidogo, unaona chini mpaka kuku unawaona. Ukienda na gari hutaona, ukienda na ndege kule juu hutaona. Mkaone matatizo ya Watanzania. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba niseme naunga mkono hoja hii. Kwanza, naomba nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Simbakaliya, kwa kazi nzuri anayoifanya kule Mkoani. Vile vile naomba nimkaribishe Mkuu wangu wa Wilaya;

karibu sana Nanyumbu, nakuahidi kwamba nitakupa kila ushirikiano unaostahili. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naomba niipongeze Serikali hasa Hotuba ya Waziri Mkuu, kwa maamuzi yake ya kuwaongezea posho Madiwani. Kwa kweli Madiwani ni watu ambao wanatusaidia sana Wilayani na Vijijini. Nashukuru kwa kusikia kilio cha Wabunge na sasa Serikali imekubali kuwaongezea posho. Naomba isiishie kwa Madiwani tu, hata Wenyeviti wa Serikali kule Vijijini na Vitongojini, wapewe posho kwa sababu wao ndiyo hasa wanaotusaidia katika kazi nyingi sana kule Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni kero kubwa sana Wilayani kwangu Nanyumbu. Hatuna maji juu na wala hatuna maji chini ya ardhi. Nasema chini ya ardhi kwa sababu sijui kama huku chini kuna maji, lakini ninaposema juu nina maana kwamba Wilaya ya Nanyumbu karibu yote kwa ujumla wake ni kavu. Kuna maji ya Mto Ruvuma, maji yake yanakwenda tu baharini hayafanyi kazi yoyote, hayachangii pato lolote, hayachangii maji safi na salama kwa ajili ya Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu. Kwa hiyo, ninaposema kero ya maji ni kubwa sana, ukienda Nakanya, Nanderu, Naneme, Likokona, Nawaje, Chitandi, Chipuputa, Chitowe, Muhinawe, Namalombe na Mkwajuni, kote huko kuna tatizo kubwa la maji, achilia mbali Wilaya nzima ya Nanyumbu. Ninaomba sana Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, atakapofanya majumuisho yake au kwenye bajeti

yake, nione ni jinsi gani atatatua kero ya maji Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naomba nikwambie kwamba, Wilaya ya Nanyumbu ina Vituo vya Afya vitatu na Zahanati kumi na tano tu. Wananchi wanapata tabu sana, wanasafiri umbali mrefu hasa akina mama ambao wanaenda kujifungulia huko kwenye Zahanati na kwenye Vituo vya Afya. Wanakwenda mwendo mrefu ajabu na wengine bahati mbaya ikitokea wanajifungulia njiani. Kwa hiyo, naiomba Serikali itusaidie kuongeza Vituo vya Afya na Zahanati katika Wilaya yangu ya Nanyumbu. Vile vile kuna uhaba mkubwa wa watumishi kwenye kwenye Zahanati na kwenye Vituo vya Afya, naomba Serikali ituongezee watumishi hawa na sehemu nyingine kuna wahudumu tu; mfagizi yeye huyo huyo ndiye anahudumia kutoa dawa na kuchoma watu sindano, kitu ambacho hakiruhusiwi ni hatari kubwa sana, lakini kutokana na uhaba huu wa watumishi, inabidi watu hawa wafanye kazi hizo. Uhaba wa madawa vile vile ni mkubwa sana kwenye Vituo vya Afya na Zahanati zetu. Nilisikitika sana nilipoona kwenye Taarifa moja ya Wizara ya Afya kwamba, dawa za bilioni nne ziliharibiwa. Sasa fikiria kama hizi dawa zingekwenda Wilayani kwangu Nanyumbu, nadhani zingeweza kumaliza kama siyo kupunguza tatizo la madawa Wilayani Nanyumbu.

Vile vile Wazee wa Wilayani Nanyumbu, wameniambia kila ninapotembea, ninapokwenda kukutana nao kwenye mikutano ya hadhara kwamba, kila wanapokwenda Zahanati au kwenye Vituo vya

Afya, pamoja na kwamba ni Wazee waliozidi umri wa miaka 65, 70 na 80, lakini hawapati ule msamaha ambao Serikali imesema kwamba Wazee wa zaidi ya miaka 65 wapate huduma za matibabu bure. Kwa hiyo, naomba Wazee hawa wafikiriwe, wapate matibabu bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, hii dhana ya KILIMO KWANZA Wilayani Nanyumbu bado. Mwaka 2010/2011, matrekta madogo yalikuwa 25 na matrekta ya kati yalikuwa matano tu, sasa unaweza kuona ni jinsi gani Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu wasivyoweza kulima kilimo cha kisasa. Wanatumia zana duni ambazo tija yake ni ndogo kabisa. Pamoja na hayo, mpaka leo hii, pembejeo ya Zao la Korosho bado haijawafikia Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu. Sasa leo ni mwezi wa sita, hii ni kero kubwa sana. Sijui itakuwaje wananchi hawa waweze kupata mavuno bora katika msimu ujao kwani bado hawajapata pembejeo yoyote ya Zao la Korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Kijiji cha Mkumbaru bado hawajalipwa pesa zao za Zao la Korosho. Fedha hizo zilikuwa zinapelekwa huko zikaibiwa njiani, lakini mpaka leo hii wananchi wale wanalalamika hawajalipwa fedha yao ya korosho; naomba Serikali ifanye haraka wananchi hawa waweze kulipwa fedha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miundombinu, nitoe pongezi kwa Wizara ya Ujenzi kwa ujenzi wa Daraja la Nangoo. Mimi nitajikita zaidi kwenye Daraja la Mto Lukwamba kule katika Kata ya Napacho.

Daraja hili kila mwaka linatengewa pesa lakini haiendi na wananchi wanapata tabu sana wakati wa masika kwenda upande mwingine wa kijiji. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Ujenzi iharakishe ujenzi wa Daraja la Mpombe ili wananchi hawa waweze kuvuka ule Mto kwa urahisi zaidi.

Vile vile naipongeza Serikali kwa sababu sasa itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Mtambaswala kufika Mangaka mpaka Tunduru. Ninaloomba ni fidia kwa wananchi ambao wamewekewa X kwenye majumba yao ilipwe haraka, kwa sababu mpaka sasa hawajui ni nini la kufanya, waendeleze nyumba zao au vipi. Naomba sana fidia hii ilipwe. Vile vile kuna ile barabara ambayo Rais aliahidi ya kutoka Nangomba mpaka Nanyumbu, wananchi pale wameshawekeka X, ile ni ahadi ya Rais, naomba sana Serikali ianze ujenzi wa barabara ile sambamba na Barabara ya kutoka Mtambaswala - Mangaka mpaka Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la vijana Wilayani Nanyumbu limesahaulika, ninamwomba Waziri mwenye dhamana na Uwezeshaji aniambie tutawasaidiaje Vijana wa Wilaya ya Nanyumbu. Ukienda Sengenya unakuta vijana, ukienda Laikokola kuna vijana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nina kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa kunifanya hivi nilivyo, ninayaweza yote katika yeye anitiaye nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda kuwa finyu, nitachangia katika maeneo machache. Tanzania ni *Sovereign State* na katika bajeti iliyopita, nilizungumzia hili jambo kwenye Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kwa mapana sana. Kuna Mataifa mengi makubwa ambayo yana teknolojia ya juu sana, kitu ambacho nilikuwa najiuliza kwa nini Tanzania mpaka leo hii hatuna mahusiano ya karibu ya Kibalozi na nchi ya Israel. Kwa nini tusiwe na *fully flagged Embassy Tel Aviv*? Hilo ni la kwanza. Vile vile Tanzania pale Dar es Salaam tuna Balozi kama za Canada, Uingereza, Australia na kadhalika; cha kushangaza ni kwamba, Watanzania wanapohitaji *Visa* kwenda katika nchi hizi inabidi waende Nairobi; ni kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge ninayetokea Mkoa wa Mbeya, tunapozungumzia *Kiwira Coal Mine* imekuwa kizungumkuti. Naomba nitamke wazi, sasa hivi tusipopata majibu ya kina na yenye tija, sintaunga mkono Bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Kwa nini nasema hivyo? Tunapozungumzia *Kiwira Coal Mine*, tunazungumzia pia Mlima wa Kaburu. *You can't separate the two, ni identical twins.* Tunapozungumzia *Kiwira Coal Mine* siyo lleje pekee

yake, siyo Rungwe pekee yake, siyo Kyela pekee yake, siyo Mkoa wa Mbeya pekee yake na Mikoa ya jirani na nchi nzima *for the national interest. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasikia tu mambo mengi kwamba, *Kiwira Coal Mine* imeuzwa kwa *Australian Company*; imeuzwa vipi? Ilitumia vigezo gani? Tujue.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa Serikali imetenga Bajeti ya *40 billions* kumlipa nani? Kwa nini *and what next?* Tunaomba majibu. Hili suala la *Kiwira Coal Mine* limekuwa ni utata mtupu, wananchi kule wamekuwa *poppers*, wamekata tamaa ya maisha kabisa. Mgodhi huu uko *idle*, umekufa kabisa, hii ni hasara kwa Taifa. Ningeomba Tume iundwe, kama haitaundwa basi kuwe na *competitive bidding* ili uweze kufanyika utaratibu *on a transparency manner under the good governance*. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali katika Sekta hiyo hiyo ya Nishati na Madini kwa kuongeza *royalty* kutoka asilimia tatu mpaka nne kwenye makampuni ambayo yalikuwa yana mikataba na yanaendelea ku-*exist*. Vile vile naomba niishauri Serikali, katika ukurasa wa 30 kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumzia suala la *STAMICO* kuwa na hisa kwenye makampuni mapya haya yanayokuja.

Mimi ningeshauri Serikali, kwa sababu kwenye *Revised Mining Act* ya 2010 ipo hiyo; Serikali iweze ku-*negotiate* na hizi *existing mining companies* ambazo

zipo tayari ili hii *STAMICO* iweze kuwa na hisa huko kuliko kuzungumzia makampuni mapya. Hatuwezi kuzungumzia makampuni haya mapya eti ndiyo tuanze ku-*negotiate* nao kwa sababu hatuna uhakika kama yatakuja au hayatakuja. Kwa hiyo, kama iliweza ku-*negotiate* kwenye yale makampuni ambayo yana-*exist* katika *royalty from three to four percent* kwa nini isiweze ku-*negotiate* pia katika suala la *STAMICO* kuwa na hisa kwenye haya makampuni ambayo tayari yana-*exist*? Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali ni huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, naomba niipongeze Serikali kwa kukumbuka kuwaongeza posho Waheshimiwa Madiwani, katika ukurasa wa 55. Vile vile kwenye ukurasa wa 11 wa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, ameelezea kuhusu Maafisa Tarafa, hajaeleza tija. Hawa Maafisa Tarafa wanapata shida sana. Kwa mfano, kule Mkoani kwangu Mbeya, hawana vyombo vya usafiri, hawana ofisi, Maafisa Tarafa wanafanya kazi kwenye Ofisi za Kata. Maafisa Tarafa hawa wao ndiyo makarani, wahudumu na ndiyo kila kitu. Mara ya mwisho Mkoa wa Mbeya, Maafisa Tarafa walipata usafiri wa pikipiki mwaka 2002. Naomba hili liangaliwe kwa umakini na vile vile kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atuambie ni lini hasa watapata hivi vyombo vya usafiri na ofisi kwa sababu haijaelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbuke ndugu zetu Wenyeviti wa Vijiji na Serikali Mitaa. Hawa ndiyo mahakimu, watendaji wenye kusilikiza kero na

kila kitu kule kwenye *grass root*, ninaomba wapewe posho wamesahaulika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, naomba nizungumzie suala la viwanda. Kule kwetu Mbeya, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu naye ni shahidi, alitembelea Kiwanda cha *Tanganyika Packers*. Kile kiwanda ukweli kina *machinerics* nzuri za kisasa, lakini kipo *idle*, hatujui ni kwa nini, bado tunasikia tu masuala ya uwekezaji, hatujui hatima yake ni nini. Vile vile siyo hicho tu cha *Tanganyika Packers*, kuna viwanda kama cha *HISOP*, kuna kiwanda kama kile cha Zana za Kilimo, vyote hivi vimekufa na vijana wa pale Mbeya hii ingeweza kuwa ni tija katika soko la ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la wafanyabiashara. Wafanyabiashara wa Mkoani Mbeya, naweza nikasema kodi ni kubwa. Huwezi kumlinganisha mfanyabiashara anayefanya biashara Mwanjelwa pale kama jina langu lilivyo au mfanyabiashara anayefanya biashara kule Ipinda au kule Kambikatoto au Masukulu au Vywao na mfanyabiashara ambaye anafanya biashara Kariakoo. Mzunguko wa pesa wa ndugu zangu hawa ni mdogo ukilinganisha na mzunguko wa pesa wa kariakoo.

Kwa hiyo, ningepomba suala la kodi hapa liangaliwe kwa sababu hawa wafanyabiashara sasa inafika mahala wanaondoka Mbeya kwa kusema tukimbile Dar es Salaam kwa sababu mzunguko wa pesa ni mdogo, lakini wanatozwa kodi. Sasa Mbeya itaendeleaje bila wafanyabiashara hawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni makampuni ya simu. Kwa kweli mapato wanayopata ukilinganisha na kodi wanayolipa huwezi kuamini; mwaka 2010 yalipata zaidi ya shilingi trilioni sita, lakini kodi ikalipwa *2.7 billion*. Kenya, Uganda na Rwanda wanalipa mara kumi zaidi ya sisi Tanzania. Najiuliza kwa nini makampuni ya simu na madini ambayo ndiyo mapato yake makubwa zaidi walipe kidogo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeeomba niishauri Serikali; Makampuni ya Simu haya *royalty* yake ni 0.8 ya mapato yao na Sheria ya Mawasiliano ya 2003 ipo, basi angalau walipe *royalty* ya 1.2, hii tofauti ya 0.4 iongezwe na iende Hazina na *TICRA* wataendelea kuwa na ya kwao kama kawaida. Kwa hiyo, naomba liangaliwe hili jambo. Ningeeomba sana na naomba nitamke kuwa, suala la *Kiwira Coal Mine* kama sitapata maelezo ya tija, sitaunga mkono hoja. *This is unacceptable. Thank you.* (*Makofi*)

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini nitangulie kusema kwamba, ninaunga mkono hoja hii kwa sababu kubwa nne:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kwanza, Mkoa wa Ruvuma tumepangiwa bajeti ya bilioni 125.5 kwa ajili ya barabara ambazo zinatoka Mangaka mpaka Nakapanya. Nakapanya mpaka Tunduru, Tunduru mpaka Lumesule, tunaeelekea mpaka Kilimasela, Kilimasela tunaenda mpaka Namtumbo, Namtumbo tunaenda mpaka Songea, lakini tutaenda

Peramiho mpaka Mbinga na Mbinga mpaka Mbamba Bay. Naishukuru sana Serikali kwa kutenga kiwango hicho cha pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hizi zinaendelea vizuri, lakini Barabara za Tunduru bado zinasuasua. Ninaiomba Serikali itusaidie, iwasiliane na Mkandarasi yule ili kasi iweze kuongezeka. Sababu ya pili ni kwamba, Serikali imepanga shilingi bilioni 9.5 kwa ajili ya umeme utakaotoka Makambako mpaka Songea. Mradi huu utatusaidia, lakini pawe na kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya tatu ni ile nia ya Serikali, kujenga reli ambayo itatoka Mtwara mpaka Mbamba Bay. Huu ni ukombozi mkubwa sana kwa Wananchi wa Mkoa ya Kusini, kwa hiyo ninaipongeza Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya nne ni kwa sababu Serikali imesikia kilio cha Madiwani na hivi sasa imeongeza posho za Madiwani. Naipongeza sana Serikali kwa hatua hii ya kuongeza posho za Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia katika maeneo matatu: Eneo la kwanza ni kero za Mkoa wa Ruvuma. Eneo la pili, nitachangia katika Sekta ya Fedha. Eneo la tatu nitachangia katika kuwawezesha wananchi kuboresha sekta binafsi na hasa rasilimali watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Ruvuma una kero nyingi, lakini katika vikao vyetu mbalimbali tumekaa na tumeona kwamba, tutoe kipaumbele kwa

kero ya umeme. Umeme ni tatizo katika Mkoa wa Ruvuma hususan Mji wa Songea, yaani ni tatizo kubwa haifai kusema. Pamoja na kwamba, Serikali ina nia ya kuleta umeme kutoka Makambako, lakini tuna Mradi wa Makaa ya Mawe ya Ngaka. Serikali ni vizuri ikaangalia Mradi wa Makaa ya Mawe ya Ngaka, ikaunganisha umeme utokee makaa ya mawe ya Ngaka uje Mbinga, uje Songea, uende Namtumbo na uende Tunduru ili tuweze kupata ukombozi wa Mkoa huu wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kero nyingine kubwa ya soko la mahindi. Mimi ninaiomba Serikali, kero hii ya soko la mahindi imefikia kiwango kikubwa sana na wananchi wameanza kukata tamaa ya kuzalisha. Mahindi yanazalishwa kwa wingi Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Ruvuma ungeweza kulisha Tanzania nzima, lakini adha ya soko ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Watu wa Mkoa wa Ruvuma tunauliza ni kwa nini tusijengewe soko la mahindi kama ilivyo Kibaigwa? Kwa nini tusiwe na soko kubwa la mahindi Mkoa wa Ruvuma? Mkoa wa Ruvuma tumechoka, tunahitaji kuwa na soko ambalo linaweza kuendelea kwa muda wa mwaka mzima wananchi wapate pesa jamani. Ule umaskini wa Mkoa wa Ruvuma ni nani ataujibia? Kama wananchi wanazalisha, lakini leo wanashindwa kupata soko, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, analijua sana hili tatizo na ana Wataalamu wengi wa Masoko; atume Tume Maalum itatue tatizo

hili milele. Kwa Mkoa wa Ruvuma, tumechoka tatizo la soko la mahindi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakubaliana na wewe kabisa, soko kama la Kibaigwa.

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumzia kero ya vijana walioko Songea, Mkoa wa Ruvuma na hususan Songea, viwanda hakuna na ndiyo maana tunasema vijana wale wanahangaika. Tuna Kiwanda cha Tumbaku kikubwa na nikwambie tu kwamba, tumbaku ndiyo zao la kwanza kuingiza pesa katika nchi hii. Tumeingiza pesa nyingi sana na sisi Watu wa Mkoa wa Ruvuma tunalima tumbaku nyingi kutoka Namtumbo. Leo kwa nini tusiwe na kiwanda cha kusindika tumbaku? Itawezekanaje sisi tunavyohangaika kulima, wanawake wanahangaika, wanaume wa Namtumbo; lakini leo kiwanda cha kusindika tumbaku tupeleke Morogoro au sehemu nyingine? Haiwezekani, mnatuonea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kero nyingine kubwa, tumeahidiwa *EPZ*, tunaishukuru Serikali, lakini *EPZ* hiyo, Ukanda Maalumu wa Kuzalisha, wale wananchi hawajalipwa fidia huu mwaka karibu wa tano au wa sita hawalimi. Watu wa Mwenge Mshindo na Ruwiko, wote wanashindwa kulipa fidia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri Mkuu, awasiliane na Waziri wa Viwanda, lakini pia

ahadi tumechoka; Mtendaji Mkuu wa *EPZ*, amekuwa akituahidi kila mwaka kwamba atalipa, lakini malipo haya ya fidia hayajalipwa. Wananchi wa Mwenge Mshindo, leo watafungua *TV*, watafungua Redio, kusikiliza kama kweli Waziri Mkuu, atajibu hii kero ya malipo ya fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeletewa viongozi wazuri sana Mkoa wa Ruvuma. Tuna Mkuu wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Mwambungu, lakini hataweza kufanya kazi vizuri kama miondombinu ni duni kiasi hiki. Hawa Watendaji, mtawa-*frustrate* kwa sababu hawana miundombinu bora ya kuweza kufanya kazi. Tunaomba umeme uwepo Songea ili hawa Viongozi wanaoenda waweze kufanya kazi nzuri Mkoa wa Ruvuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie kidogo suala zima la Sekta ya Fedha. Sekta ya Fedha inakua kwa kiwango kidogo sana hapa nchini. Takwimu zinaonesha kwamba ni asilimia 13 tu ya wananchi hapa nchini ndiyo wanapata huduma za fedha zilizo rasmi, asilimia 31 wanapata huduma za fedha ambazo siyo rasmi sana na asilimia 56 hawapati huduma za fedha hususan vijijini; hii ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Sekta ya Fedha ikue. Tulienda kuwatembelea wakulima na tulimtembelea mkulima mmoja tu wa Mtibwa, alisema yeye binafsi anatafuta mkopo wa shilingi bilioni 70 ili aweze kuendeleza kilimo cha miwa na aweze kuzalisha sukari ya kutosha, lakini leo tunafungua Benki ya Kilimo

kwa bilioni 40. Si atachukua yeye peke yake tu huo mkopo? Kwa hiyo, hii Sekta inatakiwa kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, anafahamu kwamba, kuna mkakati wa *Rural Financial Service Strategy*, umeanza tangu mwaka 2007 mpaka leo hatuuoni!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba, watu wa *Community Bank* wamekuwa na mawasiliano mara nyingi na Waziri Mkuu ili kuangalia *Community Banks*. Wabunge wengi, wanahangaika kufungua *SACCOS*, *Community Bank*, lakini Serikali hatujawaona mnachangamka zaidi. *Community Banks*, zinaweza zikatusaidia sana hususan maeneo ya Vijijini. Ninaomba Serikali ichangamkie mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumshukuru sana Mama Mary Nagu, ambaye tumeshirikiana nae vizuri katika Kamati ya Fedha na ametuahidi kwamba, Sekta Binafsi sasa hivi itashika uchumi na ndiyo itakuwa injini ya uchumi katika nchi yetu. Ninamshukuru sana kwa sababu yeye binafsi ameamua kulivalia njuga suala zima na amekubali kuanzisha Dawati Maalum kwa ajili ya Vikoba. Ninakushukuru sana kwa maana ya kwamba, Serikali sasa imesikia kilio cha wanavikoba na katika hilo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mary Nagu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo; ukurasa namba 48 wa Hotuba ya Waziri Mkuu, umezungumzia suala zima la lishe. Tusipoangalia, watoto wetu watadumaa na tutakuwa na raia ambao hawana tija katika nchi hii. Suala la lishe lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatuma salamu za Watu wa Mkoa wa Ruvuma kwa Waziri wa Kilimo; katika Miradi ya SAGCOT ni lazima aweke maeneo ya Mkoa wa Ruvuma. Kuna bonde kubwa sana la Mto Ruvuma, liingie katika Miradi ya SAGCOT. Ninatuma salamu kwa Waziri wa Kilimo, kuna bonde zuri sana la Lumesule na...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Nitajikita moja kwa moja kwenye kilimo na sababu za msingi za kwenda huko ni wazi kwamba, karibu asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo. Mkoa wetu wa Rukwa na Katavi, karibu asilimia 95 ni wakulima na Jimbo langu la Kwela karibu asilimia 99 ni wakulima. Kwa hiyo, sina sababu kabisa ya kukwepa kuzungumzia suala hili, nitakuwa sijawatendea haki Wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Wananchi wa Jimbo langu la Kwela.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo limeanza tangu utawala wa huko nyuma na limekuwa na misemo mingi sana na maazimio mengi sana, kwa nia njema ya kuweka hamasa mpya ili kuboresha kilimo. Kwa sasa tuna jina jipya kabisa linalotaja KILIMO KWANZA; mimi nafikiria jina hili ifike mwisho sasa

kutunga majina ya kuhamasisha kilimo. Unaposema KILIMO KWANZA, sijui jina lingine litatoka wapi, maana umelishalipa namba moja ambayo ni sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani yapo mambo ambayo tunapaswa kuyazingatia ili twende sambamba na dhamira ya Serikali, kwa maana ya kukipa kilimo kipaumbele. Yapo mambo ambayo nadhani yanaweza kuwa yanahitaji kupata nguvu ya ziada au yanahitaji Serikali iangalie kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ambayo nadhani nayaona kila mkulima mzalendo anatakiwa kuwa na ardhi ya kulima, awe tajiri awe maskini; katika jambo hili, sisi tunakaa vijijini, wapo wananchi ambao hawana maeneo ya kulima kabisa, ili walime wanatakiwa wakodi shamba kwa watu wengine ndiyo walime; huyo maskini. Wakati huo huo Serikali inazidi kuongeza Wawekezaji katika maeneo hayo hayo ambayo wananchi wake wengine hawana mahali pa kulima. Kwa hiyo, nadhani Serikal, ingefanya kwanza utafiti wa kutosha, inapoingiza uwekezaji katika eneo fulani, ihakikishe wananchi wazalendo wa eneo hilo wana eneo la kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ninadhani Serikali inapswa kuliangalia ni Sera nzuri ya Kilimo, kwa maana ya mitaji. Unaposema mtu alime ni lazima uandae mazingira ya mitaji. Mimi ninaishukuru Serikali kwa Ilani yake ya Chama cha Mapinduzi, imetaja wazi kabisa kwamba, ili kila mmoja aweze kupata fursa ya kukopa kwenye mabenki au taasisi za fedha, inabidi kurasimisha nyumba na mashamba ili

aweze kupata kitu cha kumdhamini wakati anaenda kuomba mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu, suala hili halijapewa msukumo wa kutosha. Huu ni mwaka wa pili sasa tangu nimekuwa Mbunge, karibu naelekea miaka miwili na nusu, lakini suala hili halijapewa msukumo wa kutosha. Naiomba Serikali iweke msukumo wa kutosha katika suala hili. Serikali ikiweka msukumo wa kutosha katika suala hili, itakuwa imepunguza kelele ya watu kusema hatuna mitaji, hatuna nini. Bahati nzuri wananchi wamejenga nyumba nzuri kabisa vijijini, ambazo zikipewa thamani inaweza kuwa ni moja ya dhamana inayoweza kumfanya aende akakope mkopo ili aweze kuendeleza kilimo. Kwa hiyo, ninaihimiza Serikali iweke mkazo wa kurasimisha mali za wananchi vijijini ili waweze kupata fursa ya kukopa fedha katika mabenki mbalimbali au taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni zana za kilimo. Ili mkulima huyu aweze kulima vizuri ni lazima awe na zana za kilimo. Mimi ninashangaa, tangu nimekuja hapa, nimekuta matrekta yamerundikana pale Dodoma na ukipeleka Mhasibu pale hasara itakayotoka ni kubwa sana. Ukipeleka Mkaguzi aende pale kukagua ni lini matrekta yale yameingia, faida gani tumepata na hasara kiasi gani, utakuta bongwe ya hasara; yanazidi kupata kutu na mengine hayatafanya kazi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunafika hapo? Hayo matrekta jamani yapelekeni Rukwa na

Sumbawanga. Pelekeni kwenye Halmashauri, Halmashauri ndiyo inajua watu ambao wanaweza wakawa na uwezo aidha wa kuyanunua au kukopa. Kwa nini mnayarundika hapa Dodoma? Yanafanya kazi gani? Maana kwa mbali unazidi kuona tu kwenye runinga, kule vijijini hakuna runinga, watu hawatazami, yapelekeni kwenye *site*, wananchi waweze kuyaona na kuhamasika waweze aidha kukopa au kuyanunua. Sasa matrekta yanazidi kukaa hapa na mimi ninaiomba Serikali, fanyeni *audit* mtaona hasara itakayotokea pale. Tangu matrekta yameingia ni muda mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakuwa na dhamira nzuri, lakini tatizo ni namna gani dhamira ile ifike moja kwa moja kwa mkulima. Nia inakuwa ni nzuri, lakini dhamira haifikii mwisho. Unarundika matrekta Dodoma, yamekaa zaidi ya miaka miwili yako pale yanafanya kazi gani? Ile ni hasara, bora hata uwapelekee Wananchi wa Mkoa wa Rukwa uwakopeshe maana ukiwakopesha watazalisha chakula kwa wingi zaidi, Serikali itapata faida. Kuna sababu gani ya kuyaweka pale? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni tatizo la Wataalamu. Ninaishukuru Serikali kwa upande wa Wataalamu, imejitahidi sana kuandaa Wagani. Kwa hili, ninaipongeza Serikali na ninaomba jitihada hizi ziendele; ni msaada mkubwa sana wa Wataalamu ambao Serikali mmejitahidi. Naomba suala hili liendele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni bei nzuri ya mazao. Ili mkulima aweze kuhamasika ni lazima aone bei nzuri ya mazao na ni vizuri zaidi ikatangazwa kabla ya msimu wa kilimo kuanza ili imvutie. Sasa bei ya mazao inatangazwa wakati Mkulima ameshalima, akipiga hesabu anaona ni hasara, hana pakwenda, analazimika kuuza hata kwa hasara. Kwa nini bei za mazao zisitangazwe kabla ya msimu wa kilimo ili kuweza kumvutia mkulima avutiwe, awe na maamuzi zao gani alime ambalo linaweza kumpa faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni lazima kuwe na uhakika wa soko. Uhakika wa soko ukiwepo ni moja ya vigezo vya kuvutia Mkulima aweze kulima. Lingine ni miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la Mkoa wa Rukwa na Katavi; Serikali inadhoofisha sana jitihada za Wakulima wa Mkoa wa Rukwa. Serikali inatoa ahadi ya kununua mazao hainunui; kwa mfano, wastani wa miaka mitatu, Mkoa wa Rukwa umekuwa ukizalisha tani laki 7,462.4 na ziada ya chakula kwa Mikoa hiyo ni 1,024,214, ziada inayobaki ni 5,076,248. Serikali inanunua asilimia nane tu ya ziada hiyo, kwa hiyo, mazao yote yanabaki, wananchi wanaamua kuuza kwa hasara wanazidi kurudi nyuma. Naomba Serikali ilianganalie hilo; ni kudhoofisha jitihada za wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la Mawakala wa Pembejeo. Mwaka jana tumepitisha bajeti hapa kwamba, hawa Mawakala

watalipwa na bajeti imepita. Sasa hivi zimebakia karibu siku mbili tumalize msimu, lakini bado Mawakala wanapata tabu, hawajalipwa pesa, kila siku wanaenda benki wanakaa pale mpaka jioni hamna pesa, Serikali haijapeleka pesa. Hivi hatuoni kama tunaidhalilisha Serikali?

Ningeomba Waziri anayehusika, atoe majibu kwa nini Mawakala mpaka leo hii hawajalipwa pesa wakati tunafikia mwisho wa mwaka. Tatizo ni nini na kwenye Mpango mlipanga, bora msingesema kuliko kuwatesa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuwarudisha nyuma, halafu mnauwa mitaji yao. Riba za benki mtalipa ninyi maana wengine wamekopa mitaji? Naomba Serikali itoe majibu katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni mikopo; ni bei za mazao zielekee kwa mkulima kabla ya msimu, hilo nimelizungumzia.

Suala lingine ni kuhusu wanaosambaza pembejeo, wasambaze pembejeo kwa mazao yote siyo mahindi tu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Malocha.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja mpaka nipate ufafanuzi wa masuala haya. *(Makofi)*

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia machache katika Bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, nianze kutoa shukrani zangu kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuona umuhimu wa Serikali kumalizia ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Singida na Kamati hiyo imeshauri Serikali kuingia mkataba na taasisi za kifedha ili iweze kupata fedha kwa ajili ya kumalizia Hospitali hiyo kubwa ya kisasa na ambayo itaweza kusaidia kuokoa maisha ya wananchi wakiwemo wanawake na watoto. Nami nazidi kuisisitiza Serikali ichukue ushauri huo ambao ni mzuri ili hapo baadaye tuwe na hospitali nyingi ambazo ni za rufaa kuhakikisha kwamba afya za wananchi zinakuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kuhusu suala la elimu. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 42 mpaka wa 44 ameelezea umhimu au utekelezaji wa Miradi ya Elimu ya Msingi mpaka Elimu ya Vyuho Vikuu. Pia imeelezea mafanikio kadhaa ambayo yameweza kupatikana katika utekelezaji huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu, naomba nikiri wazi na Waheshimiwa Wabunge hususan walimu na wadau wa elimu mnisaidie kusema wazi kwamba suala la elimu katika nchi halijatekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunashuhudia watoto wetu bado wanaendelea kukaa kwenye mawe, matofali na kwenye visalfeti na walimu

wanaendelea kuwafungia wakurugenzi milango wakidai haki zao. Nasema suala hili bado halijatekelezwa ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu Miradi mikubwa ambayo tuliitegemea ingeweza kusaidia katika kuendeleza Miradi ya Elimu. MEM II na MMES II imekuwa ikitengewa fedha kiasi kidogo sana. Nitoe mfano wa MMES II, bajeti ya mwaka 2010/2011 ilipangiwa shilingi bilioni 68.96 badala ya shilingi bilioni 127.39, hii ni pungufu ya shilingi bilioni 58.44. Kama haitoshi, bajeti ya mwaka 2011/2012, MMES II ilipangiwa kiasi cha shilingi bilioni 74.7 badala ya shilingi bilioni 139.39 pungufu ya shilingi bilioni 60.96; mafanikio yapo wapi hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuache uwongo, sasa hivi imefika wakati walimu wanapata shida kufundisha uhalisia wa mambo, mwalimu anakuwa darasani anapofundisha Kiingereza kwa mfano anawaambia watoto wachore kiti, anawaambia *draw a chair*, mwanafunzi anashindwa kuchora kiti anachora jiwe au anachora tofali au salfeti, hajui *chair* ni nini! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusicheze na masuala ya elimu, elimu ni msingi wa maendeleo ya nchi na taifa la wajinga katu halitakaa liendeleo; tuache mzaa ndugu zangu Wabunge tushirikiane kwa pamoja.

Mheshimiwa naibu Spika, katika masuala haya ya elimu, niende pia kwenye ugatuaji wa madaraka na upangaji wa bajeti. Sera ya ugatuaji wa madaraka inasema kwamba, Serikali za Mitaa ndiyo yenye jukumu

la kutekeleza ugatuuji huu wa madaraka, yaani inatekeleza na kurahisisha maendeleo ya wilaya na vijiji. Inapokuja kwenye suala la bajeti, Serikali Kuu inahama katika shughuli zake za kutunga sera na kuangalia ubora wa miradi iliyotekelezwa, inakimbilia kwenye kupanga bajeti hasa katika Mipango ya MMEM na MMES. Mfano mzuri ni bajeti ya mwaka jana, Serikali Kuu ilipanga jumla ya shilingi bilioni 17.2 za MMEM II na MMES II, Fungu 46, fungu dogo la 3001 na fungu 4001. Hii maana yake nini?

Maana yake ni kuzifanya Serikali za Mitaa zishindwe kutekeleza majukumu yake hasa katika Miradi ya Maendeleo, madawati, zana za kufundishia, nyumba za walimu, madarasa na kadhalika na kadhalika. Kwa nini Serikali inakimbilia kwenye pesa au kwa sababu ni pesa za wahisani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli shule za sekondari na shule za msingi zipo chini ya Serikali za Mitaa, basi Serikali ziachwe zifanye kazi hii. Vinginevyo, naungana na Mheshimiwa Charles Mwijage, jana alisema kwamba elimu itoke huko TAMISEMI ipangiwe chombo kingine cha kuisimamia kama kweli tunataka tuwe na elimu bora na tuwe na taifa lenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia zaidi kwenye Wizara ya Elimu. Niende moja kwa moja kwenye Sera ya Ubinafsishaji; pamoja na kusifiwa sana Sera hii sijaona kama ni Sera ambayo inawanufaisha wananchi wa kipato cha chini. *(Makofi)*

Nitolee mfano wa ubinafsishaji wa viwanda na hususan viwanda vya korosho; Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma nikiwepo mimi Mjumbe, tulifanya ziara mwaka huu mwezi wa tatu kutembelea viwanda vya kubangua korosho Mkoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda niseme wazi kwamba, asilimia 75 ya viwanda vilivyobinafsishwa tena kwa wazawa vimetekelekezwa na vimebadilishiwa kazi zake. Viwanda hivi badala ya kubangua korosho, vimekuwa viwanda vya kutunzia korosho ghafi kwa mtindo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Newala One, kiliuzwa kwa jumla ya shilingi milioni 75. Hizi ni Shilingi za Kitanzania siyo dola milioni 75 tu. Tena kiwanda cha Newala One kikiwa kipya kabisa. Niseme wazi, walionunua Kiwanda hicho ni Viongozi wa juu Serikalini, waliwahi kushika madaraka Serikalini na wengine wapo hapa dola inawafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani ni aibu, wamechukua bure kiwanda kipya wamekitelekeza wanafanya godauni; hiyo maana yake nini? Hatujarogwa tunafanya makusudi, mimi ulozi siuamini tunafanya makusudi na huu ni uroho wa wazi wazi na wizi wa wazi wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali wakati inajumuisha itoe majibu hawa watu hasa hawa Viongozi wa juu Serikalini wanatutia aibu,

wanachukuliwa hatua gani na kwa nini Serikali isivichukue viwanda hivi ivirudishe Serikalini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru sana endapo Serikali itakuja na majibu ya msingi tusiendeleo kulalamika. Kuna watu wanasema Wabunge wanalalamika, Mawaziri wanalalamika, kila mtu analalamika; sasa hapa tufanye nini?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaamini ofisi yako, ninaamini utatumia busara kuangalia viwanda hivi, tusiendeleo kusafirisha korosho ghafi. Tunasafirisha korosho na ganda kwa Wahindi, wenzetu India wanatuletea, sisi tunabaki maskini. Naongea kwa uchungu, sitoki Mtwara wala Lindi, lakini hii ni kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu. Mapato haya yatasaidia shule zetu, yatasaidia kujenga maabara na mabweni, kuepusha watoto wa kike kupata mimba zisizotarajiwa, yatasaidia kuleta madawa kwenye hospitali na yatasaidia kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo nimalizie hapa, sitaunga mkono hoja mpaka nipate majibu ya kutosha. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waride Jabu, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nami kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu,

aliyenijalia uzima na afya na kuweza kusimama mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 12, kuhusu wa Muungano. Katika maelezo tuliyoelezwa hapa, tumeelezwa kuwa kulifanyika vikao 14 vya kisekta vya Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini walijadili hoja 12 ambazo ni changamoto za Muungano. Cha kusikitisha kabisa, hoja mbili tu ndizo ambazo zimepatiwa ufumbuzi, tunashukuru kwa hoja ya *TANESCO* na *ZACO* kupatiwa ufumbuzi lakini inasikitisha sana, inahuzunisha sana na kwa kweli inakatisha tamaa kuona kuna matatizo mengi. Changamoto nyingi na mambo mengi yanayohusu Muungano wetu na katika mwaka mzima katika hoja hizo ni hoja mbili tu ambazo zimeshughulikiwa; hii inasikitisha sana. (*Makofi*)

Tunasikitika kwa sababu sisi hasa tunaishi Zanzibar, tunaelewa jinsi hali ya utulivu na amani ilivyokuwa tete katika Visiwa vyetu inatokana na Viongozi wetu kuwa bado hawajawa tayari kutoa maamuzi katika changamoto hizi au kero hizi za Muungano. Kuna mambo mengi; kwa mfano, hili la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Hili ni tatizo kubwa na tunalijua uhalisia wake na tunalijua tangu lilipoanzia ndani ya miaka 48 ya Muungano bado suala hili halijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kikao cha tarehe 24 Januari 2012, Viongozi wetu hawa walikaa na katika makubaliano yao walisema kabisa, kwa kuwa

mchakato mzima wa mambo haya watu wakae pamoja na Wizara zinazohusika na ndani ya kipindi cha miezi minne wawe wameshapata maazimio au jibu. Cha kusikitisha, Mheshimiwa Waziri Mkuu amkuja hapa hakueleza lolote kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha na ufunguaji wa Akaunti ya Pamoja. Hili ni suala ambalo tangu mwaka 2006 nilikuwa nasikia katika Bunge linajadiliwa na kwenye vyombo vya habari. Kwa kuwa suala hili lipo katika kutafutiwa ufumbuzi wake na toka 2006 Tume hii tayari imeshaleta mapendekezo yake, cha kusikitisha zaidi mpaka leo bado hatujalipata jibu na hatujajua ni lini matatizo haya ya Muungano yatamalizika. Mimi naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, jamani tunaupenda Muungano na tunautaka udumu uendelee; kwa hiyo, suala hili litafutiwe ufumbuzi wa haraka tuweze kuendelea na Muungano, utulivu wetu na amani yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendeleo kuchangia kuhusu chenji ya rada; kwa ufahamu wangu, rada ni chombo ambacho kinatumika au kitatumika kwa ajili ya usalama wa nchi yetu na ulinzi na usalama wa anga yetu. Kwa hiyo, ukitazama kwa haraka haraka hayo mambo mawili, kuitoa Zanzibar kwa sababu ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumeunga anga na tumeunga kila kitu. Kwa hiyo, katika maelezo ya chenji ya rada katika Kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, ameeleza kabisa kutokana na uamuzi huo kila Halmashauri itapata mgao wa madawati na namwomba sana Waziri Mkuu

atakapokuja kwenye majumuisho ya hoja yake, atueleze Zanzibar kuna Halmashauri na nitatoa mfano ndani ya Jimbo langu la Kiembesamaki, nina karibu madarasa manane hayana madawati kabisa. Kwa hiyo, naomba mgao huo wa madawati ufike Zanzibar na tamko hilo tunamwomba sana Waziri Mkuu kwa upande wa Zanzibar atuambie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie suala la uratibu wa maafa au menejimenti ya kukabiliana na maafa. Nilikuwa najiuliza mara nyingi hata sisi Wabunge humu ndani tunaona labda sijui ni ufahamu au ni kitu gani ambacho bado Wizara hii kwa maoni yangu, bado Serikali haijaipa kipaumbele. Kwa mfano, hata katika maelezo tuliyopewa, nadhani katika ukurasa 61, tumeambiwa kabisa Serikali itajenga uwezo zaidi kwa nchi kuzuia kujiandaa na kukabiliana na maafa na kurejesha hali ya kawaida kwa waathirika.

Jamani hii sentensi ipo *very broad* sijui nisemaje na ukiangalia unaposema Serikali itajenga uwezo zaidi kwa nchi yetu katika kuzuia, yaani tupo tayari kuwa na programu kuanzia ngazi ya mkoa mpaka vijiji ya kufundisha wananchi wetu jinsi ya kukabiliana na maafa, jinsi gani maafa yatakapotokezea kuweza kujihami au jinsi gani mali ambazo tunawekeza katika nchi zetu tutazinusuru na maafa yatakayotokea.

Jamani nawaombeni au nawaambia Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo kusali sisi wenyewe hapa ndani ya hili Bunge, hatujui hii hali itakuwaje; kwa sababu nilipoingia humu ndani kwanza niliangalia

milango ya kutokea nikaiona nikashukuru Mwenyezi Mungu, lakini baadaye milango hii huwezi kufungua bila ya kuwa na ufunguo wa usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyoelewa, Dodoma ni Ukanda wa Bonde la Ufa na matetemeko yanatokezea. Je, Taasisi yako imeshajipanga tayari kwa lolote tatizo lolote la umeme litakalotokea kwa Wabunge kujua wapi tutatokea? Huu mlango utakuwa hautoshi, Mungu atunusuru na tuendeleo kusali kwa hayo yasitokezee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia katika Mikoa yetu, zile *Command System* za kukabiliana na maafa zipo ndogo kwa sababu hata Idara yenyewe wafanyakazi wake wataalam ni kidogo.

Ukienda pale Wizarani kuwaona wataalam utaambiwa wote wamepangiwa shughuli nyingine labda mmoja yuko Singida kwenye njaa, mwingine yuko Mwanza kwenye mafua ya ndege na mwingine sijui wapi. Kwa hiyo, inaonekana *capacity* ya Idara ni ndogo na hata kule katika mikoa yetu, hakuna watu wanaoshughulikia maafa.

Tunaliona hili suala ni dogo kwa sababu yanatokea maafa; kwa mfano, njaa anachukuliwa mtu yeyote katika Halmashauri anaambiwa kashughulikia maafa kwa sababu hatuna mtaalam au mtu mahususi ambaye anashughulikia au anaratibu maafa au aliyekuwa na A, B, C, D ya maafa. Mimi naiomba sana Serikali, katika mipangilio yake na mipango yake, kuna kozi ambazo zinatolewa katika

Chuo cha Ardhi cha Dar es Salaam, *Degree ya Disaster Management* na *Master's ya Disaster Management*, tuwasomeshe watu hawa tuwapeleke katika mikoa yetu na wilaya zetu waweze kuratibu na kufanya shughuli hizi za maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukilifanya hilo tutakuwa tumelinda na kuokoa mali za nchi zetu. Sasa hivi Tanzania au ulimwenguni kote ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mengine nitachangia kwa maandishi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waride, kwa mchango wako, lakini niseme mambo mawili; moja kuhusu usalama wa Jengo hili endapo matetemeko ya ardhi yatajitokeza. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Jengo hili limejengwa kwa teknolojia ya kisasa kabisa, kiasi ambacho uwezekano mkubwa wa tetemeko likitokea hatuwezi kuhisi chochote hapa.

Kwa sababu limejengwa baada ya lile la mwanzo ambalo liliwahi kutokea tetemeko na tukapata tabu sana, siku nyingine tutaambiana ni nini ambacho kilifanyika kulifanya liwe *secured* sana na tetemeko labda liwe la kiwango kikubwa sana.

La mwisho, Waheshimiwa Wabunge, mnaongelea sana suala la hela za rada lakini si mnajua kuna waliozifuata hata hamsemi na Halmashauri ya Kongwa ipate zaidi kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, atafuatiwa na Mheshimiwa Nassari.

MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha mimi siku hii ya leo kupata fursa hii adhimu kuzungumza kwenye Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza kwa dhati ya moyo Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Nzega kwa kuniruhusu mimi Mbunge wa Jimbo la Nzega pamoja na wananchi wa Jimbo langu kuandamana siku ya tarehe 16/6/2012. Mbali na mashaka na wasiwasi mkuu uliokuwa umejionesha kwenye mifumo ya kiusalama lakini tuliandama kwa amani na utulivu kuonesha hasira zetu, chuki zetu dhidi ya dhuluma na ukandamizaji unaofaywa na kampuni ya uchimbaji dhahabu ya *Resolute Tanzania Limited* kwenye Mgodhi wa *Golden Pride* uliopo Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo kabisa naomba pia nimpongeze Mkuu mpya wa Mkoa Mheshimiwa Fatma Mwassa kwa jitihada anazozifanya

kutuletea maendeleo sisi watu wa Nzega, lakini pia kwa ubunifu anaouonesha katika kutekeleza majukumu yake katika harakati za kuleta maendeleo kwa watu wa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani na pongezi, naomba niende moja kwa moja kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa ahadi za kuwapatia wananchi wa Mkoa wa Tabora maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria lakini pia kwa kutoa ahadi kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2010 kutujengea barabara ya lami kutoka Nzega mpaka Tabora na barabara nyingine ambazo zipo katika mkoa wetu. Lakini hapa pia niwasilishe masikitiko yangu kwamba ujenzi wa barabara ya kutoka Nzega mpaka Tabora unasusua. Hivi ninavyoongea hapa leo hii, Mkandarasi huyo wa *China Communication Constructions Company* ambaye anajenga kipande cha kutoka Nzega mpaka Puge amesimama ujenzi, amefukuza watumishi wote na nitaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anajumuisha atupe maelezo ni kwa nini mradi huu umesimama wakati mradi huu ni muhimu sana, kwanza kihistoria kwani Mkoa wa Tabora ni muhimu na maarufu lakini mbali na hivyo barabara hii ni muhimu sana kuunganisha watu wa Nzega na Makao Makuu ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Mheshimiwa Stephen Massatu Wassira mwaka jana kwenye Bunge la Bajeti akifanya majumuisho ya Wizara ya Maji alinjibu katika maswali niliyokuwa nimeuliza kuhusiana na mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kuja mpaka Nzega, Tabora mpaka Igunga, alinjibu akisema

kwamba upembuzi yakinifu ungeanza mwezi Oktoba mwaka 2011, lakini hivi ninavyoongea hapa hakuna cha upembuzi yakinifu wala ujenzi ambao umeanza kwenye ujenzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Nzega naomba niwasilishe mbele yako leo haya masikitiko yetu kwamba ni kwa nini mradi huu hautekelezwi. Lakini pia nieleze kwamba kisiasa Mkoa wa Tabora ni mkoa ambao unakipenda na kukithamini Chama cha Mapinduzi na ni Mkoa ambao umekipa kura nyingi sana kwenye uchaguzi mkuu uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachelea kusema hapa kwamba kura hizo nyingi ambazo zilielekezwa kwa chama changu cha Mapinduzi pengine zilitokana na ahadi hizi nzuri za Mheshimiwa Rais za kutujengea barabara ya lami kutoka Nzega mpaka Tabora, lakini pia barabara nyingine ya kuunganisha Mkoa wa Tabora na Wilaya zinazozunguka lakini pia kuleta maji kutoka Ziwa Victoria maeneo ya lthelele, Misungwi, Kwimba na kuyafikisha mpaka Mkoani Tabora. Sasa mwaka 2015 si mbali sana, naomba wenzetu katika Serikali muutupie macho Mkoa wa Tabora pengine ikiwezekana msimamisha miradi mingine mipya mwende mtimize hii ambayo tayari tulikwishaahidi siku za huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nikimbie kwenye hoja ya wananchi wa Nzega inayohusiana na uwekezaji mkubwa uliofanyika miaka 15 iliyopita katika mradi wa kuchimba dhahabu. Mradi huu toka uanze

mpaka leo umevuna ratili za dhahabu zipatazo milioni 2.2 ambazo kwa *valuation* ambayo iko *very conservative* zina thamani isiyopungua trilioni tatu na tangu mradi huu uwekwe pale Tanzania imepata pesa zisizozidi bilioni 100. Lakini pia kwa miradi yote ya dhahabu ambayo tunayo hapa Tanzania ina thamani ya zaidi ya bilioni za Kimarekani 49 ambazo zinaweza zikatafsirika kwa *exchange rate* ya leo kama trilioni 78. Lakini pia Tanzania ina hazina ya gesi ambayo ina thamani ya trilioni za Kitanzania zaidi ya 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mapato ambayo tumeyapata kama nchi kwa njia ya kodi na kwa njia ya mrahaba kwa mwaka uliopita tu ambapo dhahabu iliyovunwa ilikuwa trilioni 3.3 za Kitanzania, kodi tuliyopata pamoja na mrahaba tuliyopata ulikuwa una thamani ya bilioni za Kitanzania 100 si zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipendekeze kwamba tusitishie uwekezaji mpya katika sekta hii ya madini lakini pia tusitishie uwekezaji mpya katika sekta ya gesi na zaidi ya hapo tupitishie azimio katika Bunge hili la kuipitia mikataba yote ya huko nyuma ili iweze kuendana na Sheria mpya ya Madini na Tanzania iweze kufaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda si rafiki naomba nieleze kwamba, mimi ni Daktari na nina maslahi kwenye fani ya Udaktari kama Daktari, lakini nina maslahi kwa sababu ni mwakilishi wa wananchi ambao wanategemea huduma za tiba kutoka kwa Madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme nimesikitishwa sana na kauli mbalimbali ambazo zimekuwa zikitolewa hapa Bungeni na Serikali yangu na sidhani kama ni kauli ambazo zinaelekeza kwenye kumwagia moto maji badala yake naona kama ni kauli ambazo zinaelekeza kwenye kuweka petroli kwenye moto ambao umeanza kuwaka. Lakini vilevile ninasikitishwa kama mwakilishi wa wananchi na mgomo ambao unaendelea katika fani yangu ya Udaktari ambapo wananchi wanaingizwa katika matatizo makubwa, wanakosa huduma za afya na mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu ni kuomba Madaktari pamoja na Serikali warudishe mioyo yao chini, warudishe mioyo yao nyuma wajifikirie upya badala ya kuendelea kumwaga petroli kwenye moto wakae mezani watafute suluhu ya mgogoro huu ili wananchi wa Tanzania wapate tiba stahiki kama inavyoelekezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimesikitishwa zaidi na Ndugu yangu na rafiki yangu Dokta Ulimboka Stephen ambaye ni Daktari, ametekwa jana na watu wasiojulikana...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Daktari Kigwangala, muda haupo upande wetu. Sasa baada ya Mheshimiwa Dokta Kigwangala kama nilivyosema Mheshimiwa Joshua Nassari atafuatiwa na Mheshimiwa Seleman Zedi. Mheshimiwa Nassari!

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili kwa niaba ya wananchi wa Arumeru Mashariki niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze na tatizo ambalo limekuwa sugu kwenye sehemu mbalimbali kwenye nchi yetu na hususan kwenye Jimbo langu na Wilaya yetu ya Arumeru ambalo ni tatizo la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kabisa kwamba ndani ya siku chache zilizopita migogoro ya ardhi imejitokeza tena kwenye Jimbo langu la Arumeru Mashariki na mpaka kupelekea baadhi ya watu kupoteza maisha. Nimeitafuta hotuba ya Waziri Mkuu ya mwaka jana nikalinganisha na ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba yake ya mwaka jana Waziri Mkuu alizungumzia sana suala la ardhi na akapendekeza kwamba, Serikali inakuja na mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuweza kuzuia maafa ambayo yanaweza yakatokana na migogoro ya ardhi. Lakini kitabu cha mwaka huu kwenye suala hilo hilo la ardhi kinachoonyeshwa ni hati kwenye vijiji zaidi 11,000 yaani mipaka ambayo imepimwa, lakini haioneshi ni migogoro mikubwa mingapi kati ya wawekezaji au wamiliki wa mashamba na wananchi ambayo yametatuliwa wala hatua ambazo Serikali imechukua badala yake, suala hili limekuwa likichukuliwa kisiasa na watu wanasema kwamba

vurugu zinafanyika Arumeru kwa sababu ya CHADEMA wakati mwaka 1952 kabla ya Tanganyika kupata uhuru Arumeru walikusanya pesa wakamtuma Ayo Japhet Kiriro Umoja wa Mataifa ikiwa *UNO* kwenda kwa sababu ya *Meru Land Case*, sasa sijui kama mwaka 1952 hata kabla ya kupata uhuru sijui kama Japhet Kiriro naye alikuwa CHADEMA au CHADEMA ilikuwepo kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ardhi tulichukue kwa umakini mkubwa sana, tumekuwa na migogoro mikubwa kwenye madini kwenye nchi yetu lakini migogoro hii iko kwenye maeneo husika yale ambayo yana madini, lakini tatizo la ardhi limekuwa ni kubwa kabisa kwenye nchi yetu kila kona ya nchi hii na kama tukiendelea kulifumbia macho kuna tatizo kubwa mbele yetu litakuja na maafa yatazidi kujitokeza kwa wingi. (*Makofi*)

Kuna barua hapa kutoka Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tangu mwaka 1999 na inaainisha mashamba 11 ndani ya Wilaya ya Arumeru ambayo yalipata kibali cha Rais ili yaweze kufutiwa hati, lakini mpaka leo tunapozungumza mashamba yale yapo yamemilikiwa na watu, wananchi hawajayapata na mpaka leo yanaendelea kuzusha migogoro na watu wanaendelea kupoteza maisha. Niseme tu kwamba sitakuwa tayari kuunga mkono hoja kama Ofisi ya Waziri Mkuu isipotueleza kinagaubaga kwamba ni hatua gani zimechukuliwa au Serikali inakwenda kuchukua ili kuweza kuzuia matatizo haya ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Halmashauri zetu Madiwani wamekaa na wataalam wakaunda timu, wakaenda wakafanya utafiti na wakatoa mapendekezo yao tangu mwaka jana mwezi wa tatu, kipindi hicho sijawa Mbunge lakini mpaka leo hii ile taarifa inaonekana haijafika Wizarani na wala Serikali haijaipata kwa ajili ya kuweza kuchukua hatua stahiki. Niseme tu wakati mwingine tunawakatisha tamaa Madiwani na Wataalam wetu kwenye Halmashauri kwa sababu wanafanya kazi zao lakini Serikali inakuwa haiwachukulii maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo suala la matumizi yasiyokuwa ya lazima. Jana Mheshimiwa Wenje ameongea hapa na mimi leo nitaongea kuweka msisitizo kwamba leo tunazungumza kwamba nchi ina hali mbaya kiuchumi na kifedha halafu tunajadili bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Wakuu wa Mikoa wote wako Dodoma, wasaidizi wao wako Dodoma, Madereva wao wako Dodoma, Ma-RAS wako Dodoma, wapo hapa sijui wanafanya nini!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini simaanishi kwamba sitaki kuonana na Mkuu wangu wa Mkoa lakini tunaonana kwenye *RCC*, tunaonana kwenye *Road Board* na tunaonana Mikoani. Sasa kuna haja gani ya wao kuwa hapa ndani wakati ofisi zao hazifanyi kazi sasa hivi mikoani? Hizi ni kazi za televisheni ambazo tumenunua ambazo zipo kwenye Ofisi za Wakuu wa Mikoa, wakae kule waangalie kama wanataka kufuatilia Bunge waangalie huko wakati wanaendelea kuwatumikia wananchi kwani hakuna sababu yoyote ya msingi ya wao kuwa hapa, walipiwe

hoteli, *per diem*, chakula na wasaidizi wao pia. Kwa kweli nafikiri ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hivyo tu kwamba leo hii tunazungumzia hali mbaya kwenye nchi halafu bado tunazidi kuongeza Baraza la Mawaziri, halafu kama haitoshi Rais anamteua mtu anampa Uwaziri asiyekuwa na Wizara Maalum, sasa nikajiuliza hivi huyo *plate number* ya gari lake itaandikwa Waziri wa nini, sijui ofisi yake iko wapi, sijui anawahudumia akina nani? Sijui tunaongea nini hapo kwa sababu matumizi mabaya ya mali za umma imekuwa ni tatizo kubwa na linaimbwa kila siku kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la uwekezaji na uwezeshaji. Kuna suala linaitwa *EPZ* na kwenye Jimbo langu la Arumeru Mashariki kwenye Kata ya Kirero, eneo la Marura wananchi mashamba yao yamechukuliwa, ni kwa miaka sasa na mpaka leo hakuna hata mmoja amepata fidia na hatujui wanapewa lini fidia na kwa *rate* ipi. Napenda Ofisi ya Waziri Mkuu ituambie kwamba ni lini watu hawa wanakwenda kupewa fidia zao na kama Serikali haipo tayari watu warudishiwe ardhi ili waendeleo kufanya kilimo mpaka pale Serikali itakapokuwa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la rada, chenji ya wizi wa fedha za rada. Zaidi ya shilingi bilioni sabini kwa mujibu wa kauli ya Waziri Membe zina uwezo wa kujenga nyumba za Walimu zaidi ya 1196, zina uwezo wa kujenga vyoo 200,000 kwenye shule zetu pia. Hizi fedha pia zingekuwa na

uwezo hata wa kuchonga na kununua madawati kwa ajili ya shule zetu lakini mpaka leo hii tunavyozungumza bado wananchi vijijini wanasumbuliwa kila mwaka madawati, mtoto anakwenda shule akimaliza mdogo wake naye anaingia shule naye anaambiwa aje na dawati, kila siku! Na kuna watu tunajjuliza...

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kengele ya kwanza!

NAIBU SPIKA: Ndiyo ya kwanza, endelea.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunajjuliza kwamba hizi fedha wanadai zinarudishwa na nakupongeza Mheshimiwa Naibu Spika kwamba na wewe ulikwenda ukahakikisha kwamba unazirudisha na kwa sababu wewe ni Naibu Spika, huwezi kuzungumza humu ndani, lakini sisi tutakusemea na watu wa Kongwa kwamba hata kule nyumba za Walimu zitajengwa, vyoo vitajengwa na mabati vile vile yapelekwe. Lakini ni lazima tufahamu kwamba, hawa watu wamechukuliwa hatua gani au wanachukuliwa hatua gani kwa sababu itakuwa ni *tendency* ya kila siku kwenye nchi, watu wanapiga pesa zisipostukiwa poa, zikishtukiwa zinarudishwa chenji, lakini hatua stahiki hazichukuliwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tuna kila sababu ya kuwa *serious* zaidi katika hili suala la watu waliohusika wachukuliwe hatua za kisheria ili kwamba tujiridhishe ili wengine wasiendeleo kufanya hivyo kwa sababu huu utakuwa ni wizi wa kila siku na hii biashara

itakuwa ni *business as usual* na hatupo tayari kuendelea na suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Wabunge wenzangu wanaotokea kwenye Majimbo yanayolima Kahawa. Kumekuwa na tatizo kubwa sana kwenye kilimo cha kahawa na wananchi wananyanyasika kwani gharama za utunzaji na kulima kahawa zinakuwa kubwa kuliko ile bei wanayokwenda kununua sana sana kwa sababu ya soko huria, watu ambao wameruhusiwa kwenda kununua kahawa mbichi. Watu wanajipangia bei, hao hao ndiyo Mawakala, halafu ukienda kwenye soko hao hao ndiyo wahusika vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kuna haja ya Serikali kutoa kauli kwamba wakulima wasiuze kahawa mbichi yaani ya maganda kwa mawakala wa soko huria ili waweze kupata stahiki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee suala la utalii. Kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ameongelea suala la kukuza utalii na kuutangaza utalii kupitia Balozi zetu. Juzi nilikuwa Marekani na nilikwenda kwenye Ubalozi wetu wa Tanzania nilichokikuta pale ni *brochure* ambazo zimewekwa pale kwa wale ambao wanatembelea ni sisi wenyewe Watanzania, sasa sijui kama tunakwenda kujifunza utalii Marekani ili tuje kwenda Ngorongoro Tanzania, sielewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu unakwenda sehemu kama Arusha kwenye eneo la Kisongwe, kwenye jengo la *TANAPA* unakuta imewekwa ile *screen*

kubwa ya fedha nyingi ambayo inatangaza mbuga za wanyama wakati mzungu anayepita ile barabara ni yule ambaye tayari yuko barabarani kwenda safari. Nafikiri hizi screen ziwekwe kwenye airport kubwa kama Heathrow, JFK na hata Amsterdam kwamba tutangaze utalii wetu nje ya nchi, lakini mnakwenda kutuwekea *screen* Kisongwe wakati tupo safarini kuelekea mbugani sasa sijui tunatangaza utalii gani na ni utalii gani unaotangazwa Tanzania wakati tunaifahamu Ngorongoro vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba sitakuwa tayari kuunga mkono hoja mpaka maswali yote yapatuwe majibu sahihi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nassari. Mheshimiwa Seleman Zedi simuoni basi nafasi yake nampa Juma Nkamia na Mheshimiwa Kakoso ajiandae. Mheshimiwa Nkamia!

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii, lakini pia kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala* ambaye ameniamsha salama hii leo na Watanzania wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niunge mkono hotuba ya Waziri Mkuu, lakini sababu iliyonifanya niunge mkono ni moja tu pengine kumbembeleza ili aende kwenye mradi wa Ntomoko ili aende kujionea jinsi wananchi wa Jimbo la Kondoia Kusini kule Chemba, Kinkima, Churuku, Hamayi na Songolo wanavyohangaika kubadilisha mahindi kwa

maji, ndiyo sababu kubwa iliyonifanya niunge mkono hoja hii nimbembeleze tu aende, wala siyo mbali, ni kilomita 165 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwapongeze sana wananchi wa Kijiji cha Jinji ambao walizuia gari la kuchimba maji lililokuwa linataka kuondoka baada ya kuchimba mita nne na kutaka kuwadanganya wananchi. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa kumteua Mkuu wa Mkoa Dokta Rehema Nchimbi ambaye kwa kweli ziara yake ya kwanza baada ya kuona *concern* ya tatizo la maji kwenye Wilaya ya Chemba alikwenda katika ule mradi wa Ntomoko. Nampongeza sana Mama huyu na Mungu aendelee kumbariki. Lakini pia nampongeza Rais kwa kuwateua Wakuu wa Wilaya ya Kondo na Chemba Mzee Kwaang'w pamoja na Francis Isaac.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze na kilimo. Tumekuwa na mgogoro wa ardhi kwa muda mrefu sana katika eneo la Kiteto na Wilaya ya Chemba. Wananchi karibu 72 walinyang'anywa mashamba yao katika eneo hili na wamekuwa wanahangaika siku hadi siku na kumekuwa na vurugu za hapa na pale na vifo vimewahi kutokea. Lakini vilevile tumekuwa na tatizo la mpaka kati ya Jimbo la Mheshimiwa Nyalandu na Jimbo langu katika eneo la Nduamganga. Nia ya kufanya mazungumzo na watu hawa tunayo ili tutafute suluhu, uwezo wa kufanya mazungumzo nao tunao,

sababu ya kufanya mazungumzo nayo tunayo, lakini ikifika wakati tutashindwa, inabidi tupeleke salamu kwa njia nyingine. Nadhani hiyo njia nyingine inaweza kusaidia zaidi hatua za haraka zikaweza kuchukuliwa. Hatuwezi kuona wananchi wale wananyang'anywa mashamba pale, Serikali imekaa kimya, nimelisema mara kwa mara jambo hili pengine mie kwa sababu ni mfupi sisikilizwi sana, sasa nadhani tutumie njia nyingine ili tuweze kusikilizwa katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kilimo Mikoa ya Manyara, Singida, Dodoma, Iringa ni wakulima wazuri sana wa zao la alizeti. Leo Naibu Waziri alikuwa anajibu swali pale Bungeni akatoa *data* kwamba tunahitaji kiwango gani cha mafuta ya kula kutoka nje, *data* ambazo *absolutely* siwezi kukubaliana nazo *even a single word. This is not about Tom and Hurry*, hili ni suala la kufanya *research*. Tuna karibu tani 27,000 katika Mikoa ya Singida na Dodoma, leo zipo kwenye magodauni. Juzi Waziri wa fedha anasema ili turudishe ile *VAT* iliyokuwa inatozwa *crude oil* kutoka nje lazima kwanza Mawaziri wa Fedha wa Afrika Mashariki wakae. Si kweli! Hili halipo kwenye *East African tariff*, hakuna! Ningeomba sana jambo hili lifanywe kazi haraka. Ie *VAT* irudi ili alizeti inayozalishwa katika mikoa hii iweze kupata soko la uhakika. Hatuwezi kuacha watu wawili wanahodhi biashara ya mafuta ya alizeti katika nchi hii. *Its only two families* na tunawajua.

MBUNGE FULANI: Wataje!

MHE. JUMA S. NKAMIA: Eeh, makampuni mawili tu, *Murza Oil* na *Mount Meru* na walimtuma mtu wao

ndani ya Bunge hili kuja kufanya *lobbying* ili ile VAT isiweze kurudi. Hatuwezi kukaa kimya. Naomba jambo hili lizingatiwe sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la fedha za rada limekwishazungumzwa sana na wenzangu, ningeomba na sisi Kondoa na Chemba tupate.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye suala la maji. Suala la maji kwenye Jimbo la Kondoa Kusini ni kubwa. Leo wananchi wa Churuku pale debe moja la maji wanabadilisha kwa debe moja la mahindi, Kinkima pale na Songoro, siwezi kuja hapa mimi mwakilishi wao nikakaa kimya. Niliwahi kuuliza swali hapa Bungeni Spika akanizuga zuga tu hivi, nilisikitika sana, lakini nikasema *time will come and I will talk*. Mradi wa Ntomoko nilisema siku ile hapa, Baba wa Taifa na Mama Maria wamelala porini pale siku saba (7) kuchimba ule mtaro wa Ntomoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ile imegawanywa sasa, mradi wa Ntomoko *source* yake Kondoa, wanaotumia maji yale Kondoa Kusini ama Chemba kuna *conflict of interest*. Watu wa Kondoa kule hawawezi kuhudumia ule mradi kwa ajili ya watu wa Chemba. Naiomba Serikali tumezungumza kwenye *RCC* hebu chukueni ule mradi wa Maji ya Ntomoko uende Serikali Kuu ili kuwe na uhakika wa kuweza kufanya miundombinu ikarekebishwa katika eneo lile ili ule mradi uweze kufanya kazi yake vizuri. Naombeni sana na ndiyo maana nikasema naunga mkono na nambembeleza Waziri Mkuu ili aende kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kitu nimejifunza pia ambacho nilidhani ni vizuri nikakisemea kwa taaluma yangu. Tunapofanya chaguzi ndogo, i bahati nzuri nilikwenda Arumeru. Kama hatukuwa *serious* kwenye jambo hili tunaweza kuiingiza nchi hii kwenye matatizo hasa kwa baadhi ya vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Siasa vinawatumia Waandishi wa habari kwa kuwanunua. Anayemlipa mpiga zumari ndiye anayechagua muziki. Mwandishi anaambatana na Vyama vya Siasa, analala kwenye kambi za Vyama vya Siasa, ataandika nini kizuri? Mtaingiza nchi hii kwenye matatizo. Angalieni namna gani Msajili wa Vyama vya Siasa ama Tume ya Uchaguzi iwe *responsible* kwenye suala la waandishi kwenye chaguzi. Naombeni sana, nimelisema hili kwa sababu ni taaluma yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijaona duniani chama cha siasa kinamlipa Mwandishi wa habari kwenda *ku-cover election, never! It's only here in Tanzania.* Hakuna!

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema tuna Wodi ya akinamama hapa Dodoma inahitaji *five* bilioni, mmetupa bilioni mbili. Gharama zinaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka, hebu malizeni kwanza ile *project*. Jengo la Mkuu wa Mkoa pale mmetoa 1.5, gharama zinazidi, hebu jitahidini malizeni. Kama Mkuu wa Mkoa wa Dodoma anapanga jamani si vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hivi ni nani anayesafirisha mahabusu ama Wafungwa kutoka kwenye Mahakama za Kata? Mtu anahukumwa pale anaambiwa Mtendaji ndiye amsafirishe.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Nakushukuru sana. Kwa hiyo, naunga mkono hoja ili Waziri Mkuu aende kule. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Machali muda wangu ni mdogo sana, kuna nini?

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kuomba Mwongozo wako.

Mheshimiwa Mbunge ambaye amemaliza kuchangia katika hoja ya Waziri Mkuu ametueleza hapa kwamba kuna baadhi ya makampuni ambayo yamekuja kufanya *lobbying* kwa Wabunge ili kuweza kupitisha mambo fulani fulani. Sasa pengine kwa kuwa Taifa linakabiliwa na matukio ya ufisadi ya hapa na pale, naomba Mwongozo wako ili kusudi Taifa liweze kuondokana na tatizo ambalo limekuwa linasababisha Serikali inapoteza mapato, wakulima wanaendelea kunyonywa kama ambavyo ameeleza kwamba

baadhi ya makampuni yameteka biashara ya mafuta nchi nzima. Inawezekana kuna misingi ambayo siyo halali kwa mujibu wa Mheshimiwa Mbunge. Ni kwa nini asitusaidie kwa kuwataja watu hawa ambao wametumwa kuja kufanya *lobbying* ndani ya Bunge hili ili kusudi Bunge liweze kukomesha tabia hiyo ambayo ni haramu na imekuwa inasababisha Serikali kupoteza mapato yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana nakushukuru Mheshimiwa. Niseme tu kwamba baadhi ya nchi wametunga sheria kabisa *against lobbying*, lakini siyo hapa kwetu. Hapa kwetu *lobbying* ni kitu cha kawaida. Mnachotakiwa ninyi Wabunge msiwe *lobbied*, vibaya, basi! Maana mtu anaye-*lobby* anajaribu kuuza *agenda* fulani. Kwa maneno mengine Mheshimiwa Nkamia unaweza ukawanong'oneza Serikali kama kuna *lobbying* mbaya ambayo imefanyika.

Tunaendelea na Mheshimiwa Moshi Kakoso na atafuatiwa na Mheshimiwa Highness Kiwia.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naunga mkono kwa sababu kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mkuu wa Mkoa Mpya wa Katavi na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa karibu sana na Mkoa huu mpya wa Katavi ambao kimsingi mikoa hii ni mikoa ambayo iko nyuma sana kimaendeleo. Kwa hiyo, nina

wajibu wa kuipongeza na kuikubali bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo napenda nijikite zaidi ni miundombinu. Miundombinu katika mkoa huu mpya bado ni mibovu. Pamoja na kwamba tumepitishiwa barabara ya Sumbawanga kuja Mpanda bado ujengaji wa barabara hii umekuwa ukienda kwa kusuasua. Ningependa sana Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi ifanye kila linalowezezana kuhakikisha miradi ile ya barabara inayojengwa kwa kiwango cha lami iwezi kukamilika kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa huu unategemea kilimo na mazao ya kilimo kama hayajapata miundombinu mizuri bado tutakuwa hatujawasaidia wakulima. Tuna barabara nyingine ya kutoka Mpanda kwenda Kigoma, Serikali ilikuwa imeahidi kwamba ingeanza ujenzi huo kwa kiwango cha lami Kilomita 100 kutoka Mpanda Mjini mpaka Vishamo, bado mpaka sasa ujenzi huu haujaanza. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu katika majibu yake ya hotuba hii aweze kutoa maelezo ya kina ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kuna barabara muhimu sana, barabara ya Mpanda kwenda Tabora. Barabara hii inatumiwa na wananchi walio wengi na mikoa mingi hasa ile ambayo ina njaa. Barabara hii inabeba magari ambayo yanabeba tani ambazo hazina uwezo wa kuhimili barabara hii. Kwa hiyo, tulikuwa tunaiomba Serikali ifikirie kuangalia

umuhimu wa barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami. Tutakuwa tumewasaidia sana wananchi wa Rukwa na Katavi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu mingine ambayo tunahitaji kuimarishiwa ni ya Bandari. Serikali iliahidi kuimarisha Bandari ya Kipiri, Karema na Kabwe, lakini mpaka sasa bado bandari hizi hazijafanyiwa kitu chochote. Katika Bunge lililopita nilichangia na nilieleza hali halisi ya mradi ule wa Bandari kule Karema kwamba kiwango kilichokuwa kimejengwa pale ilikuwa wamekwenda kujenga choo, baada ya kuzungumza hayo, Mkandarasi alikwenda kumalizia kile choo na akajenga nyumba za watumishi baadaye akatoweka jumla. Naomba Serikali iangalie kwa kina kuhakikisha kwamba inaimarisha bandari zile zote ambazo ziliahidiwa ili wananchi waweze kunufaika na kile ambacho Serikali ilikuwa imekiazimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukanda wa Ziwa Tanganyika una meli moja tu ya *MV*. Liemba ambayo ndiyo inayofanya shughuli za usafiri katika Ziwa Tanganyika. Meli hii imezeeka, na inafanya safari mbili (2) kwa mwezi, hivyo kuwafanya wananchi walio wengi kutumia boti ambazo siyo salama na hatari kwa maisha yao. Naiomba Serikali iharakishe kuhakikisha inarejesha meli ya *MV*. Mwongozo ambayo kwa sasa imebadilishwa matumizi na kuanza kufanya utafiti wa mafuta kule kwenye Ziwa Tanganyika. Huduma ya usafiri kwa wananchi wa eneo lile ni tete sana. Naomba Serikali iliangalie kwa kina sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la reli. Tuna reli ya Mpanda inayounganisha kwenda Tabora. Reli hii imechakaa na treni inayofika kule haina uhakika wa kuweza kutumiwa na wananchi. Naomba Serikali iongeze huduma ya mabehewa, ilete injini ambayo itakuwa ni nzuri, lakini iwahakikishie usalama wananchi walio wengi wanaotumia reli ile. Reli ile ni muhimu sana kwa kusaidia mizigo inayotoka ukanda wa Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma. Ni vizuri tukaiimarisha ile reli ili tuwasaidie wananchi walio wengi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa waweze kusafirisha mizigo yao na kuwasaidia wananchi ambao hawana chakula cha kutosha katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la kilimo. Eneo hili ni eneo ambalo ni ukanda wa kilimo. Bahati mbaya Serikali haijaonesha nia ya kuweza kuwasaidia vizuri wakulima hawa. Serikali inahitaji ipeleke matrekta ya kutosha katika Mikoa hii ya Rukwa na Katavi kwani ndiko ambako kuna uzalishaji wa nafaka mbalimbali yakiwemo mahindi na mpunga. Bahati mbaya mikopo ya kuwawezesha wananchi wa kawaida haipo na Matrekta yanayokuja ni kidogo. Naiomba Serikali iangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anazindua Soko la Tumbaku katika Mkoa wa Rukwa kipindi hicho na sasa mkoa mpya wa Katavi, aliwaahidi wakulima wa Tumbaku kwamba angewatafutia soko la tumbaku nje ya nchi katika maeneo ya nchi ya China. Lakini ahadi hiyo mpaka leo haijatekelezwa. Naiomba kauli aliyokuwa ameitoa aifanyie kazi ili wananchi wa Tanzania nzima

wanaozalisha zao hili waweze kupata soko ambalo litawasaidia kuboresha kilimo chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa kauli ya kuwahakikishia wakulima wa zao la Tumbaku kwamba wangelipwa *two percent*. Naomba atakapokuwa anajumuisha bajeti yake hii aweze kutoa maelezo ya kina kwamba *two percent* iliyokuwa imeahidiwa kwa wakulima wa tumbaku wataipata vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika suala la maji. Maji katika maeneo haya ni tete sana. Vijiji vingi sana katika Mikoa ya Rukwa na Katavi vina uhaba wa maji sana. Vijiji kama Katuma, Kasekese, Kabage, Kamsanga, Igagala, Vikonge na kadhalika, ni vijiji ambavyo havina huduma ya maji. Tunaomba Serikali iweze kupeleka maji katika vijiji hivyo ambavyo ukweli hawajawaji kupata huduma ya maji ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro ya ardhi. Katika eneo hili kuna migogoro mikubwa sana ya ardhi kati ya wananchi na wakulima. Naiomba Serikali itafute suluhu. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kwa kuwa ni mara ya kwanza tangu nilipotoka katika jaribio la kutaka kutolewa roho yangu lililotokana na wafuasi wa Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Ilemela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ilemela, Wabunge na wananchi wote wa Tanzania ambao waliweza kuniombea na nikaweza kupata matibabu ambayo kimsingi yalipelekea niweze kupelekwa nchini India na kutokana na *fracture* mbalimbali katika kichwa changu nililazimika kufanyiwa *surgery*. Nawashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Ilemela na Watanzania kwa ujumla kwa maombi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Ilemela natambua ulikuwepo mpango wa muda mrefu wa kutaka kuniua, taarifa nilizipata, nikazipuuzia lakini kilichonikuta ni dhahiri kwamba, mpango huo ni wa ukweli na bado upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko katika Jimbo la Mwanza hususan Wilaya ya Ilemela hayawezi kuzuiliwa kwa kuondoa roho ya mtu mmoja peke yake. Kwani hata kama nisipokuwepo dhamira ya mabadiliko ya wananchi wa jiji la Mwanza iko pale pale. Naomba niwahakikishie wananchi wa Jiji la Mwanza kwamba niko *fit* na mapambano bado yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie wale waliokusudia kufanya hili kwamba mimi sio kuku

wa Christmas unachinja wakati wowote unaotaka. Nimefinyangwa kwa mikono ya Mwenyezi Mungu na yeye ndio ataamua lini nitaondoka katika ulimwengu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo yanayofanyika katika Taifa hili. Kimsingi unashindwa kutambua kwamba sasa nchi hii imekuwa ni *Mafian country* au la. Ni muda mfupi tu tumepata taarifa zingine za Mwenyekiti wa Jumuiya ya Madaktari kutekwa Dokta Ulimboka na kupelekwa katika msitu na sasa hali yake ni mbaya sana na anapelekwa kwenda kupata matibabu. Taifa hili linakwenda wapi? Tunawafundisha nini Watanzania, ni kizazi gani tunachokitengeneza?

Mheshimiwa Naibu Spika, waasisi wa Taifa hili walitarajia kwamba nchi hii itakuja kuwa na viongozi ambao watakuwa na ndoto ya uzalendo, uadilifu na viongozi bora. Ndio maana Baba wa Taifa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiwia una uhakika na jambo hilo.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ni nchi ya Watanzania wote na kama Mtanzania lazima nisikitishwe na tukio lolote kimsingi ambalo linakwenda kinyume na haki za Mtanzania, pamoja na kwamba siungi mkono mgomo wa Madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichangie. Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa agizo la Serikali

iliondoa kodi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kodi ya Maendeleo na Kodi ya Leseni za Biashara na baada ya agizo hilo Serikali inaendelea na utamaduni wa kutoa fidia. Lakini baadaye Serikali iliagiza kwamba Halmashauri ya Jiji la Mwanza ianze kukusanya Kodi za Leseni na ikaagiza Halmashauri itafanya zoezi hilo tu pale Serikali itakapotoa waraka wa utekelezaji. Baada ya hapo Serikali haikuendelea kutoa fidia ya kodi zile ambazo ilisitisha zisitolewe katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini matokeo yake mpaka ninapozungumza hapa sasa hivi, Serikali haikutoa waraka wa kuidhinisha Halmashauri kukusanya Kodi ya Leseni na wakati huo huo tayari Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilikuwa inakusudia kukusanya zaidi ya shilingi bilioni mbili fedha ambazo zingeelekezwa kwenye mahitaji mbalimbali, kuboresha huduma za afya, kuboresha miundombinu, kuboresha shule zetu na mengineyo. Naomba kutoa kauli ya Serikali juu ya suala hili kwa sababu kimsingi linatokana na Serikali yenyewe na agizo la Serikali yenyewe la kusababisha Halmashauri ya Wilaya ya Jiji la Mwanza kukusanya zaidi ya shilingi bilioni mbili. Naomba kujua Serikali ni lini itakwenda kulipa fidia? Naomba nipate ufafanuzi juu ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza suala la ardhi. Nimekuwa nikija hapa Bungeni mara kwa mara kulalamikia migororo ya ardhi katika Wilaya yangu ya Ilemela, hususan inayosababishwa na Wanajeshi. Wanajeshi katika maeneo ya Mlima wa Nyagunguru, Kata ya Ilemela waliingia kwenye eneo la makazi ya

watu na kuweka mizinga pamoja na silaha mbalimbali za kijeshi. Jambo ambalo ni la muda mrefu na kuzuia shughuli za maendeleo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiwia kaa chini kidogo namwona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 68, msemaji amesema kwamba anafahamu watu waliohusika kutaka kufanya jaribio la kumwua ni wanachama wa CCM wa Ilemela. Lakini pili, amesema anajua na ana uhakika juu ya taarifa na nia za kutaka kumwua. Sasa huyo ni kiongozi na ni mwenzetu na nchi hii inatawaliwa na utawala wa sheria na hakuna sheria inayoruhusu mtu kumtisha wala kufanya vitisho kama hivyo vya kutaka kumwua tena akiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimesimama hapa kuomba Kiti chako tumWombe huyu Mheshimiwa Mbunge atoe ushahidi wa hawa watu wanaotaka kumwua na ili ikithibitika Serikali iweze kumsaidia kwa sababu moja ya jukumu la Serikali ni kulinda raia wake ili iweze kuchukua hatua na kuhakikisha kwamba ina-save maisha yake. Kwanza atoe ushahidi wa hao wanachama wa CCM na hiyo njama ambayo wanataka kumwua, lakini pia awafichue hao ambao ana uhakika nao kwamba wanataka kumwua ili tu-save maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba atoe uthibitisho huo ili kuweza kumsaidia na yeye.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Highness Kiwia hili ni kwa faida yako na ni haki kwako kwamba katika mazingira ambayo umetuambia sisi wenzako sote hapa kwamba ulipata matatizo makubwa sana kwa sababu ya wanachama fulani fulani wa CCM. Kwa kweli ni vizuri ikafahamika ni akina nani na kubwa zaidi hawa ambao wanapanga kukuuu ni vizuri ikafahamika. Tafadhali.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia suala la mgogoro wa ardhi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Highness ni jambo kubwa ambalo tunaomba kujua kutoka kwako sisi Wabunge wote, kwa sababu ni suala la usalama wa maisha yako, jambo ambalo ni muhimu sana. Ukishatufafanulia hilo utaendelea na jambo lako la ardhi.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa nitaleta ushahidi baadaye, lakini ili kudhihirisha hilo siku ya tukio gari la Mbunge Mheshimiwa Maria Hewa lilikuwepo siku ya tukio. Huo ni ushahidi wa kwanza na hiyo ni dhahiri kwamba huo ni mpango maalum. Naomba ushahidi mwingine nitauleta baadaye.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Kwa kuwa unahitaji muda ili kuleta ushahidi basi nakupatia siku saba ili uweze kuleta ushahidi Mezani kwa Katibu utamfikia Spika ili tuweze kujua ni tatizo gani ambalo linampata Mheshimiwa Mbunge na ikiwezekana na sisi kama viongozi wa Bunge tunahusika katika usalama wa Waheshimiwa Wabunge. Nimelisema hili kwa nia njema kabisa. *(Makofi)*

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na nitakushukuru zaidi ukizingatia na kunirudishia muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia suala la mgogoro wa ardhi ambao unasababishwa na Wanajeshi katika Kata ya Ilemela. Baada ya Wanajeshi kuchukua hatua ya kupeleka vifaa vya kijeshi katika eneo hilo na ni zaidi ya miaka mitano sasa.

NAIBU SPIKA: Taarifa, nakuomba Mheshimiwa Highness ukae.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na ushahidi alioutoa msemaji kwamba gari la Mheshimiwa Maria Hewa lilikuwepo. Nataka kumpa taarifa kwamba hata hapa Dodoma nje ya ukumbi huu gari la Mama Maria Hewa liko hapa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nilishafunga ule mjadala na nilikwishatoa muda maalum. Kwa hiyo, Mheshimiwa Highness hebu endelea bwana. Endelea

tafadhali, nakulinda endelea, huna haja ya kuijibu hiyo taarifa endelea.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kwamba kuna watu wanaleta mzaha na maisha ya watu wengine. Kwa sababu hayo hayakuwakuta wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mgogoro wa ardhi kwa wananchi wa Nyaguguru, Kata ya Ilemela unatokana na Wanajeshi kuingia katika eneo lao na kuweka vifaa vya kijeshi. Vifaa ambavyo vinaweza vikasababisha matatizo mengine kama ilivyotokea huko Mbagala na maeneo mengine na kulipatia Taifa hasara kubwa sana. Suala hili nilishaliwasilisha hapa Bungeni na Waziri aliahidi kuja Jimboni kulishughulikia, tangu mwaka wa jana mpaka leo sijamuona Waziri na suala hili bado ni tatizo, wananchi wanashindwa kuendeleza makazi yao, nyumba ikibomoka hawezi kujenga kurudishia ukuta.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Highness Kiwia. Mheshimiwa Khatib Saidi Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Sukum.

MHE. KHATIBU SAIDI HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nami kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika mjadala uliokuwepo mbele yetu. Lakini nataka nitumie dakika zangu mbili kwa kutoa *bashraf* kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi katika vyombo mbalimbali vya habari vya hapa nchini na nchi

nyingine kulikuwa na habari njema ambayo si vibaya kwa faida ya Wabunge na Watanzania nami nikaitoa hapa ili wale ambao hawakuiona kwa bahati mbaya wanaweza kuizingatia. Kulikuwa na habari inasema kwamba Wabunge 140 katika Bunge la Zimbabwe wameshiriki katika kampeni na kujitolea kutahiriwa. Hii ni habari njema katika kujikinga na maambukizi ya UKIMWI, ningetoa wito kwa Wabunge wenzangu ambao bado hawajafaidika na hili basi waitikie wito kwa faida ya Watanzania na wao wenyewe. Napenda ku-*declare interest* juu ya hili, mimi tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib bado naangalia kanuni, huo wito wako uko ndani ya kanuni, lakini endelea tu uchangie. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. KHATIBU SAIDI HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kutoa mchango wangu. Jana kwa bahati mbaya kiongozi wetu wa Kambi makini ya Upinzani hapa Bungeni Mheshimiwa Habib Mnyaa alipokuwa anamalizia kutoa mchango wake dakika za majeruhi alikatishwa kulingana na muda ningependa niunganishe pale ili kwa faida ya Watanzania wajue ni kipi alikusudia kukiongelea Mheshimiwa Habib Mnyaa. Mheshimiwa alikuwa anazungumzia kuhusu Tume ya Kuratibu Maoni ya Katiba ambayo ilizunduliwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 6 Aprili, 2012. Alijaribu kusema kwamba miezi 18 iliyoundwa kwa mujibu wa Tume hii kukusanya maoni ya Watanzania kuhusu mabadiliko ya Katiba tayari miezi mitatu imeshatumika hivyo inamaanisha imebakia miezi 15. Kwa mawazo

yake nami nayaunga mkono alidhani miezi 15 kwa kufanya kazi ile haitatosha. Itakapotokea hilo kama bahati mbaya haikutosha, tunaingia katika Uchaguzi unaofuata mwaka 2015 bado tutakuwa tunaingia katika Uchaguzi kwa kutumia Tume ya Uchaguzi hii ambayo bado ipo ambayo si huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, alichojaribu kutaka kukieleza ni kwamba wakati tunasubiri mabadiliko hayo ya Katiba ambayo yanaratibiwa na Jaji Warioba kama Taifa tumejiandaa je iwapo katika muda huu malengo hayakufikiwa. Je, Watanzania hasa sisi vyama vinavyoonewa tutakuwa tayari kuingia katika Uchaguzi kwa Tume ile ile, mambo yale yale na chama kinachotawala kile kile, Rais yule yule na mambo yote ni yale yale. Je, itakuwaje? Alijaribu kutaka kuomba Serikali ifikirie kuleta sheria ambayo kama ikitokea katika muda ule yale makusudio hayakufikiwa, basi tuweze kuwa na sheria nyingine ambayo Tume ya Uchaguzi itafanyiwa marekebisho ili tuweze kwenda katika Uchaguzi katika Tume inayoaminika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, nataka kuzungumzia Muungano. Kwa bahati mbaya sana tunapozungumzia mambo ya Muungano hasa sisi Wazanzibar tunaonekana tuna vichwa ngumu sana. Lakini nataka nikuambie kwamba sisi kule Zanzibar hatuna mti mwingine tulioupanda ambao tunaweza kulalamikia bei katika soko la dunia imeshuka. Hatuna mikoroshu, pamba, hatuna chochote. Mheshimiwa Baba wa Taifa na Baba wa Jamhuri iliyokuwa ya Zanzibar wakati ule walipochanganya ule udongo, mti uliopandwa pale ni Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana Muungano huu haukuzaa matunda yaliyotarajiwa pamoja na sherehe kubwa tunazozifanya kila inapofikia kuadhimisha sherehe za Muungano huu. Kwa mawazo yetu sisi haukuzaa tunda lililotegemewa, tunda la Muungano halikuzaliwa na badala yake tunasherehekea kitu ambacho hakipo. Tunapoteza mamilioni ya Watanzania kusheherekea sherehe za Muungano, wakati makusudio na dhamira ya Muungano ni kusaidiana na kuleta hali njema za wananchi wetu, hilo halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumeundwa Tume, Kamati inayoongozwa na Makamu wa Rais Mheshimiwa Bilal kushughulikia kero za Muungano. Nataka niisome katika hotuba hii ya Waziri Mkuu, kifungu cha 18 ukurasa wa 12, naomba kunukuu. "Tarehe 26 Aprili, 2012 Muungano wetu ulitimiza miaka 48 ya Watanzania kuishi pamoja kwa amani na utulivu. Katika mwaka 2011/2012 vikao 14 vya kisekta vya Mawaziri, Makatibu Wakuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vilifanyika kutafuta ufumbuzi wa changamoto wa kero za Muungano. Kikao cha Kamati ya Pamoja SMT na SMZ chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais, kilifanyika ambapo hoja 13 zilijadiliwa na hoja mbili tu zilipatiwa ufumbuzi. Hoja ya *TANESCO* kwenda *ZEC* na hoja ya Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mzaha mkubwa sana kwa Wazanzibar. Huu ni mzaha, hii ni dhihaka ambayo kama Wazanzibar bila kujali vyama vyenu.

Nimemsikia Mheshimiwa Leticia akiomba hela ya rada kwenda katika fungu la Zanzibar. Nawaomba Wabunge wa Zanzibar tusikubali, hatukusema kero za Muungano ni hoja ya bili ya *TANESCO* na *ZEC* wala hatukusema kwamba shida ya Wazanzibar ni habari ya Mfuko wa Jimbo shilingi milioni 20 anazopewa kila Mbunge, hiyo sio *issue*. Shilingi milioni 20 nini? Tunalalamika Wazanzibar tumekataliwa kujiunga na Jumuiya ya *OIC* kwa maslahi ya uchumi wa Zanzibar, tumekataliwa kuchimba mafuta yetu, leo mnakuja kutuambia bili ya *ZEC*, bili ya *ZEC* ni nini nitawalipia mimi Wazanzibar wote bili ya *ZEC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sio *issue* tunacholalamika ni kitu cha haki. Kuna mambo makubwa mgao wa mapato ya misaada kutoka nje 4.5% mnatufanya Wazanzibar kama *toys*. Haikui, hainenepi, 4.5% toka ilipozaliwa mpaka leo. Maana yake ukinunua *toys* unaweka ndani wewe ukienda, ukirudi nguo ni hiyo hiyo, chakula hataki, sivyo hivyo. Naomba kero hizi ndizo zinazozalisha kila kukicha tunatafuta fitina nyingine, lakini malalamiko yoyote na manung'uniko hayazai mtoto anaitwa Kheri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib. Naheshimu sana mawazo yako na wajibu wangu hapa ni kulinda uhuru wako wa mawazo. Lakini maneno kama mnatufanya Wazanzibar kama ma-*toy* sidhani kama ni maneno mazuri, yanaangukia kwenye kifungu cha maneno ya kuudhi upande wa pili. Kwa hiyo, naomba tu kama unaweza ulitoe hilo neno halafu uendelee.

MHE. KHATIBU SAIDI HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nafuta hilo neno na naomba radhi kama litakuwa limeudhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nililotaka kulisema ni kwamba zile hoja za msingi zinapotolewa muhimu zifanyiwe kazi katika muda muafaka. Leo hii nawaomba Wabunge wenzangu wa Zanzibar kama fungu letu la rada halikuja tusiunge mkono bajeti hii ya Waziri Mkuu. Tena sote na atakayekiuka hili mimi naomba lakini naomba nitoe na msisitizo kwa kweli Wazanzibar hawatawaelewa. Kwa sababu ni haki yetu. Hii ni haki yetu pesa ya rada lazima tupewe kama wenzetu mnatengeneza madawati tunao watoto wanasoma. Sasa tumeletewa karatasi hapa ambayo inaning'inia katika ile...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbarouk. Nakushukuru sana. Sasa Mheshimiwa Rose Sukum, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Nkumba. Mheshimiwa Rose Sukum!

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali. Mojawapo ya majukumu wa Wizara hii ni utekelezaji wa Malengo ya Milenia na kuwapunguzia umaskini wa kipato na chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye sekta ya Utawala bora, kwanza nianze nayo. Katika suala la utawala bora limebaki kwenye vitabu kwa sababu kama viongozi wa nchi katika ngazi ya vijiji

na vitongoji hawapo madarakani, huku ni kuwanyima wananchi maendeleo kwa sababu hakuna wasimamizi na wafuatiliaji wa miradi ya maendeleo na mapato. Hivyo basi Serikali ilione hilo kwa sababu hata tunapopanga fedha zinapokwenda vijijini maana yake inatumika vibaya. Sasa kama tutalidharau hilo kwa ajili ya kisiasa nadhani sasa tuondokane na siasa tuwaone wananchi ni muhimu zaidi kuliko siasa tunazozitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri unapopeleka fedha Halmashauri, matokeo yake taarifa unazotoa ni kwamba wamepeleka fedha kwenye vijiji hivyo ambavyo havina viongozi, halafu zimetumika vibaya kwenye Halmashauri. Hili tulione na tukalifuatilie kwa undani.

Mheshimiwa Spika, suala la udhibiti wa matumizi ya Serikali. Nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake wamesema wengine wamechukuliwa hatua na hiyo kazi itaendelea. Lakini naomba sana sana nimweleza wazi kwamba katika Halmashauri zetu taarifa wanazotoa zingine zina kigugumizi na afahamu pia kwamba kwenye Halmashauri zetu ni wataalam mmewapeleka kule wanaojua kuweka hesabu vizuri. Sasa na wakaguzi wetu bahati mbaya wanapokwenda kukagua wanawekwa sawasawa. Matokeo yake fedha zinatumika vibaya, suala la maendeleo kwa kweli tuliangalie kwa kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa kuona kama kweli fedha hizo zimetumika kwa maendeleo halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri fedha zilitolewa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Hanang

kwa ajili ya mradi wa barabara. Zile hela Mfuko wa Barabara wametoa taarifa mwezi wa Nne kwamba zimepokelewa shilingi milioni 215, kumbe fedha zilizoingia kwenye Halmashauri hiyo ni milioni zaidi ya 400. Sasa uone wazi kwamba Madiwani wamedanganywa kwa hilo. Hilo tuliangalie kwa undani sana kufuatilia hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia miradi ya barabara iliyotekelezwa ni ya shilingi milioni 218 wakati hata mradi mmoja haukuanza wakati huu. Naomba hilo tuliangalie sana kwenye suala la udhibiti na matumizi ya Serikali na hii ni mifano tu naitoa lakini naomba sana kile kitengo ambacho amekiunda Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu waende wakaangalie *value for money*. Ndiyo mahali ambapo fedha zinatumiwa vibaya. Lakini kwenye taarifa ya kwenye mahesabu inaweza kuwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili liendane moja kwa moja na suala la Madiwani. Limetolewa suala la posho ya Madiwani, lakini hiyo posho hapa kwetu sisi sasa hivi hatujui ni kiasi gani kilichoongezwa na Serikali hii. Inawezekana ni kidogo sana lakini na sisi pia mwaka jana tulikuwa tunapiga kelele kwamba wapewe mshahara sio posho peke yake haitoshi. Itasaidia sana Madiwani kufanya kazi kwa bidii, tunashukuru kuongezewa posho na hiyo posho itakuwa ndogo tunafahamu lakini tunahitaji sasa wapewe mshahara wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji na uwezeshaji. Tanzania iko nje kabisa ya mstari wa kuwapunguzia

wananchi umaskini wa kipato na chakula. Nalizungumzia hilo kwa maana ya kwamba nikienda kwenye sekta ya kilimo takribani asilimia 80 ya wananchi wote wanategemea kilimo. Lakini katika uzalishaji wa chakula, kama tungewatumia wakulima wadogo wadogo nina uhakika kwamba tungezalisha vya kutosha na pia mazao yanayobaki tungeuza nje tukapata fedha za kigeni. Lakini kwa wakulima wadogo wadogo sisi hatuwaoni sana tunakimbilia suala la ubinafsishaji kwa wafanyabiashara wakubwa au makampuni makubwa na wenzetu kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutolea mfano mashamba ya ngano yaliyoko Hanang yalibinafsishwa kwa wawekezaji, lakini mashamba hayo awali yalipokuwa na *NAFCO* yalikuwa yana watumishi zaidi ya 400,000. Halafu pia walikuwa na vibarua zaidi ya 2,000 na ina maana rasilimali watu ilikuwa tayari imechoshwa kwa kule. Lakini leo baada ya kubinafsishwa hizo ekari 40,000, shamba lililobinafsishwa na *RAI Group* ambao wanaitwa *Ngano Limited* wamepewa ekari zaidi ya 30,000, leo wanazalisha ekari 15,000 hivi kweli tunakwenda wapi? Je, tungewapa wakulima wadogo wadogo si wangepanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na watumishi waliowaajiri ni watumishi 60 na vibarua 90. Hebu *imagine* kutoka laki nne au tatu zile mpaka 60. Hivi kweli ni sahihi? Mlubadau ilichukuliwa na Haidom *Lutheran Hospital* na Watanzania wenzetu. Hilo shamba lina ekari 10,000 lakini wanajitahidi kulima ekari 8,000 na watumishi wako 55, shamba hilo moja na

inawezekana kwamba pia wana vibarua zaidi ya 90,000. Huoni kwamba haya ni manufaa makubwa. Nadhani sasa ifikie mahali haya mashamba yaliyobinafsishwa kwa wawekezaji wa nje yarejeshwe kwa wananchi wadogo wadogo ili walime, walete tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi napenda kuzungumzia upande wa kilimo. Sisi tumefuta kodi ya kuingiza ngano nchini kwa asilimia sifuri. Je na hawa wakulima wa ngano walioko kusini na walioko kaskazini watauza ngao yao wapi wakati kipato wanachopata ni laki sita kwa heka moja? Ina maana ngano yao haitauzwa. Basi Serikali ifanye juu chini kuhakikisha kwamba wanapata soko mahali pengine ili waweze kuuza ngano yao kwa sababu wenye viwanda hapa Tanzania wanaosaga unga ni wachache sana na hawazidi watano. Je, hizo ngano watapeleka wapi Watanzania wenzetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala la mikopo. Wakulima hawa wangeweza kukopeshwa kwa kupewa zana za kilimo ambayo kweli imepunguzwa bei kwenye hii ya Suma JKT. Nadhani bado hatujafikia hapo. Kuna aina nyingi lakini mikopo hiyo inakwenda kuchukuliwa mbali. Ukienda kwa mfano, *TIB* lazima uende Dar es Salaam na gharama ni kubwa sana. Zaidi ya milioni 15/- tunatumia sisi kwa ajili ya kupata mikopo. Hivi majuzi matrekta tuliyopata sisi Basotu, matrekta sita tulitumia zaidi ya milioni 15/-, mzunguko ule wa kuhangaika na kuandikiwa andiko na kadhalika. Ni fedha nyingi sana kwa mkulima hawezi. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri ifike mahali Benki zingine zilizoko za *NMB* kama nilivyokuwa naiomba kila

wakati wapewe fursa ya kuwa na hilo dirisha dogo waweze kuwakopesha wakulima wadogo wadogo, hiyo itawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala la vizuizi. Vizuzi sasa hivi inashangaza sana. Pamoja na kwamba Serikali imesema imepunguza sana vizuizi, lakini barabara kuu bado ina vizuizi kwa wale watoza ushuru wa mazao na imefikia mahali hata watu kutekwa nyara kwa sababu hakuna ulinzi zaidi ya hao watoza ushuru. Tunaomba sana tusaidiwe kwenye hilo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rose Sukum. Mchangiaji wetu wa mwisho leo atakuwa Mheshimiwa Said Nkumba.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika zangu zizingatiwe. Kwanza naomba nianze tu kusema yafuatayo. Tanzania ilishakombolewa sasa hivi kazi ni kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Wale wenye uchungu sasa hivi na nchi hii hawana nafasi, aliye na uchungu anakwenda hospitali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumwa na wananchi wa Sikonge na haya nitakayokuwa nayazungumza hapa ni maelekezo tu ya kuielekeza Serikali ikafanyie kazi.

Moja, mgogoro wa mpaka *WMA* Ipole, upatiwe ufumbuzi. Mbili, mgogoro wa *scheme* ya umwagiliaji Uluwa ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu alishiriki utafutiwe ufumbuzi haraka iwezekanavyo. Tatu,

bwawa la Unyanyama limeshakamilika, wananchi wa Mji wa Sikonge wanahitaji maji, pelekeni maji Sikonge. Nne, migogoro ya wakulima na wafugaji nchi nzima sasa ni tatizo, Serikali ishughulikie. Tano, miundombinu ya barabara, nashukuru barabara za Mkoa wa Tabora zinaanza kujengwa, lakini naomba kasi iongeze kwa haraka zaidi. Naomba vilevile ile barabara ya kutoka Tabora kwenda Sikonge, hatua za haraka zianze kufanyika ili kazi za ujenzi wa lami iweze kufanyika haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine *SES* ya tumbaku kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu naiomba sana Serikali itimize ahadi yake na wito wangu ni kuendeleza suala la kutoza asilimia tano, asilimia mbili ibaki kwa kuendelea zao na asilimia tatu iende Halmashauri zote zinazolima tumbaku ili ziweze kusaidia na zilete maendeleo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, naomba niseme mambo mengine yafuatayo. Watanzania wataendelea kuheshimu Bunge na Watanzania wataendelea kutuheshimu wanasiasa. Lakini nilikuwa nafuatilia Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambayo imejaa maelezo ya kutaka Watanzania wawe na utulivu waendeleo kuwa na amani. Nataka niseme hapa katika nchi zote ambazo hali ya usalama, hali ya utulivu imepotea, wanasiasa ndiyo wamesababisha kwa kiasi kikubwa hali hiyo itokee. Nataka kuwaonya Watanzania, nataka kuwaonya wanasiasa wenzangu, tunayoyasema hapa lazima kwa kweli kwa namna moja au nyingine tuwe tunayafanya katika maeneo yetu hasa tunapokuwa katika shughuli zetu za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mfano hapa kiongozi unahutubia mkutano, saa kumi na mbili ndiyo mwisho wa mikutano yetu ya kisiasa kwa mujibu wa Sheria, muda umefika, Polisi anakwambia teremka muda umekwisha, unagoma. Unapokuja hapa Bungeni unawaambia wananchi na Watanzania kwamba sisi Wapinzani nia yetu ni kuifanya Tanzania iwe nchi ya utulivu, unawadanganya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba na nawasihi sana Watanzania wanatutegemea sana, Watanzania wataendelea kuhakikisha kwamba maneno tunayoyasema ndiyo maneno ambayo yanaendelea kujenga amani na utulivu wa Tanzania. Kwa hiyo, naomba tuzingatie.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Machali, muda wangu ni mdogo sana, labda kwa kifupi sana, ni nini? Mheshimiwa Nkumba subiri kidogo tu.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nataka kumpa taarifa mzungumzaji anayeendelea kwamba atambue kwamba si kweli kwamba mikutano yote ya Vyama vya Siasa inapaswa kwisha saa kumi na mbili, isipokuwa nyakati za kampeni za uchaguzi. Lakini kama sio kampeni za uchaguzi tunapaswa kuendelea kwa mujibu wa taarifa ambazo tumetoa kwa Jeshi la Polisi ila isiingie usiku. Nampa taarifa hiyo ili aweze kulitambua hilo na aweze kuweka mambo sawasawa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nkumba endelea.

MHE. SAID J. NKUMBA: Taarifa naikataa na kwa kweli nataka kusema kwamba unapofika mahali unahutubia mkutano kuna ulinzi. Sasa kwa namna moja au nyingine hali ya ulinzi itakapofika muda basi ni vizuri ukatii wale wanaokupa maelekezo kwa sababu ndiyo wanaoangalia vilevile usalama wako.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho nataka niseme tu kwamba, yale tunayoyasema ni vizuri vile vile tukayazingatia sisi wenyewe. Tumekuwa na maelezo mengi sana ya kuitaka Serikali ya Chama cha Mapinduzi ipunguze matumizi lakini leo nimepata mshangao mkubwa sana hapa. Badala ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuiomba ipunguze matumizi leo Mzee Ndesamburo ametuhamasisha sasa tutumie helikopta kwenda kuwatembelea wananchi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe ufafanuzi hapa kwamba, yale matumizi ambayo kwa kweli yanaweza yakatumika kwa magari na matumizi yanayoweza kutumika kwa helikopta nataka nipewe ufafanuzi hapa kama kweli matumizi haya yapi yako juu na yapi yako chini. Maelezo haya yanatuthibitishia kabisa kwamba bado hatujawa na chama mbadala, bado hatujawa na Wapinzani makini wanaoweza kupima matumizi gani ambayo yanaweza kuwa sahihi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niendeleo kuwaomba Watanzania waendeleo kukiamini Chama cha Mapinduzi, waendeleo kuiamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ina watu makini wa kuendelea

kuwaletea maendeleo. Naomba tushirikiane, tushikamane tujenge nchi yetu. Ukombozi wa Watanzania ulikwishafanyika na baada ya sisi kupata ukombozi tukawasaidia wenzetu wa bara la Afrika kuleta ukombozi. Naomba tusonge mbele, naomba tusaidiane katika kuhakikisha kwamba tunaendelea kuleta maendeleo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, naomba nishukuru sana na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Namwona Mheshimiwa Arfi labda anataka kutueleza kati ya gari na Helikopta ipi ni ghali zaidi. (*Kicheko*)

MHE. SAIDI A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa hilo. Pamoja na maelezo ambayo aliyotoa mchangiaji wa mwisho suala la amani na utulivu ni la pande zote mbili na wala huwezi kuzielekeza lawama kwa upande mmoja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ni Kanuni ipi? Ni mwongozo au ni nini?

MHE. SAIDI A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika ni taarifa tu kwamba...

NAIBU SPIKA: Kama ni taarifa amekwishakaa.

MHE. SAIDI A. ARFI: Nimesimama kabla.

MHE. NAIBU SPIKA: Alikwishakaa samahani. Ungemwahi kidogo kama sekunde mbili hivi.

MHE. SAIDI A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kabla.

NAIBU SPIKA: Samahani tufuate Kanuni. Mheshimiwa James Mbatia ilikuwa ni hilo hilo.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni mwongozo wa jambo lililotokea Bungeni. Nikitumia Kanuni ya 64 (1)(g).

NAIBU SPIKA: Naomba uisome.

MHE. JAMES F. MBATIA: Inasema kwamba bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayohitajika na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Msemaji aliyemaliza kusema sasa hivi amesema mtu anayesema anasikia uchungu inabidi aende hospitalini, wakazae. Sasa huku ni udhalilishaji wa kundi mojawapo. Amedhalilisha wanawake wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na duniani. Wakiwemo akinamama wa Sikonge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili mwongozo wako ni kwamba Mzee Ndesamburo alipokuwa anasema asubuhi alikuwa anatoa ushauri.

NAIBU SPIKA: Mwongozo ni mmoja tu.

MHE. JAMES F. MBATIA: Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wa Kiti ni kwamba, mzungumzaji alikuwa sahihi kabisa. Mheshimiwa Said Nkumba kwa vile ni ukweli ulio dhahiri kabisa kwamba, wenye uchungu basi wanakwenda kujifungua. Kwa kweli huwezi kumtoa hapo itakuwa ni vigumu sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbatia naomba tuvumiliane tu.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa michango yenu mpaka sasa. Tutaendelea jioni ya leo na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Ezekiel Maige atafuatana na Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Ahmed Ngwali ajiandae, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Jenista Mhagama. Baada ya kusema hayo naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni ya leo.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka
Saa 11.00 jioni)*

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Kama nilivyokuwa nimetangaza mapema asubuhi, mchana huu mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Ezekiel Maige na atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe. Mheshimiwa Maige.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii na haya ni maelekezo dhahiri kabisa ya wananchi wa Jimbo la Msalala, ambao wiki tatu zilizopita waliniambia niunge mkono bajeti ya Serikali hii na ya sasa. Kimsingi, kwa sababu wanaridhishwa sana na hatua ambazo Serikali inachukua hasa katika kusukuma maendeleo ya Mkoa wetu wa Shinyanga, ikumbukwe kwamba Mkoa wa Shinyanga ukisoma *statistics* zake zinasikitisha kidogo kwa sababu kuna *contradiction* kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nifahamishe jengo hili Tukufu kuwa, Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa idadi ya watu nchini hapa. Ninazungumzia Mkoa wa Shinyanga ule wa zamani, unajumuisha Simiyu na Geita. Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa idadi ya mifugo, Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa uzalishaji wa dhahabu, Mkoa wa Shinyanga ndiyo Mkoa pekee unaozalisha almasi, Mkoa wa Shinyanga unaongoza vilevile kwa uzalishaji wa tumbaku, *actually* ni miongoni mwa Mikoa mitatu inayozalisha tumbaku kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali hizi za Mkoa ukiziangalia haziwiani kwa kiasi kikubwa na mazingira halisi ya wananchi wa Mkoa ule pamoja na *statistics* hizo nilizozionyesha kwa upande wa utajiri wa Mkoa. Mkoa huu ukiangalia mambo ya kimaendeleo uko nyuma sana. Mkoa huu wa Shinyanga kwa miaka kadhaa, kwa mfano umekuwa ni miongoni mwa Mikoa inayoongoza kwa mauaji ya *albino* na vikongwe, mauaji ambayo kwa kiasi kikubwa yanahusishwa sana na imani za kishirikina na ukosefu wa elimu. Mkoa wa Shinyanga kwa muda mrefu umekuwa ukishika nafasi ya mwisho kwenye mtihani wa Darasa la Saba. *Actually* ni zaidi ya miaka mitano mfululizo, matokeo ya mtihani wa Darasa la Saba kwa Mkoa huu yamekuwa ni mabaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *statistics* nyingi za kielimu na kiuchumi, Mkoa huu uko nyuma sana. Ukiangalia uwiano kati ya walimu na wanafunzi, Mkoa huu una mwalimu mmoja wanafunzi 62 na ni wa pili kutoka mwisho kwa Mikoa yote nchini; Mkoa huu una uwiano mbaya wa idadi ya Shule za Sekondari *vis-a-vis* Shule za Msingi; Mkoa huu una uwiano mbaya mbaya wa idadi ya walimu *vis-a-vis* wanafunzi; Mkoa huu una uwiano mbaya wa idadi ya nyumba za walimu na idadi ya walimu; Mkoa huu una uwiano mbaya kati ya vitabu *vis-a-vis* wanafunzi; kwa ujumla Mkoa huu uchumi wake uko duni sana, ni miongoni mwa Mikoa minne ya mwisho kwa kuangalia *per capital income* ya mwanachi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazingira hayo, tunatumia nafasi hii kuiomba sana Serikali kwamba

jitihada ambazo imeanza kuchukua kuboresha elimu hasa kuanzia mwaka 2005, tulipoanza mradi wa kuboresha Elimu za Sekondari hasa zile za Kata, mradi ule uendelee pamoja na miradi mingine. Kwa kiasi kikubwa kutatua matatizo ya Mkoa wa Shinyanga unahitajika msukumo wa kiserikali ili kuwajengea uwezo wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kuweza kunufaika na rasilimali zao vizuri hasa. Kwa hiyo, naiomba Serikali itusaidie yafuatayo: La kwanza, elimu kama nilivyosema na *statistics* zilivyoonyesha, tunaomba Mkoa huu uwe na kipaumbele cha kipekee sana kwenye suala la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa elimu katika Mkoa ndiyo unafanya wananchi wasiwe na uwezo wa kutumia rasilimali zao. Mkoa huu badala ya kutumia rasilimali zake kama mifugo, ambao kwa sasa ndiyo unaoongoza kwa kuzalisha, watu wanaotangatanga nchini na rasilimali zao, Mkoa huu badala ya kunufaika na madini unaongoza kwa kulalamika kwamba hawanufaiki na ni kweli ukifika utaona kuwa hali hairidhishi. Yote hayo ni kwasababu elimu ya wananchi hawa ni ndogo, lakini kubwa zaidi ni kwamba Mkoa huu una uwiano mdogo kati ya nafasi za viongozi za maamuzi *vis-a-vis* idadi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira hayo, kwenye maamuzi ya kiseri yanayohusu nchi pale ambapo panakuwepo na uwakilishi mdogo kuna athari ya kwamba watu wanaona kuwa kwa kiasi kikubwa hawajashirikishwa. Jambo la pili ambalo naiomba Serikali ni kutazama rasilimali madini Mkoa wa Shinyanga kama nilivyosema ni tajiri sana kwa madini

na hasa dhahabu na almasi, lakini manufaa tunayopata kutoka kwenye raslimali hii ni kidogo sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Shinyanga hivi karibuni pamoja na mambo mengine, tulimweleza kwamba moja ya tatizo kubwa tulilionalo ni zile *MDA (Mining Development Agreements)*, yaani mikataba ya madini ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiomba kila wakati iletwe hapa Bungeni ili iweze kuonekana kwa Wabunge wengi na iweze kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa vipengele ambavyo havifai ni kipengele kinachozuia kwa mfano, Sheria ya *Local Government* kuizua Halmashauri kutoza ushuru wa *Service levy* kwa mgodi. Badala yake Halmashauri inaruhusiwa kutoza au kulipa dola laki mbili kwa uzalishaji wa mgodi wa Bulyanh'ulu na Buzwagi mwaka 2010. Kahama ilitahili kupata dola za Kimarekani milioni 2.4, badala yake imepata dola za kimarekani 400,000 yaani dola 200,000 Buzwagi, dola 200,000 kutoka mgodi wa Bulyanh'ulu ingeruhusiwa itoze *0.3 percent* ya *gross turnover* kwa kuangalia *production* yao na kuangalia *price per ounce* ya dhahabu Wilaya ingepata zaidi ya dola milioni 2.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la manufaa ya madini kwa Mkoa wenyewe. Tumekuwa tukilisema hili suala, linaonekana kama vile linaweza lisilete sura nzuri kwa umoja wa Kitaifa na kadhalika. Lakini niseme, mbona kwenye gesi imewezekana baada ya gesi kugundulika Mtwara na Lindi? Ilikuwa ni kipaumbele kuwapatia wananchi wa Mtwara umeme, tunaomba, nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Bomani, tumezunguka kote duniani, *arrangement* ni kwamba

pale ambapo madini yanachimbwa wananchi wale wanapata *share* ya mrahaba. Katika mapendekezo yaliyowahi kutokea ni kwamba inapendeza sana pale ambapo madini yapo, kwa mfano, Wilaya ya Kahama ikapata asilimia 40, halafu asilimia 60 ikaenda Serikali Kuu. Kwa kufanya hivi, tutaondokana na kelele, tutaondokana na kilio wananchi kulalamika kuwa wanaachiwa mashimo, wana-*polute* mazingira na hakuna kinachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana suala hili la muhimu litizamwe kwasababu ninaamini linaweza kutusaidia. Suala la tatu ni suala la kilimo. Sidhani kama ni sahihi Mkoa wa Shinyanga kuwa ni Mkoa unaoongoza kwa kupewa chakula cha msaada kila mwaka. Mvua zinanyesha, mazao tunalima, lakini hali ya mazingira ya Shinyanga yanahitaji Kilimo cha Umwagiliaji. Naiomba sana Serikali tuwe na *scheme* kubwa za umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika kwenye Kijiji cha Chela na kwa heshima, wananchi wa Mkoa wa Shinyanga na hasa Wilaya ya Kahama wakamtunuku kuwa Mtemi Nkumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Mtemi Nkumbi ahadi uliyoitoa Kilimo cha Umwagiliaji kwenye *scheme* ya Chela ambayo kwa sasa hivi tayari wananchi wamesema *scheme* iitwe Pinda, kwa heshima yako. Tunaomba sana maelekezo ambayo uliyasema kwamba Waziri wa Kilimo sasa hivi Mheshimiwa Chiza atakuja ili kuona na kupanua *scheme* ile, yatekelezwe. Inasikitisha kwamba Mkoa mzima sioni kama kuna *scheme* yoyote inayofikia Shilingi bilioni moja ya fedha za uwekezaji uliofanyika.

Kwa hiyo, suala la Kilimo cha Umwagiliaji bonde la Msalala, bonde la Solwa kule Salawi ni maeneo ambayo yanaweza kulisha Mkoa mzima, ile ndiyo Mbarali ya Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, nilitaka kuzungumzia kuhusu utengenezaji au ukarabati wa barabara wa Kahama – Geita. Wenzetu wa Mgodini wa Geita nasikia wamekubali kushirikiana na Serikali kutengeneza kwa kiwango cha lami kutoka Geita mpaka mpakani mwa Kahama na Geita. Naomba Serikali zungumzeni na *ABG* ili nao waweze kusaidia kuchangia ujenzi wa barabara hiyo kuja Kahama kutoka mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu, kwa sababu muda ni mchache, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja yenyewe. Kwanza kabisa, napenda kuchangia kupitia Mkoa wa Katavi katika mgawanyo wa bajeti ya ruzuku ya matumizi ya kawaida katika Halmashauri. Katika Mkoa wa Katavi Halmashauri ya Mlele haijapata mgawo wowote na haipo. Sasa nilitaka kujua Halmashauri hiyo itajiendesha vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hivyo tu, ukiangalia pia kuna Wilaya nyingine kama ya Bariadi ambayo unakuta kwenye mishahara na matumizi mengineyo hakuna. Lakini la pili, napenda kuongelea

suala la ajira. Kwenye suala la ajira, tumesema kwamba tutatoa ajira za kutosha kwa vijana, lakini sasa ukiangalia mfumo uliopo sasa hivi wa ajira, unakuta ajira nyingi sasa hivi zinatangazwa na Sekretarieti ya Ajira. Sasa tumeona kwamba kwa kwetu kama vile Mpanda, Katavi, Rukwa, Songea kwa kweli mpaka matangazo yamfikie mwananchi aliyeko kule kwa kada hizi za chini na ninakumbuka mwaka jana nimeuliza swali kama hili na nikajibiwa kuwa Halmashauri zinaweza zikaomba kibali na zikaweza kuajiri kwa kada za chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kushangaza, jana nimepata taarifa kutoka Mpanda, Halmashauri ya Mji iliomba kibali na ikaajiri wafanyakazi wa kada za chini wakaletewa barua ambayo imewazuia wasiajiri. Sasa ili kuondoa mkanganyiko kama huu, ni vyema kukafanyika taratibu upya waone ni namna gani Halmashauri zinaweza kutoa ajira kwa vijana ambao wako vijijini, wenye nafasi kwa kada za chini, vinginevyo sisi tunasema tunapeleka madaraka kwenye Halmashauri, *Decentralization of power*, lakini bado sasa tunaunda Tume na ile Tume inakuwa kama *center*. Sasa tunakuwa hatuwatendei wananchi haki kwa ujumla kwa maana kwamba hata hii Tume bado inaonekana ina udhaifu katika kutangaza na kutoa ajira na kufanya usahili kwa ajili ya vijana ambao wanatoka mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo naomba Serikali ilianganalie. Lakini la tatu, nakwenda kwenye suala la maji. Kwa kweli kwa Mkoa wa Katavi kwa sababu ni Mkoa mpya, na tumesema kwamba sasa hii Mikoa ya

pembezeni inafunguka, kwanza naishukuru Serikali kwa kuweza kuupa kipaumbele Mkoa wetu wa Rukwa kwa kuweza kutoa barabara ambayo inaunganisha Tunduma kwenda mpaka Kigoma na nyingine ambazo zinakwenda mpaka Tabora. Mheshimiwa Said Nkumba yeye alisema tu ile ya mpaka Sikonge, mimi naomba Serikali iangalie namna ambavyo itaweza kuunganisha barabara hiyo kutoka Tabora mpaka Mpanda kuelekea Kigoma, ili wananchi waweze kutoa mazao yao na kujipatia kipato ili waweze kujiletea maendeleo kwa haraka.

Lingine, napenda kuongelea suala la madini. Tumesema kwamba Serikali itatoa mikopo midogo midogo na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuwakopesha wachimbaji wadogo wadogo. Lakini nikisoma humu kwenye hiki kitabu, naona wachimbaji hawa wadogo wadogo yametengwa maeneo kama Rwangasa, London, Pongwe na Bagamoyo. Sisi Mpanda pia tuna madini, sijaona kama kuna eneo ambalo limeweza kuwekwa hapa, suala ambalo hata Mheshimiwa aliyetoka kusema hapa ameliongelea. Sasa nisingependa nilirudie, lakini pia yafikiriwe maeneo yote yenye madini ili hivi vituo vijengwe ama viwekwe ili wachimbaji wadogo wadogo waweze kukopa vifaa hivyo na waweze kuwezesha ili waweze kupata madini na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji tumeongelea kuwa, kwa sababu Mkoa wetu unakua na ni mpya, najua watu wengi wataingia na kuja kujenga mahoteli na tunawakaribisha wawekezaji na hata Wabunge. La msingi ni kwamba na ninaongea

kwa ukweli kutoka moyoni, Mpanda mjini kwa wale waliowahi kufika, maji tunapata kwa mgao mara moja kwa wiki au mara mbili, mambomba yamechakaa visima vikifika kama hivi kipindi cha kiangazi hata kama ni visima virefu havitoi maji. Kisima kinachobaki kinategemewa pale mjini ni kisima kilichopo pale Polisi katika ofisi za Halmashauri ya mji. Kwa hiyo, unakuta vijana wao kwa sababu wana nguvu, ndiyo wanaokwenda kupanga foleni pale na kuchota yale maji, wanarudi kuwauzia wananchi dumu moja Sh. 500/=, dumu la lita ishirini. Kwa kweli ni kuwatesa akina mama ambao ndio wenye shughuli nyingi za jikoni na za usafi nyumbani, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali pia iangalie namna ya kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza wiki iliyopita swali kuhusu suala la maji katika vijiji vya Kata ya Majimoto. Niliongelea lile eneo nikasema kuwa lile eneo ni la maji moto lote na kwasababu Kata ya Mamba na Kata zinazozunguka kule za Mfinga mpaka kama unakuja Kibaoni, ile njia yote ina maporomoko ya maji. Mwaka jana niliongea na Waziri aliahidi kwamba angetuma *team* kwenda kuyachunguza yale maji na kuhakikisha kwamba ni salama ili yaweze kutegwa wakaingizwa kwenye pampu na kuweza kuwapatia wananchi maji, wananchi wanateseka na ndiyo maana tunaona mpaka leo kuna ugomvi kati ya wakulima na wafugaji, mto huo huo ng'ombe wanakunywa maji hapo, mbuzi wanakunywa maji hapo, mwingine anaoga hapo. Kwa kweli siyo salama na ndiyo maana hata mkiangalia kwenye takwimu za afya, maeneo hayo kipindipindu kipo kila mara kutokana na tatizo hilo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la maji lipo pia kwenye vijiji vya Kata ya Kakese na Kata ya Misunkumilo. Serikali ilisema ilipeleka hela, lakini mpaka sasa hivi hela tulipitisha kwenye bajeti ya mwaka jana hazijafika na leo tunaongelea bajeti nyingine. Sasa naomba hilo pia litolewe maelezo ili wananchi wa Kata hizo za Kakese pamoja na Misunkumilo wapate kuelewa tatizo liko wapi, mpaka sasa hivi hawajapata hizo hela na hawajachimbiwa visima, mpaka sasa wako kwenye matatizo ya maji, wanatumia maji ya mto Mpanda ambako huo mto uko hatarini kukauka, na maji yake yamechafuliwa na watu wanaoosha magari pale, na shughuli mbalimbali zinazohusiana na maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika haya, napenda pia kuongelea suala la reli. Suala la reli limekuwa ni tatizo sana. Reli tunaambiwa kuwa inakarabatiwa na mimi hiki ni kilio changu sana. Sawa, tunakubali kuwa inakarabatiwa, lakini ukarabati huo ukoje? Kwa sababu isije ikawa tunakarabati, leo ndani ya siku mbili reli imebomoka, wananchi wanalala njiani. Wiki iliyopita, wananchi wamelala Katumba pale *station* kwa siku mbili. Katumba na Mpanda Mjini kwa pikipiki ni mwendo wa dakika kumi, watu wamelala pale. Kwa kweli ni mateso, watu wanatoka Mpanda wanatumia hiyo treni kwenda Bugando kitibiwa kuja Tabora kutibiwa na kuja Dar es Salaam. Sasa ukarabati huo tunaomba kama mainjinia, kama ni Wizara husika wananisikia hapa, wasimamie vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee haraka haraka la kuhusu madawati. Limeongelewa suala hili la kuhusu pesa hizi zilizotengwa kwa ajili ya madawati. Ni kweli kuwa tuna upungufu wa madawati na shule nyingi hazina madawati. Lakini kila mwaka wazazi wanapeleka madawati na wakandarasi na mafundi wanatengeneza hayo madawati. Lakini ndani ya muda mfupi, madawati hayo unakuta yameharibika. Tunaongelea upya suala la madawati, kwa hiyo, tuangalie mpango endelevu. Nilikuwa naongea na Mheshimiwa hapa, nikamwambia nafikiri inawezekana tukatengeneza kama vile viti vya mlimani, vimbwete, nikimaanisha vile viti vya *cement*, labda vinaweza kuwa ni vya muda mrefu kidogo. Lakini sasa kwenye baridi, mwingine anaweza kuuliza utakaliaje kile kiti kwenye baridi? Unaweza kutengeneza kamto *and then* mwanafunzi anaweza akachukulia kile kimto kikawa *portable*, anakwenda nacho nyumbani, anarudi anakalia pale, inaweza ikawa ni suluhu ya kudumu, au ya muda. Najua ilionekana kama ni kichekesho kuwa sasa huyu mama vipi, labda anataka kuturudisha nyuma kwenye ujima kwamba tukakalie tena *cement*, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukilifikiria kwa undani, unaweza kukuta kwamba hapo hapo uta-*conserve* misitu ambayo ni mbao, ama Serikali iangalie ni namna gani inaweza ikapata mbadala ambao ni suala endelevu la kuweza kutengeneza hayo madawati sambamba na majengo ya shule. Inatisha! Nimepita shule ya nyumbani kwangu Mtisi, kwa kweli niliogopa kuingia nyumbani kwa mwalimu. Mimi ni mwalimu, niliogopa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa
Mzungumzaji kwisha)*

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Ahsante. Ninaunga mkono hoja.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesimama hapa kuzungumzia suala la urejeshwaji Mahakama ya Kadhi na siyo kama wengi wanavyozungumzia uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi. Nasema urejeshwaji, kwa sababu hakuna kati yetu asiyejua kuwa Mahakama ya Kadhi ilikuwepo hadi mwaka 1963 ilipoondoshwa pasina ridhaa ya Waislamu wakati wa kuanzisha wa Mahakama moja nchini. Suala hili limekuwa moja katika masuala mtambuka toka pale lilipoingizwa katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi mwaka 2005/2010 ambapo ninaomba ninukuu. Inasema: "Kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara"

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la urejeshwaji wa Mahakama ya Kadhi na uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi ndiyo chimbuko la sintofahamu baina ya Waislamu na Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waislamu hawataki ianzishwe Mahakama ya Kadhi, bali irejeshwe Mahakama yao ya Kadhi iliyoporwa pasi na ridhaa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maneno mengi yamekuwa yanasemwa na hoja mbalimbali zikitolewa juu ya suala la Mahakama ya Kadhi, wengine wakidai suala hili haliwezi kushughulikiwa kwa sababu suala hili ni la kidini na Serikali haiwezi kuingilia mambo ya kidini. Hoja hii haina mashiko, wala haiendani kabisa na hali halisi ya mambo yanavyokwenda duniani. Mbona majirani zetu Kenya wanayo Mahakama ya Kadhi, tena katika Katiba yao mpya na Makadhi wanalipwa na Serikali? India, Uingereza na nchi nyingine nyingi Duniani za *ki-secular* zina Mahakama ya Kadhi ndani ya Katiba zao na nyingine ndani ya sheria zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nionavyo mimi, suala la urejeshwaji wa Mahakama ya Kadhi Tanzania linaangaliwa kwa ubaguzi wa kidini kinyume na Ibara ya 13(4), 13(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inakataza ubaguzi wa aina yeyote katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu Ibara ya 13 (4) (5) inasema: "Ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu au mamlaka yeyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yeyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yeyote ya mamlaka ya nchi." Ibara ya 13 (5) inasema: "Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Ibara hii, neno kubagua, maana yake ni kutimiza haja, haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbalimbali kwa kuzingatia utaifa wao, kabila, mahali wanapotokea, maoni ya kisiasa, rangi, dini, jinsia au hali yao ya maisha kwa maana ambayo watu wa aina nyingine wanafanyiwa au wanahesabiwa kuwa dhaifu au duni na kuwekewa

vikwazo au masharti ya pingamizi ambao watu wa aina nyingine wanatendewa tofauti au wanapewa fursa au faida iliyopo nje ya masharti au sifa za lazima, isipokuwa neno kubagua haitafafanuliwa kwa maana ambayo itaizua Serikali kuchukua hatua makusudi zenye lengo la kurekebisha matatizo mahsusi ya kijamii." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika jamii ya Kiislamu inayo mahitaji mahsusi ya Mahakama ya Kadhi na haiwezi kupatikana pasi kuwepo Mahakama ya Kadhi. Maneno haya yanaungwa mkono pia na aliyekuwa Jaji Mkuu wa Tanzania Jaji Augustino Ramadhani aliposema, naomba nimnukuu: "Tofauti na Ukristo, Uislamu una sheria maalumu zenye maelezo na ufafanuzi wa kina.

Hali hii anasema inahitaji Serikali kuchukua hatua maalum kuwezesha utekelezaji wa sheria hizo. Anasisitiza kuwa, Hakimu katika kesi ya Kiislamu ni lazima awe Muislamu. Sheria ya Kiislam inatoka kwa Mungu na masuala ya kiimani. Kwa hiyo, ni yule tu aliyeamini ndiye anayeweza kuhukumu. Haki siyo itekelezwe tu, bali ionekane imetendeka. Ni vigumu haki kutendeka kama Hakimu siyo Muislamu." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika wakati wa kujenga Taifa la watu wenye kuheshimiana na siyo watu wenye kuvumiliana, kwa sababu watu wenye kuvumiliana, maana yake hawafurahii ya wengine, bali wanajilazimisha kuishi na wenzi wao jambo ambalo siyo jema kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama imewezekana Kenya kuwa na Mahakama ya Kadhi ambako Waislamu ni chini ya asilimia 13, India ambako Waislamu siyo zaidi ya asilimia 15 kwa nini Tanzania isiwezekane ambako Waislamu ni zaidi ya asilimia 52 kutokana na tafiti mbalimbali zilizofanywa, ukiachilia mbali tafiti zilizofanywa na *CIA*, inaonyesha Waislamu ni asilimia 32 na kutangazwa na *TBC*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ngwali hiyo asilimia unanukuu chombo gani? Endelea. (*Kicheko*)

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo habari kwamba, Serikali ina dhamira ya kuanzisha Mahakama ya Kadhi kupitia *Islamic Law Restatement Act* ya mwaka 1964 ambayo inampa mamlaka Waziri husika wa mambo ya sheria kutafsiri au kusababisha kutafsiriwa sheria za Kiislamu ili zitumike nchini na zikishatumika na kisha kutangazwa katika gazeti la Serikali na ndiyo itakuwa kauli ya mwisho. Sheria imeshapitwa na wakati, na haiendani kabisa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 19 (2).

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho ni kwa Watanzania kukubali kujenga utamaduni wa kutofautiana pasi kuchukiana kwa kuruhusu Mahakama ya Kadhi iwekwe katika Katiba mpya. Tofauti zetu zinapaswa kuwa ndiyo sababu ya nguvu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ngwali, nilikwisha mtaja Mheshimiwa Mdee na Mheshimiwa Rage ajiandae.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru. Kwanza nikiwa kama Mbunge, napenda kuchukua nafasi hii kulaani yale yaliyomtokea Daktari Ambokile. Sitaki kujiaminisha kwamba ile *statement* kali iliyotolewa leo asubuhi ina mahusiano ya moja kwa moja na kilichotokea, lakini ninaamini Serikali itahakikisha wale wote waliohusika na huo unyama wanapatikana. Ikishindikana itatufanya kile kiwe kielelezo kwamba sauti ya haki inazimwa na bahati nzuri Mungu kamsaidia...

NAIBU SPIKA: Sina hakika sana Mheshimiwa Halima kama Wabunge wenzako tunaweza tukafuatilia unaongelea nini hasa!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, najua unaelewa, ndiyo maana umenisimamisha. Ninaelezea kipigo alichokipata Kiongozi wa Chama cha Madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama Mbunge wa Dar es Salaam, ninasikitishwa na kauli iliyotolewa na Waziri Mkuu wakati wa hotuba ya Wizara ya Ardhi akitambua migogoro ya ardhi iliyokuwepo Mkoa wa Dar es Salaam akaahidi atakutana na Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam kuweza kutatua changamoto

mbalimbali, akashindwa kufanya hivyo. Hii ni dharau kwa Wabunge, na Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Dkt. Ndungulile kwamba kwa hii bajeti, Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam hatuiungi mkono. Lakini zaidi, wananchi wangu wa Mabwepande, mtakumbuka mwaka jana mwishoni yalitokea mafuriko Mkoa wa Dar es Salaam. Serikali kupitia Mkuu wa Wilaya na kupitia Mkuu wa Mkoa, wakaenda kwa wananchi wa Mabwepande kuwaambia waachie maeneo yao wakiwaambia watalipwa fidia wawahifadhi Watanzania wenzao. Mbaya zaidi, viongozi wa Mkoa na viongozi wa Wilaya wakamleta Rais wa Jamhuri ya Muungano Mabwepande wakitoa ahadi lukuki za kuwalipa fidia za kuwagawia wananchi wa Mabwepande ardhi, lakini tunavyozungumza, mpaka sasa hakuna fidia iliyolipwa, hakuna viwanja walivyopewa wananchi wa Mabwepande, licha ya kwamba ardhi yao ndiyo imechukuliwa na Serikali kuwapa watu walioathirika na mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tuhuma nzito kutoka kwa wananchi wa Mabwepande wakimlalamikia Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa kwa uchakachuzi wa viwanja husika. Suala hili tumelizungumza katika vikao mbalimbali na mbaya zaidi, sio Mwenyekiti wa Mtaa, sio Diwani, sio Wabunge walioshirikishwa katika mchakato wa mgawo wa viwanja. Mgawo ulitawaliwa na usiri mkubwa na hivi tunavyozungumza wananchi wamesema Serikali isipojibu, watarudi kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Waziri Mkuu ambaye kitengo cha maafa kipo chini ya ofisi yake, ahakikishe wananchi wangu wa Mabwepande wanapata haki yao, kinyume na hivyo hatuwezi kuruhusu. Tutaagiza wananchi warudi kwenye maeneo kama ilivyo kwenye mradi wa Kigamboni. Hatuwezi kuruhusu miradi ambayo inaendeshwa shagalabagala ambayo inaathiri wananchi wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam ipite hivi hivi. Wananchi wa Kigamboni wajue Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam tuko nao. Hatuwezi kupindisha sheria, kupokea maeneo ya watu pasipo kufuata taratibu na sheria za nchi kwa sababu tuna dola. Hili ni ujumbe kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nizungumzie kilimo. Yamezungumzwa mengi sana kuhusiana na migogoro ya ardhi. Mwaka jana wakati ninachangia bajeti ya Wizara ya Ardhi, nilisema, ni kwa namna gani Serikali kupitia viongozi wakubwa wamekuwa ndiyo madalali wa ardhi kwa wawekezaji kwenye nchi yetu, matokeo yake ni kwamba wananchi wanyonge wananyang'anywa ardhi kwa nguvu za Serikali. Nikatoa mfano mmoja wa *AgriSol* Rukwa kwa Waziri Mkuu na Waziri Mkuu akanijibu kwa maelezo kwamba waliingia makubaliano ya awali, nikamwambia Waziri Mkuu ama wamekudanganya ama na wewe hauko makini. Akaniambia kuna *Memorandum of Understanding* ambayo wameingia baina yao na yule mwekezaji, akasema yale yalikuwa ni makubaliano ya mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia hii *Memorandum of Understanding* kuonesha kwa namna

gani sasa hivi Serikali ndiyo inasaidia mabeberu kuja kuchukua ardhi yetu, kipengele cha tatu kinaonesha kwamba wanasema wakati huyu Mwekezaji anaendelea na *feasibility study* wakaingia makubaliano Halmashauri pamoja na yule Mwekezaji, wakatengeneza mkataba. Sheria za nchi ziko wazi na nilisema kipindi kile kwamba Sheria ya Ardhi kifungu cha 19 na 20 na Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 inakataza Halmashauri ama mtu yeyote kutoa eneo la uwekezaji. Mamlaka pekee ya kutoa maeneo kwa wawekezaji iko kwa *TIC*. Lakini hapa kwa makubaliano na ambayo Waziri Mkuu anakiri alishiriki wameonesha hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbaya zaidi kipengele kingine kinaonesha kwamba hawa jamaa watakuwa wanalipa Sh. 200/= kwa kila heka, na hii ni *MOU* ambayo Waziri Mkuu namba tatu wa nchi ameingia. Wengine wafanye nini? Anakuja hapa anadanganya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia wanalalamika Rufiji kwamba wawekezaji wanakuja wanapitia migongo ya nyuma wanachukua ardhi. Ni muhimu mkaelewa kwamba kitu ambacho kitakuja kuleta vita nchi hii ni ardhi. Mmeonea migodi kule, yalikuwa ni maeneo ya watu wachache, mnapokuja kupoka ardhi ya Watanzania na kuwapa wageni, mtapata aibu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema mkabisha, wale ambao walikuwa *Ohio State University* Chuo cha Kilimo Marekani ambacho kilikuwa kije kisaidie kuwafundisha

wakulima, baada ya kuona kwamba yule mtu wa *AgriSol* hana nia njema kimejitoa! Ni aibu kuona kwamba eti Serikali inafurahia trilioni 1.4 ya msaada kutoka G8, wakati nyuma ya mgongo wa G8 ukiangalia *SAGCOT*, kitabu cha *SAGCOT* nimekipitia, wadau wote ni wa kampuni binafsi ya Kimarekani, ya kibeberu, inatoa msaada mbele, inakuja nyuma, mnawapa maeneo. Vijana tumechoka! Inawezekana wazee hamna miaka mingi ya kuishi. Sisi tumeshasema msije mkatuachia makapi, msije mkamaliza nchi mkatuachia makapi! (*Makofi*)

TAARIFA

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mdee, kaa chini. Taarifa.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii naitoa kulingana na kifungu namba 68 (7) ambayo inasema hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna mbunge mwingine anayesema kuomba Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni namba (8) Vile vile Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kusema Taarifa na kwa ruhusa ya Spika atatoa Taarifa au ufafanuzi kwa Mbunge anayesema.

NAIBU SPIKA: Upo sahihi, endelea.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji aliyekuwa anaendelea kusema amesema kwamba tamko la Waziri Mkuu asubuhi alilotamka ameliunganisha na tatizo lililotokea la kupigwa kwa Daktari Mlimboko,

WABUNGE FULANI: Dkt. Ulimboka.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Huyo huyo! Mimi naomba kuuliza, anaweza kutuhakikishia kwamba tamko hilo ni kweli na Serikali inahusika katika kipigo hicho? *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa vipi tena? Si nilikuwa naambiwa mimi nielekeze nini cha kufanya? Tulieni kidogo. Ni kweli Mheshimiwa Halima alipoanza kuchangia, alituacha hoi ndiyo maana nikauliza swali, kwa sababu ameinganisha vitu ambavyo vimetuacha njiani, kwamba kuna mtu amepigwa mahali fulani halafu na tamko la Waziri Mkuu asubuhi, hebu tuweke sawa halafu uendeleo kuchangia.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba dakika zangu.

NAIBU SPIKA: Dakika zake mzilinde Makatibu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Hiyo moja. Lakini pili, nilichokisema sasa naomba nirudie. Nimesema ninalaani kipigo alichokipata Bwana Ulimboka kwa kutekwa nyara usiku na watu ambao inasemekana ni Maafisa wa Polisi. Inasemekana! Nikasema sitaki

kujiaminisha wala sitaki kuamini kwamba ile kauli nzito iliyotolewa na Waziri Mkuu leo asubuhi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima nadhani tu nikuruhusu uendeleo kuchangia kwa sababu tukianza kuzungumza habari yanayosemekana na kadhalika, hapa tunazungumza vitu ambavyo Wabunge tumeshajiridhisha navyo, lakini tukiruhusu hapa kila mtu aanze yanayosemekana Mitaani, mimi ninakuhakikishia mtu atasimama sasa hivi aseme inasemekana Halima jana... Sitaki kuendelea sana. Hebu endelea kuchangia. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe umefika, lakini niendeleo. Kwa kumaliza namwomba Waziri Mkuu, ofisi yake imepewa jukumu kubwa sana la kusimamia uwekezaji, na ni aibu juzi Waheshimiwa Wabunge wanashabikia boda boda kuondolewa kodi. Wakati wote tunajua kwamba boda boda ndiyo zinawapa ulemavu, ukienda hospitali leo vijana wamelazwa kwa pikipiki ambazo siyo mali yao. Kwa hiyo, kama kweli tunajali vijana, badala ya kutumia mabilioni ya fedha kuwaandalia miundombinu mabepari katika kilimo, tutumie mabilioni ya fedha kuandaa miundombinu ya kilimo, kuwekeza kwenye kilimo, tuwapeleke vijana wakalime kama watakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia Waziri Mkuu anijibu baada ya Chuo cha *IOWA* kujitoa, ambacho katika yale mapambio waliyokuwa wakiimba katika lile Bunge lililopita kwamba watatoa elimu ya kilimo kwa wakulima wadogo wadogo,

mustakabali wa *Agrisol* ukoje? Nanasema hili kwa sababu moja, huko Rukwa ambako Waziri Mkuu anasema anatoka na kupigania katika asilimia 100, ile ardhi ni asilimia 17 tu ya ardhi ambayo inafaa kutumika katika mazingira ya kilimo na ufugaji. Nyingine ni *games reserve*, nyingine *forest reserve*, nyingine ni maji. Sasa nilitaka akiwa anajipambanua katika haya, aeleze athari ya kujitoka katika hiki Chuo cha *IOWA* ambacho ndio mlikuwa mnajinasabua nacho, lakini vile vile muelezee migogoro ya wakulima na wafanyakazi.

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

MWENYEKITI: Ni kengele ya pili Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja hii. Ahsante sana.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pili, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza yeye binafsi Waziri Mkuu, kwa kuhakikisha wananchi wa Tabora angalau sasa wanaanza kuona mwanga wa kutatuliwa shida zao za maji. *(Makofi)*

Mwaka jana alitupatia Shilingi milioni 262 za kununua pampu. Wakati nachaguliwa, uwezo wa maji katika Manispaa ya Tabora ilikuwa lita milioni nane kwa siku. Leo hii naona furaha kusema hapa kwamba tunapata lita milioni 18. Ni matunda mazuri na

maelekezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna ahadi mbili ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hizo ahadi zinaungwa mkono na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Chama Dume, Chama tawala chenye mipango mizuri ya kuhakikisha Watanzania wake wanafanikiwa.
(Makofi)

Kwa sisi waumini wa dini, tunasema hivi, kila aliyekuwa na subira, yuko na Mwenyezi Mungu. Haraka haraka haina baraka. Hivi karibuni tarehe 18 kipenzi cha wananchi wa Mkoa wa Tabora, Mkuu wa Mkoa Bi. Fatma Mwasa aliongoza *delegation* ya kwenda lhelele ambako kuna mradi mkubwa kuliko yote katika Afrika, unaitwa Kahama, *Shinyanga Water Project*, ukifuatiwa na Mradi wa *South Africa* wa *Land Water Corporation*. Mradi huu wa maji uko Tanzania. Una uwezo wa kutoa maji kwa siku moja lita milioni 120. Lakini matumizi yake kwa sasa hivi ni lita milioni 18 kwa siku ambako wanapata wananchi wa Kahama na Shinyanga peke yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtu ambaye kwa kweli ni msikivu na mfuatiliaji, naomba atuhakikishie wananchi wa Mkoa wa Tabora hususan Manispaa ya Mjini pale, Nzega na Igunga tunaunganishwa na maji kutoka Kahama kwa sababu Serikali ya CCM tayari ilishatenga fedha na hivi ninavyoongea *feasibility studies* zinafanyika tuweze kupata maji kutoka kule lhelele ili kupunguza gharama

ya bei za maji kwa wananchi wa Kahama na Shinyanga. Nasema hivyo kwa sababu maji yakiweza kufika Tabora, tutakuwa tunatumia Manispaa ya Tabora lita milioni 25 kwa siku, Nzega lita milioni tano, Igunga lita milioni tatu, kwa hiyo, utaona tutakuwa na lita zaidi ya milioni 32 ambazo ni *almost* mara mbili ya wanayotumia Kahama na Shinyanga ambapo wananchi wanalipa Sh. 460/= kwa kila lita 1000.

Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa pale kuna pampu aina mbili wanaita *high lift pump* ambazo ziko tatu, lakini inafanya moja tu kwa sasa hivi kwa sababu iko *under utilized*. Kwa hiyo, nina imani kabisa kwamba Serikali kwa kuwa imewekeza zaidi ya Shilingi bilioni 254 katika mradi huu, basi ili kuweza kurudisha hizo fedha, iko haja ya kuhakikisha kwamba mradi huu unatoka Kahama na kufika Tabora na mimi nina imani kabisa kabla ya mwaka 2015, wananchi wa Tabora watapata maji hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki ya jana niliuliza swali Na. 4 kuhusiana na barabara za Tabora. Mimi nina ugomvi mkubwa sana na barabara zangu. Mkandarasi wa kutoka Nzega kwenda Puge, taarifa nilizozipata leo kwa Mhandisi, amesitisha kuendelea na kazi. Wale wengine wanasuasua. Lakini katika majibu ambayo Mheshimiwa Waziri alikuwa amenipa alisema kwamba Serikali ina mpango wa kulipa Shilingi bilioni 64 na ushee. Naomba hizi fedha zipelekwe haraka na ninafurahi nilipokutana na Waziri, amenihakikishia kwamba zitakwenda ndani ya siku mbili zijazo au tatu ili barabara hizo ziweze kutengenezwa katika kiwango

lami na sisi wananchi wa Tabora tuweze kukumbuka.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongelea suala la reli. Tabora ndiyo kiko Chuo Kikuu cha Reli. Wakati wa *East Africa* Chuo Kikuu kilikuwa kiko Nairobi. Sasa hiki Chuo kingine kiko Tabora. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ahakikishe kwamba Chuo kile sasa kinaanza kutumika kwa maslahi ya wananchi na kufufua reli ya Tabora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina masikitiko makubwa, kuna tukio lilitokea hivi karibuni pale katikati ya Gulwe na Kilosa, daraja lilichukuliwa na maji. Wanajeshi walitaka kutengeneza kwa kiasi cha Shilingi bilioni tano hivi, lakini bahati mbaya ikaja kampuni nyingine ya ujanja ujanga, nasikia imetumika zaidi ya Shilingi bilioni 25. Kwa kuwa sina uhakika, naomba Waziri Mkuu alifuatilie hili jambo kama ni kweli, basi siyo jambo zuri hata kidogo kwa sababu linarudisha maendeleo yetu nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vile vile kuchukua nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri wa Uchukuzi Dkt. Charles Tizeba, alikuwa Tabora siku tatu zilizopita, kufuatilia mradi wetu wa Uwanja wa Ndege. Pale tunakarabati uwanja wa kisasa kwa zaidi ya Shilingi bilioni 12, lakini Mkandarasi, sielewi huu ujanja ameupata wapi. Alifanya *variation* ya kuongeza Shilingi bilioni tano lakini Waziri akawa mkali, amemzuia na alikuwa amesimama zaidi ya miezi miwili. Kwa taarifa niliyopata leo, ameanza kazi. Kwa kweli

napenda kumshukuru Waziri kwa kazi nzuri aliyofanya.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa umuhimu wa pekee, Tabora na Mikoa ya Katavi na Kigoma kwa pamoja na Kahama tunazalisha tumbaku asilimia 86.5, *it is high time now*, ni wakati muafaka sasa kuwa na kiwanda cha Tumbaku pale Tabora ili kuweza kukidhi bei za tumbaku. Ukiangalia kwa sasa hivi takwimu za Benki Kuu, Zao la Tumbaku ndiyo liloongoza kwa fedha za kigeni kuliko zao lolote. Kwa hiyo, nina imani kabisa kama kiwanda kitajengwa Tabora, basi ile gharama ya usafirishaji sasa hivi ambayo yote inakwenda kwa mkulima, mkulima atafaidika kwa kupata bei kubwa.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mchele ni mwingi sana Tanzania. Kwa maana ya *South of Sahara* ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa
Mzungumzaji kwisha)*

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.
(*Makofi*)

MHE. AZZA HILLAL HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa afya ya kutosha na hatimaye nimesimama ndani ya Ukumbi wa Bunge na kuweza kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme naunga mkono bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. Ninazo sababu za kusema hivyo. Wananchi na Wanawake wa Mkoa wa Shinyanga wametuma haya yafuatayo kwamba wana imani sana na Waziri Mkuu. Wana matumaini makubwa na Waziri Mkuu, ndiyo sababu alipotembelea Mkoa wa Shinyanga alipewa Utemi katika Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga. Wilaya ya Kahama anaitwa Mtemi Nhumbi. Wilaya ya Shinyanga anaitwa Mtemi Kudililwa. Wilaya Kishapu anaitwa Mtemi Majebele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa imani hiyo kubwa walinayo wananchi wa Mkoa wa Shinyanga hasa wanawake, wamenituma niseme jambo la kwanza ambalo nina imani Mheshimiwa Waziri Mkuu atalifanyia kazi kwa sababu hali halisi ya Mkoa wa Shinyanga alijionea mwenyewe na siyo kuambiwa tena. Wanawake wa Mkoa wa Shinyanga wanasema wamechoshwa na suala la njaa. Hatupendi Wabunge wa Shinyanga kila siku kulisimama kuomba chakula, siyo tabia yetu Wasukuma. Lakini haya ni mabadiliko ya hali ya hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo yangu makubwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ataiangalia Shinyanga kwa jicho la huruma, kwa sababu sio wananchi wote wa Shinyanga wenye ng'ombe za kuweza kwenda kubadilisha mahindi kule Mpanda. Wala hatutemei miaka yote kwamba tukabadilishe mahindi kule Mpanda ili tuweze kupata chakula.

Tunahitaji njia mbadala ya kuweza kuona tunapata chakula cha kwetu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Mkoa wa Shinyanga, kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu aliweza kumwonyesha hakuna Wilaya ambayo alipita na mvua haikuonyesha. Nimkumbushe wakati tukiwa Wilaya ya Kahama Jimbo la Msalala katika Kijiji cha Chela ilinyesha mvua kubwa sana, kwa ahadi yake Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi Wilaya ya Kahama kuitengenezea mpango maalum kwa ajili ya kuukomboa Mkoa wa Shinyanga kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wa Kahama wamenituma niseme kwamba ile *scheme* ya Chela wameipa jina la Mzee Pinda. Ndiyo maana nasema wananchi wa Shinyanga wana imani na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, nina imani Waziri Mkuu amenisikia na kwa sababu hali anaijua, naomba itafutwe njia mbadala ya kuweza kuiondoa hali ya hewa mbaya iliyopo Mkoa wa Shinyanga. Vinginevyo, tutasimama kila siku humu ndani tunaomba chakula cha njaa. Hatutaki kuitwa ombaomba wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo naomba niende upande wa elimu. Kila siku tunaulizana, tunasema elimu imeshuka. Tunajua sababu za kushuka elimu? Kwa utafiti niliufanya, elimu inashuka kwa sababu shule zetu hazikaguliwi.

Inasikitisha sana na ninawaomba Wabunge wote mniunge mkono kwa hili na hata kama hamjalielewa, ulizeni kwenye Halmashauri zenu mtaambiwa. Nimekaa na Wakaguzi wa Elimu wa Mkoa mzima wa Shinyanga, Wilaya zote wameniambia Kitengo cha Ukaguzi kimetelekezwa. Hawajui bajeti yao inatoka wapi. Mwaka wa Fedha tunaomaliza sasa hivi Idara ya Ukaguzi, Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga walipewa Sh. 400,000/=, Manispaa ya Shinyanga walipewa Sh. 200,000/=, wanazifanyia kazi gani? Wakaguzi hawa walinihakikishia hili ni kwa nchi nzima, ndiyo maana nimesema Waheshimiwa Wabunge nawaomba mniunge mkono kwa hili. *(Makofi)*

Unapowapelekea Sh. 200,000/= kwa ajili ya kukagua shule Halmashauri ambayo ina Kata 17, anakwendaje? Hiyo fedha anaiwekea mafuta au anafanya *service* ya gari? Inasikitisha. Haitoshi, watumishi hawa huduma zote za kijamii hawazipati. Mtumishi wa Idara ya Ukaguzi anapofiwa, hana mtu wa kumwambia pale Wilayani ni mpaka Katibu Mkuu Wizara ya Elimu. Tunakwenda wapi? Hata akiugua ni mpaka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu. Nalisema hili kwa masikitiko makubwa, nawaomba Waheshimiwa Wabunge mnisaidie kwa hili. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapoinuka kujibu nipate majibu sahihi. Wamenituma Wakaguzi wa Idara ya Elimu, wanasema kama hamwezi kukijali kitengo kile na kitengo kile kilianzishwa kisheria, basi warudisheni madarasani wakafundishe kwa sababu hamwatendei haki. Kwa sababu muda haunitoshi, naomba niishie hapo, lakini nilikuwa nayo mengi ya kusema katika Idara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihamie upande wa Afya. Mkoa wa Shinyanga tuna Hospitali ya Mkoa, lakini Hospitali ile haikidhi mahitaji ya wananchi wa Mkoa wa Shinyanga. Wanawake wa Mkoa wa Shinyanga wamenituma niseme haya yafuatayo: Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga inahudumia Wilaya tatu ambazo hazina Hospitali za Wilaya za Kishapu, Wilaya ya Shinyanga Vijijini na Manispaa ya Shinyanga. Tunaitazamaje Hospitali hii ya Mkoa kwa kuhudumia Wilaya Tatu? Inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sioni fungu lolote ambalo Serikali wameitazama Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. Lakini bado haitoshi, Mkoa wa Shinyanga tumejitahidi kujenga Vituo vya Afya. Nitoe mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Jimbo la Solwa tuna Vituo vya Afya vinne. Wananchi kwa nguvu zao wameanzisha ujenzi wa Vituo vya Afya vingine vinne, wameanzisha ujenzi wa Zahanati 14. Lakini mpaka hivi ninavyoongea, Serikali haijaweka mkono wake pale. Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wameanzisha kwa nguvu zao wenyewe ujenzi wa hospitali ya Wilaya. Hospitali hiyo ya Wilaya, Waziri Mkuu alikuja na akaweka jiwe la msingi. Naomba Serikali itutazame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa, nitoe shukrani za dhati kwa

Serikali yetu kwa jinsi ambavyo sasa hivi imeanza kuiangalia Mikoa ya Kusini kwa macho mawili. Baada ya shukrani hizo, nitoe ujumbe kwa Serikali ambao nimeagizwa na wananchi wa Tunduru, Majimbo yote mawili. Wanahoji kwa nini viongozi wa kitaifa hawatembelei Wilaya ya Tunduru? Tunaamini kabisa ujio wao utahamasisha wananchi katika uzalishaji, utaleta matumaini kukiunga mkono Chama chao Chama cha Mapinduzi pamoja na Serikali yao. Kwa hiyo, nawaombeni sana viongozi wa Kitaifa pamoja na Mawaziri mitembelee Tunduru, wananchi wanawahitaji sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunduru, zao letu kubwa la uchumi ni kosho. Hadi leo ninavyozungumza, tani zipatazo 5400 ziko Tunduru hazijauzwa. Pamoja na jitihada kubwa sana za Serikali, kutafuta mnunuzi, lakini hadi leo korosho zile zipo, wananchi wanapata shida. Naomba sana kasi ya kuhakikisha kwamba korosho zile zinanunuliwa haraka iongezwe kwa sababu hali ya wananchi kwa kweli ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la korosho, licha ya suala la manunuzi, lakini vile vile zao la korosho linaambatana na pembejeo. Hivi ninavyozungumza, hata mfuko mmoja wa *sulphur* haujafika Tunduru na muda wa kupulizia muda wowote utakuwa umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, korosho zinatakiwa kupuliziwa kwa Wilaya ya Tunduru kuanzia mwezi wa tano, hatukupulizia. Mwezi wa sita unakwisha, ikishafika tarehe 5 Julai, maana yake uzalishaji wa korosho

Tunduru utakuwa hamna. Nani atakayelipa fidia kwa gharama kubwa ambazo wakulima wamezitumia katika kuyaanda yale mashamba? Mara zote Mheshimiwa Waziri Mkuu anapoahirisha Bunge, anahimiza Wabunge warudi Majimboni wakakae na wananchi, wawahimiza juu ya masuala ya uzalishaji wa Kilimo na tumefanya hivyo; na ishara kwamba tunafanya hivyo, kuwahimiza wananchi wakulima wazalishe zaidi, ni kutokana na takwimu. Tumelipokea Jimbo la Tunduru mwaka 2007, uzalishaji ulikuwa tani 2500, mwaka jana uzalishaji umepanda mpaka tani elfu saba karibu na mia nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na lengo mpaka kufikia mwaka 2020 tuzalishe tani 12,000. Je lengo hili litafikiwa kama wale tuliowapa dhamana ya kutuandalia pembejeo wanazembea? Naomba nitoe wito kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu msiwaachie hawa watu ambao tumepewa dhamana watuletee pembejeo mkiwa mnaamini kabisa kwamba watafanya vizuri. Mwatembelee na mwaulize wamejiandaa kiasi gani? Wamefikia wapi? Lakini mkisema kwamba watafanya, matokeo yake ndiyo hayo, mpaka leo na Mikoa yote ya Kusini hawajapata *sulphur* hadi leo. Msije mkaona ajabu kama hali hii itaendelea na uharibifu mkubwa ukatokea kwenye mikoroshu yetu tukaleta hoja maalum ya kuiomba Serikali itulipe fidia kutokana na gharama kubwa waliotumia wakulima bila mafanikio yoyote, kutokana na uzembe wa Watendaji ambao wamekabidhiwa dhamana na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pensheni ya wazee. Hivi hili lina ugumu gani? Hivi mnasubiri mpaka agenda hii iporwe na wale wenzetu? Naomba sana, tafadhali pensheni ya wazee iangaliwe kwa umakini sana. Ikibidi mwaka huu wa fedha, wazee waanze kulipwa pensheni kwa sababu wao ndiyo wanaotuletea yatima, ndiyo wazalishaji wakubwa na hao ndiyo wapigakura wakubwa wa Serikali hii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa na sisi wazee wa humu Bungeni tutapata pia au? Endelea tu Mtutura. *(Makofi)*

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la utawala bora, mimi nadhani pamoja na kuwepo na Kanuni ambazo zinaongoza Wabunge wakiwa Bungeni, nadhani kuna haja ya kuweka vipengele vya Kanuni ambavyo vitawaongoza Wabunge wakiwa nje ya Bunge. Kwa sababu sasa hivi katika sura hii ya kusema kwamba tunaeneza Chama chetu, baadhi ya Wabunge wanakwenda kwenye Majimbo ya wenzao na kuanza kuwashambulia na kuwatukana. Leo Mbunge wa Jimbo lingine anakuja Jimbo la Tunduru anaanza kunishambulia mimi; unadhani wapigakura wangu watakuwa na ridhaa? Wasipokuwa na ridhaa, je huoni kama amani itatoweka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito, kama tabia hii ya Mbunge mmoja kwenda kwenye Jimbo lingine kuanza kushambulia na kutoa uzushi na maneno ya

uwongo, hayo magwanda watayaachia kule kule Tunduru. *(Makofi)*

Hii naeleza kabisa, tunakubali waje watoe sera zao, hatuna ugomvi nao, lakini wakianza kusema ah, wananchi wa Tunduru Kusini kwa kweli mmepiga faulu, huyu mliyemchagua ni bomu, kwa kweli hilo bomu litawalipukia kule kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sura hiyo hiyo, baadhi ya Wabunge na viongozi wa Chama fulani, walikwenda Mtwara, Lindi na wakaeneza uwongo. Wanasema kwamba Serikali yenu imeza Bandari ya Mtwara. Napenda kutoa taarifa, mimi kama Mjumbe wa Bodi ya Bandari, hatujauza. Serikali ya Jamhuri ya Muungano haijauza hata mita moja ya Bandari na wala haikusudii kuuza hata mita moja ya Bandari ya Mtwara. Naomba kauli ile muipuuze na ndiyo ishara ya kwamba bado hawajapata madaraka, wanawadanganya wananchi. Wakipata! Naomba wananchi wa Mtwara na Watanzania wote kwa ujumla, muipuuze ile kauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere alisema kupanga ni kuchagua. Tulipanga na Mheshimiwa Rais aliyetangulia wa Awamu ya Kwanza, alitushawishi kwamba jamani tuelekeze nguvu zetu katika maeneo ambayo yatatuletea tija ili tija ile tuweze kuisambaza katika maeneo mengine. Leo baada ya tija kupatikana, Serikali imeanza kuangalia uwezekano wa kusambaza tija ile maeneo mengine. Naomba juhudi hizi Serikali iendeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba nizingumzie msitu wa Mwambesi ambao uko kwenye Jimbo langu la Tunduru Kusini. Msitu huu ni Muungano.

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yenye matumaini na naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Lulindi wamenituma nimpe shukurani za dhati kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa juhudi kubwa iliyofanywa kuhakikisha wanapata malipo ya pili ya korosho ambayo yalikuwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Mbunge wa Tunduru kueleza Serikali kwamba, tabia hii iliyoanza ya baadhi yetu kupita kwenye Majimbo mengine itasababisha kabisa upotevu wa amani katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchaguzi, ni imani ya wananchi kwamba kazi iliyo mbele yao ni

kutekeleza Ilani ya Chama kilichofanikiwa. Kwa hiyo, hakuna anayekataa kwamba viongozi wa Chama wasiende kwenye maeneo, lakini utakapokwenda kuanza kutukana, kukashifu, kwa kweli hili ni jambo ambalo Serikali yetu na vyama vyote vikae ili vilitazame, visije huko mbele ikatuletea matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mtwara una Wabunge mahiri. Tunaye Mheshimiwa George Mkuchika - Mbunge wa Newala, Mheshimiwa Hawa Ghasia - Mbunge wa Mtwara Vijiji, Mheshimiwa Murji - Mbunge wa Mtwara Mjini, Mheshimiwa Mariam Kasembe - Mbunge wa Masasi na mimi ni Mbunge wa Lulindi. Maana yake walikwenda pale wakasema mbona sisi hatumjui Mbunge wa Lulindi? Sasa nataka niwaambie, mie ndiye Mbunge wa Lulindi na ndiye niliyechaguliwa na kupewa ridhaa na wananchi kuwaongoza, kuwawakilisha katika Jimbo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwaambie kwamba sisi tuko mahiri katika kutekeleza Ilani ya Chama chetu. Kazi mbalimbali za kuondoa kero za wananchi zimeshaanza kutekelezwa na ninaamini mpaka mwaka 2015 kero nyingi zitakuwa zimetatuliwa. Kwa hiyo, ningepomba sana tujenge mahusiano mema, tusitengenezeane chuki isiyokuwa na sababu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mikoa ya Kusini nataka niwaambie kwamba, kwa muda mrefu sana walikuwa kwenye matatizo makubwa sana. Tatizo la kwanza lilikuwa mawasiliano. Palikuwa hakuna

barabara, walikuwa wanakaa wiki mbili barabarani kuja Dar es Salaam, lakini Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, sasa wanatumia masaa kufika Mtwara, Masasi, Newala. Unapotoka kwenda kuwaambia CCM au Serikali hii haikufanya lolote, wanakusikiliza tu na wanakuacha utoke, urudi kwako. Kwa hiyo, ndugu zangu nataka niseme tu kwamba, nchi hii ni ya amani, tuendeleze amani yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nije sasa kwenye maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyagusia, kwanza upande wa kilimo, hususan zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la korosho lina mlolongo mrefu sana, lakini ikiwemo na hujuma zinazofanywa kwa wakulima wetu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali iwe makini sana kuwaangalia wale ambao hawataki kuwa na mabadiliko na kutaka mwananchi aendelee kunyanyaswa na zao lake. Tulikuwa na tatizo la soko lilliloambatana na hujuma tu, na wakati Serikali ilipompata mnunuzi, tayari korosho ilinunuliwa kwa wiki moja tu, kwa sababu wanunuzi walikuwa wamesusia kununua zile korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa tuna tatizo la pembejeo linatokana na mambo mbalimbali. Moja, hazina huchelewesha kutoa fedha za *export levy* zinazonunua pembejeo. Hivi ninavyosema, hazina bado haijatoa fedha karibu Shilingi bilioni sita zinazotakiwa kwa ajili ya kwenda kulipia pembejeo. Lakini la pili, pembejeo zile ambazo zinahitajika kule,

sana sana ni ile *sulphur*, za maji zinapatikana vizuri, lakini *sulphur* ambayo ndiyo wananchi wengi wanaitaka, imekuwa ni tatizo kubwa sana. Ningeishauri Serikali, fedha zinazopelekwa kwa ajili ya ulipaji wa pembejeo zipelekwe kwenye vyombo vya Serikali na siyo mfuko ambao ni wa wakulima.

Vyombo vya Serikali vitakuwa na mamlaka kuweza kudhibiti fedha zile. Lakini tatu, natoa ushauri kwa Serikali, tunayo kampuni ya mbolea *TFC*; hivi ni kwa nini na yenyewe isihusishwe katika zoezi zima la kuandaa pembejeo za ruzuku? Tunawategemea watu binafsi ambao baadaye hawatuletei pembejeo. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali turudi kwa *TFC*, *TFC* itusaidie kuleta pembejeo za ruzuku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu labda nije kwenye eneo ambalo uliligusia kwenye ukurasa wa 29, ni juu ya kuweka thamani ya mazao yetu. Korosho ni zao lenye tija kubwa sana na ndilo ambalo linaweza kuliingizia Taifa hizi fedha nyingi sana za kigeni. Ningeomba ushauri uliotolewa na Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwenye Bunge lililopita la kutaka viwanda vile vilivyokuwa vimechukuliwa na watu ambao hawaviendeshi sasa, virudishwe na utaratibu ufanyike ili viwanda vile vianze kufanya kazi. Kwa hali ya kawaida tu, nchi yetu inapeleka tani zaidi ya laki moja nchini India ili zikabanguliwe na hatimaye India wao ndiyo wanapeleka kwenye nchi nyingine kwenda kuuza. Kwa kweli ni lazima Serikali hii tukiandae ili tuhakikishe kweli korosho zetu zinabanguliwa na ziweze kuongeza thamani na mkulima wetu apate bei nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekee kwenye suala la umeme. Napenda kuishukuru *TANESCO* kwa juhudi ilizoanza kwenye Jimbo la Lulindi kwa kuanza kufanya *survey* katika Vijiji vya Nanjota, Chiwata, Ndibwa, Mbuyuni, Lwatala, Mchahuru pamoja na Mnavira. Naiomba Serikali ihakikishe kwamba Vijiji hivi sasa kupitia Mfuko wa *REA* umeme huu uweze kuwekwa haraka iwezekanavyo ili kuwa ni kichochea cha maendeleo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikitaja Wabunge, nilisahau kumtaja rafiki yangu Mheshimiwa Njwayo wa Tandahimba pamoja na Mheshimiwa Mkapa wa Jimbo la Nanyumbu. Katika majemedari hodari wa Mkoa wa Mtwara ambao wamepewa dhamana hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningepomba sana *REA* wafanye kila linalowezekana kuhakikisha umeme unapatina katika Vijiji hivyo ili hali ya uchumi katika eneo hilo iweze kubadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mfupi, naomba nimalizie suala la maji. Wananchi wa Jimbo la Lulindi wana shida kubwa sana ya maji. Maji yapo, tatizo ni kuyaondoa pale yalipo na kuyafikisha kwa wananchi. Naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwenye mradi huo wa Shilingi milioni 580, imekwishaanza kupelekwa Shilingi milioni 50, nategemea kwenye bajeti hii fedha zitapatikana zaidi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa
Mzungumzaji kwisha)*

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama katika Bunge lako leo. Lakini niwakumbushe Watanzania wenzangu kwamba amani wanayoichezea leo, watakuja kuikumbuka siku machafuko yatakapotokea. Kama hawaamini, waende Sirya, Somalia na Sudan, wana majumba mazuri ya kuishi, magari lakini wanashindwa kuyatumia kwa sababu ya machafuko. Sikuamini niliposikia Mbunge aliyeapishwa, aliyeapa kwa kutunza na kuheshimu Katiba ya nchi, anaweza kusema kwamba Waziri Mkuu sio makini. Nasikitika, lakini kwa sababu amesema, nadhani hayo ni mawazo yake, siyo mawazo ya Watanzania na wala siyo mawazo ya Wabunge ambao tuko humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupa *RC* mzuri, makini Dkt. Rehema Nchimbi, mwanamke mwenye uwezo, hata ukipiga simu saa 8.00 usiku yuko macho, lakini cha kunisikitisha ni kwamba Mkuu wetu wa Mkoa hana Ofisi. Idara zake zimetawanyika kila mahali na sijui anafanyaje kazi yule mama. Lakini kwa sababu ya kuipenda nchi yake na kuipenda Mkoa wake na kupenda kazi yake, yule mama halali. Ninaiomba Serikali kufikiria kwa sababu pesa zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo lake ni pesa kidogo sana. Makao

Makuu ya nchi, Mkuu wa Mkoa hana Ofisi, ni aibu! Naomba pesa zitafutwe kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ili yule mama aendelee kufanya kazi zake kwa ufanisi na kwa karibu zaidi na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo, hospitali yetu ya Mkoa ilijengwa mwaka 1923, wakati huo wakazi wa Dodoma hawakuwa wengi hivi, na sasa uongozi wa Mkoa wanajitahidi sana kujenga hospitali, na tumeanza wodi ya wanawake na watoto tangu mwaka juzi wakati Mheshimiwa Lukuvi ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma. Lakini kila mwaka tunaomba pesa. Mwaka jana tuliomba Shilingi milioni 800, tukapewa Shilingi milioni 400 tu, mwaka huu tumeomba pesa, jingo lile wanalala popo na mijusi wakati limejengwa kwa ajili ya wanawake kupata matibabu pale. Ukienda hospitali ya Mkoa, wanawake wanalala wawili, watatu kwenye kitanda kimoja. *(Makofi)*

Siyo haki. Naomba mwaka huu, nimeona pesa kidogo sana lakini Waziri Mkuu, ninaimani na wewe kwamba, unaweza ukafanya unavyojua ukaongeza pesa kidogo pale ili jengo letu lile limalizike. *(Makofi)*

Vilevile kuna tatizo la umeme. Umeme uliowekwa mwaka 1923, matumizi yake sasa ni makubwa zaidi. Naomba sasa, miundombinu ya umeme katika Hospitali ya Mkoa, ifanyiwe ukarabati. Naomba sana kwa sababu, umeme unatumika sana kwa wagonjwa, hasa wakati wa upasuaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumze tena suala la *CDA*. Mwaka jana katika bajeti iliyopita tuliambiwa kwamba *CDA* wanapima viwanja na hasa Mji wa Serikali lakini pesa hazikutolewa ili *CDA* waweze kupima viwanja kwa ajili ya Mji wa Serikali na kwa ajili ya wananchi wanaotaka viwanja. Wabunge wananisumbua wanataka viwanja, leo nawatangazia Wabunge kwamba Mwenyekiti wa *CDA* ni Mheshimiwa Lukuvi, mfuateni awape viwanja. Nimeona hapa wameandika kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu kwamba *CDA* waligawa viwanja 1,728 kwa mwaka jana; mimi ninavyojua tangu mwaka 2008 *CDA* hawajaweza kuuza viwanja wala kugawa viwanja kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi wangependa kujenga Dodoma kwa sababu Dodoma ni Makao Makuu. Wabunge mnahangaika kutafuta nyumba za kuishi lakini mnashindwa kujenga kwa sababu hamjapewa viwanja na *CDA*. *CDA*, ninakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, hebu panga bajeti ya kutosha kwa ajili ya *CDA* na *CDA* waweze kupima viwanja. Manispaa wanagombana na *CDA* kwa sababu ya ukosefu wa viwanja tu lakini nadhani kama *CDA* wangepewa pesa za kutosha, wangepanya kitu kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mapitio ya Mji, mapitio ambayo yamefanywa na Mtaalamu ambaye ameajiriwa na *CDA*. Mtaalamu yule anaidai *CDA* shilingi milioni 540. Pesa zilizotengwa kwa ajili ya *CDA*, hazitoshi kumlipa Mtaalamu yule. *CDA* hawawezi kugawa viwanja kutokana na bajeti ambayo wametengewa na wala hawawezi kumlipa yule

mkandarasi ambaye amefanya mapitio ya Mji wetu wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, *CDA* kazi yao sio kugawa viwanja tu, wanapasua barabara na kuzikabidhi kwa Manispaa. Hawawezi kufanya kazi hiyo kama hawana pesa za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine, mwaka jana Wilaya ya Kongwa, waliomba shilingi milioni 40 tu kwa ajili ya kujenga wodi, hizo pesa hazikuja. Naiomba Serikali mwaka huu tupate pesa kwa ajili ya kujenga wodi pale Kongwa. Pesa hizo naomba ziwahi kuja kwa sababu pesa zinazoletwa mwisho wa mwaka huleta lawama hata kwa watumishi na *CAG* huwa anahoji sana pesa ambazo zinabaki mwisho wa mwaka lakini wafanyeje watu wa Halmashauri kama pesa zinaletwa robo ya nne? Hawawezi kufanya kitu chochote cha maendeleo kwa sababu ndio mwisho wa mwaka. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka huu ujitahidi basi pesa za maendeleo ziwahi kufika ili Halmashauri wafanye maendeleo ambayo wamepanga. Sisi Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani na tunaona kipindi ambacho pesa zinapelekwa katika Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Dirisha la Kilimo. Dirisha la Kilimo liko *TIB* lakini mwananchi wangu wa Dodoma anaweza kwenda Dar-es-Salaam akakaa siku ngapi kutafuta mkopo *TIB* kwa ajili ya Kilimo Kwanza? Naiomba Serikali sasa walete dirisha hilo *NMB*, *TIB* wawe na Mkataba na *NMB* ili pesa ziende *NMB*

kwenye matawi yote ili wananchi waweze kukopa. Ukimwambia mwananchi wa Kondo kule, aende Dar-es-Salaam, afuatilie mkopo wake *TIB* ni kazi pevu na mkopo wenyewe anaweza akaumaliza akila hotelini na kulala gesti. Nashauri Dirisha liwepo *NMB* kwa ajili ya mkopo kwa wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ipo pia Benki ya Wanawake. Benki ya Wanawake ipo Dar-es-Salaam, mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, mpango uwepo wa Benki ya Wanawake, wanawake wana hamu ya kukopa na ni waaminifu katika kurudisha na ni waaminifu katika biashara lakini benki ipo Dar-es-Salaam. Naomba sana Serikali yetu ione namna ya Benki ya Wanawake kuwa na Matawi katika *NMB*, mahali walipo wananchi walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nakerwa sana na suala la *By Election*, pale ambapo Jimbo linabaki wazi. Tunapoteza muda mwingi sana kushughulikia *By Elections*, tunapokwenda kwenye chaguzi ndogondogo. Mimi naomba Serikali iweke utaratibu kwamba Jimbo linapokuwa wazi, Serikali iweke utaratibu mwingine, wananchi wanapoteza muda mwingi, vyama vya siasa, watu wanapigana huko, watu wanapoteza muda mwingi bila kufanya shughuli za maendeleo na uvunjifu wa amani. Tuliona Arumeru, tumeona Igunga, mimi naomba Serikali itafute njia mbadala; inapotokea Jimbo liko wazi, Serikali ifanye utaratibu mwingine na waangalie nchi nyingine wanafanyaje, Jimbo linapobaki wazi nchi nyingine wanafanyaje, tu-*adopt* mambo kama haya, halafu yatatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hoja ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba sitaunga mkono hoja hii kwa sababu ya mambo makubwa mawili. Jambo la kwanza, ni jambo ambalo hata mwaka jana nimelizungumza, suala la ukubwa wa Serikali. Suala la pili ni suala zima la kutotekeleza yale yaliyoandikwa katika *speech* yake ya mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na la kwanza. Nimepitia *speech* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya mwaka jana na ya mwaka huu, nimemsikiliza kwa makini sana. Katika *speech* yake ya mwaka jana, suala la ulinzi na usalama, naomba ninukuu alisema:-

“Aidha hatua zimechukuliwa kwa kupanua, kuhakikisha kwamba wanakabiliana na msongamano kwenye Magereza kwa kupanua na kukarabati Magereza na kutoa vifungo vya nje.” Lakini katika *speech* ya mwaka huu, suala hilo halijazungumzwa hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wajumbe wa Kamati ya UKIMWI ya Bunge hili, tumepita katika

Magereza mbalimbali Jijini Dar-es-Salaam, tukiongozana na Mawaziri au Manaibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani; huwezi kuamini kama Mahabusu wanaishi katika hali ile. Tumeenda katika Gereza la Keko, vyumba ambavyo walikuwa wanatakiwa wakae Mahabusu watatu, sasa hivi wanakaa zaidi ya 15. Vyumba ambavyo walikuwa wanapaswa kukaa 15, wanakaa kuanzia 75 na mpaka 100 na kuendelea, lakini baya zaidi kwa hali ya hewa ya Dar-es-Salaam ya joto, Mahabusu wale wanafungiwa ndani kuanzia saa 10.00 jioni. Hali iliyoko pale ni *pathetic*, hauwezi kuamini uko Tanzania. Tumeenda Segerea, hali ni hiyohiyo na Waheshimiwa Viongozi Wakuu wa Nchi wanapita wanaona. Lakini kibaya zaidi katika bajeti ya Serikali, *Volume IV*, ukiangalia katika eneo la *Prison*, hakuna fedha imetengwa. Imetengwa shilingi milioni 65, fedha za ukarabati wa Magereza. Hivi kweli milioni 65, hata nyumba ya kawaida ya vyumba vitatu vya kisasa haitoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana mtu akiwa Magereza, hana tena haki ya kuwa Mtanzania? Utanzania unakuwa haupo? Hakuna utu kabisa katika Taifa hili katika watu wanaoishi mahabusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wote tunajua ni jinsi gani janga la UKIMWI limekuwa likiendelea katika nchi nyetu na mahabusu wale wanasema waziwazi ni mambo gani wanayafanya katika Magereza yale, sitataka kusema, lakini hali wanayoishi, hali wanayolala, ni moja kwa moja watoto wale au vijana wale wamesharibikiwa. Kwa hiyo, naomba, kama

kweli tunataka ulinzi na usalama na tunawatakia heri Watanzania wetu, ni lazima tuhakikishe kwamba, Magereza yetu yanapanuliwa, Mahabusu wanaishi kama raia wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo ambalo linasikitisha zaidi, kuna ambao wako Mahabusu ambao hawakupaswa kuwepo. Hivi ni kwa nini wasipewe adhabu za nje? Mtu anapatikana anazurura Dar-es-Salaam, Mitaani, anawekwa Mahabusu. Ni kwa nini, asipewe hata kazi za usafi wakati tunajua Majiji kama Dar-es-Salaam ni machafu sana, kwa nini wasifanye kazi hizo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, naomba niende kwenye suala zima la elimu. Elimu ni jambo la muhimu sana, lakini nataka niseme waziwazi kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imepuuza suala la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na mchangiaji aliyeongelea suala la *inspectorate*. Ni wazi kwamba elimu ya Tanzania inaendelea kushuka kwa sababu Kitengo cha Ukaguzi kimeachwa yatima. Nimeongea na Watendaji na nielezee tu katika Wilaya moja, walipaswa kupata shilingi milioni 78 lakini walipewa shilingi 600,000/= tu kwa mwaka jana. Sasa shilingi 600,000 hata 1% haifiki, tunawategemea watu hawa watafanyaje kazi zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inakuwaje tunashangaa kwamba elimu yetu inaporomoka wakati tunaona watoto wanamaliza darasa la saba, naomba

hili Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Elimu watuambie, inawezekanaje mwanafunzi afanye mtihani wa darasa la saba afaulu, lakini mtoto huyo hajui kusoma wala kuandika? Naomba maelezo ya kina. Ni wazi hatuna Walimu wa kutosha, ni wazi tuna mazingira magumu sana kwa Walimu wetu. Hata sisi wakati tunasoma kulikuwa na wanafunzi wanaweza kumaliza hawajui kusoma wala kuandika lakini inawezekanaje mwanafunzi huyo ambaye hajui kusoma wala kuandika afaulu darasa la saba?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani hii ni *scandal* ya Taifa na ni lazima Waziri wa Elimu na Waziri Mkuu, watueleze ilikuwaje wanafunzi zaidi ya 300 katika Tanzania mwaka jana, mtihani wa darasa la saba, wamefaulu lakini hawawezi kusoma wala kuandika. Lakini haikuishia hapo tu, Serikali, ikaamua watoto wale wafanye mtihani. Watoto wale, katika watoto zaidi ya mia tatu, 100 walitoroka, lakini wale waliopewa walau aandike jina, aandike Waziri, akopi, ameshindwa. Sasa tunaomba kujua ni *system* gani ilitumika au ni mambo gani yamefanyika mpaka wanafunzi waweze kufaulu wakati hawajui kusoma wala kuandika? Tunaipeleka wapi nchi yetu? Serikali, haijasema lolote kuhusu suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la ukubwa wa Serikali. Hili nililizungumza mwaka jana na naomba nilizungumze tena. Ni kweli Rais na Viongozi Wakuu pamoja na Waziri Mkuu, wamekuwa wakisafiri nchi mbalimbali na tumekuwa tukipewa misaada na nchi mbalimbali, ambapo nchi hizo ukiangalia Mabaraza yao ni madogo sana. Tunapata misaada

kutoka Serikali ya Marekani, tunapata misaada kutoka Japan, lakini nikichukulia mifano ya nchi hizi mbili tu au Norway, unakuta Baraza lao halina zaidi ya Mawaziri 15 mpaka 20, lakini Tanzania tuna Baraza la Mawaziri 58, hii ni aibu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tuangalie na *population*, Marekani ina zaidi ya watu milioni 314, Tanzania ina watu milioni 42, kama mara saba (7), lakini bado tuna Baraza kubwa ambalo halina tija. Vilevile Baraza hilo sasa hivi kwa kuwa Madaraka ya Rais ni makubwa sana, ameamua kuongeza Waziri asiyekuwa na Wizara; *Minister without portfolio*, maana yake ni nini? Huyu pia anatumia gharama za Serikali, gharama za walipa kodi. Kwa hiyo, tulikuwa tunadhani ni lazima Serikali iwe sikivu, iangalie ni jinsi gani inaweza kupunguza ukubwa huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninataka kuongelea ni suala zima la agizo alilotoa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Nampongeza sana kwa agizo lile kwamba, wananchi wasikate miti lakini naomba nimwambie kwamba agizo hilo Watendaji wake wamelitumia vibaya, sasa hivi Mkoani Kilimanjaro hususan Wilaya ya Moshi Vijijini, Watendaji, hususan Polisi na watu wa *KINAPA*, wamekuwa wakipita majumbani mwa watu, wakikuta mtu ana mbao moja au mbili ambazo amevuna kwenye shamba lake na miti hiyo wala sio ile ambayo imekataliwa na Serikali, wanaichukua, wanaipora, wanapeleka Polisi. Kibaya zaidi, kama mtu alikuwa na mbao zaidi ya 10, zinapelekwa mbao mbili (2), zile nyingine zote

zinataifishwa na wanaenda wanajiuzia. Kwa hiyo, naomba kumwambia Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO:...pamoja na agizo lake hilo zuri, lakini naomba Watendaji wafanye kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ... *(Makofi)*

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kabla sijaanza kuchangia, ningependa kutoa pole kwa Makada wetu wawili ambao wamefariki jana, Katibu wa Kata ya Makurumla, kwa kupitia Chama cha Mapinduzi, anaitwa Thabit Alawi Ntanda na Katibu wa Malezi na Uchumi, Haida Mtei. Nazipa familia zao pole, Mwenyezi Mungu, azilaze mahali pema peponi roho za marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kuchangia katika suala la maji. Napenda kuanza kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutenga fedha za kuweza kutatua kero ya maji katika Jiji la Dar-es-Salaam. Kwa kuwa, mpango huu ni maalum, ulioidhinishwa mpaka mwaka 2014, tatizo la maji Dar-es-Salaam liwe limekwisha, naipongeza sana Serikali yangu kwa hatua hii. Hivyo basi, naomba pia nichukue nafasi hii kuiomba Serikali kwamba ushuru katika dawa ambazo zinatumiwa kusafishia maji uweze

kutolewa ili kuwasaidia Watanzania kupata maji safi na salama na kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuikumbusha Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwamba bado tatizo la maji vijijini limezidi kuwa kubwa siku hadi siku. Vijijini kuna matatizo makubwa sana ya maji. Watanzania wetu wanakunywa maji ambayo ni machafu. Ukiangalia vijiji vingi katika Mkoa ambayo iko Tanzania, napenda kuzungumzia Mkoa wa Njombe, kuna vijiji vingi ambavyo vina shida sana ya maji; vijiji vya Dulam, Parangavano, Masimbwe, Ilula, vyote hivi vina shida ya maji. Kwa kweli, kule maji wanayokunywa ni machafu na upatikanaji wake wenyewe ni mgumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nzungumzie suala la gesi na pia kwa kuanza kuipongeza Serikali yangu kwa kuongeza kasi ya upatikanaji na ugunduzi wa gesi asilia nchini, ikiwa ni sambamba na kufuta kodi katika vyombo vinavyotumia gesi, ikiwa ni pamoja na majiko yanayotengenezwa kwa matumizi ya gesi. Hii itamsaidia mwanamke wa Tanzania kuweza kupata unafuu na gharama katika matumizi ya nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya *Tanzania Household Survey*, inaonesha kwamba, kuni zinatumiwa kwa 90%. Hivyo basi, hii nayo itatusaidia katika kulinda mazingira yetu ya Tanzania. Si hivyo tu, unaweza ukaona kwamba, suala la gesi ni suala dogo sana, lakini kama tutaitumia vizuri, kama Serikali itawaelimisha wanawake katika matumizi ya gesi, hili

suala litatusaidia kufikia malengo ya milenia katika suala la usawa wa jinsia katika suala zima la elimu, ili kufikia 50% sababu, wanawake wengi wa vijijini wanatumia kuni na wanaokwenda kutafuta kuni ni watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie pia suala la lishe, naipongeza Serikali yangu kwa kutambua umuhimu wa lishe bora kwa Tanzania ikiwa ni sambamba na kutoa ushuru katika virutubisho vya chakula na madini yanayotumika katika kutengezea vyakula. Hivyo basi, tuna uhakika wa watoto wa Tanzania kuwa na afya bora. Lakini taarifa ya *Domestic Health Survey* inaonesha kwamba katika watoto 100 watoto 42 wamedumaa na hali ni mbaya Mkoa wa Dodoma, ni asilimia 56, Lindi asilimia 54, asilimia 50 kwa Rukwa na Mbeya. Kwa kutoa ushuru tu katika virutubisho hivyo na madini, hiyo haitoshi bali naiomba Serikali yangu iweze kutoa elimu na kuhamasisha wanawake waweze kutumia vyakula hivyo bora kwa kuwapa watoto wetu ili tuweze kupunguza matatizo ya afya kwa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la udhibiti wa matumizi ya Serikali na hii napenda kujikita katika ubadhirifu wa fedha za umma. Naomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho aweze kuniambia kwamba zile Kamati za *Auditing* ndani ya Wizara, Halmashauri zinafanya kazi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba hawa *Chief Internal Auditors* ndani ya Wizara, ndani ya Halmashauri zetu ndiyo chachu kubwa ambapo

wanagundua ubadhirifu wa fedha za Serikali ndani ya Wizara na ndani ya Halmashauri zetu. Hivyo basi kitendo cha *Chief Internal Auditor* kwenda kuripoti kwa Katibu Mkuu au kuripoti kwa Mkurugenzi wake, hii inanyima fursa na inajenga mianya ya rushwa ndani ya Halmashauri zetu na ndani ya Wizara yetu. Hivyo basi, naomba hawa *Chief Internal Auditors* waweze kuripoti katika Kamati za *Auditing* badala ya kuripoti kwa Makatibu Wakuu na Wakurugenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala afya na hapa pia napenda kuipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya pesa katika dawa. Kuongeza bajeti tu ya pesa haitoshi, naishauri Serikali iongeze udhibiti wa dawa kutoka *MSD* hadi kwa mlaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile sitosita kuipongeza Serikali yangu kwa kuweza kuanza kuwalipa *On Call Allowances* za Madaktari na wafanyakazi wa afya na pia kuweza kuboresha madai yao mbalimbali kwa asilimia kubwa. Ila nakemea vikali vitendo vya migomo ya Madaktari kwani waathirika ni watu ambao hawana hatia. Hivyo basi, naiomba Serikali yangu na uongozi wa Madaktari panapokuwa na jambo hilo la migomo, wakae wazungumze na Serikali na waweze kufikia muafaka na siyo kugoma, kwa kugoma kunawateketeza watu ambao hawana hatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nizungumzie migogoro ya wafugaji na wakulima. Migogoro ya wafugaji na wakulima imekuwa ikienea

kwa muda mrefu na migogoro hiyo haiwezi kuisha kwa sababu wafugaji wanataka mfugo wake uweze kupata maji wakati huohuo mkulima naye anataka mazao yake yastawi. Kwa sababu wafugaji hawajatengewa mazingira rafiki ya kuweza kuwanyweshwa wanyama wao sehemu ambazo haziingiliani na wakulima, hivyo, naishauri Serikali kwa kupitia Wizara ya TAMISEMI, iweze kuwandaalia miundombinu vizuri wafugaji ikiwa ni pamoja na kuwajengea mabwawa na majosho kwa ajili ya kuwapatia maji wanyama wao ili wasiweze kuingiliana na wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niipongeze Serikali yangu kwa kuandaa mikakati mbalimbali ya kuweza kuwapatia vijana mitaji ili waweze kujiendeleza kiajira lakini bado naiomba Serikali iweze kufuta kodi ya bodaboda ingawa hao wamiliki wa bodaboda si vijana lakini walioajiriwa kufanya kazi hizo za bodaboda ni vijana. Kitendo cha kuweka kodi katika bodaboda kitawafanya wale watu ambao wame-*invest* katika biashara hiyo ya bodaboda kuachana na biashara hiyo na vijana hao watarudi tena kijiweni, watakosa kuwa na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimalizie kwa masikitiko makubwa na naungana na Wabunge wenzangu wa Dar es Salaam waliopita Dkt. Ndugulile na Mheshimiwa mwingine aliyeongea leo kuhusu ile kauli yake ya tarehe 16 Augosti akisema kwamba atakutana na Wabunge wa Dar es Salaam ili kujua kero...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Neema Hamid, simwoni Mheshimiwa Said Arfi, naomba nimwite Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Fakharia Shomar ajiandae.

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na leo kunipa uwezo kuichangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, naipongeza ofisi ya Waziri Mkuu, vilevile na watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliyotuletea hapa leo kwa sababu hotuba hii ni nzuri na ndiyo maana ukaona orodha iko kubwa kila mmoja anataka kuichangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na machache tu ya kuboresha. Kwanza nilikuwa nataka kulizungumzia suala la chenji ya Rada. Najua wenzangu wengi wamelizungumza hilo lakini na mimi sina budi kulizungumza na kila mmoja atalizungumza kwa stahili yake. Mimi nakubaliana kabisa na fedha hizo za Rada kupelekwa shuleni lakini najua Tanzania nizungumzie Bara wao wanazipeleka fedha hizo kwenye elimu ya msingi, zikienda kwenye elimu ya msingi kwa vyovyote Tanzania Visiwani itakuwa haipati kitu. Kwa sababu Muungano wetu siyo kwenye elimu ya msingi, ni elimu ya sekondari. Sasa naomba wangepanya kila mbinu, ikiwa wao wanapeleka kwenye elimu ya msingi wangepeleka kwenye Tanzania Visiwani hapo Zanzibar kwa elimu ya

sekondari ambayo hiyo ndiyo inayostahiki kupata fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa hawafanyi hivyo ile kero ya Muungano inajipenyeza hapo kidogokidogo, ili kuiondoa kero ya Muungano na tunakwenda kwenye Katiba, suala la hili chenji ya Rada naomba kwa sababu hata hizo sekondari na vyo vyetu vinahitaji vitabu, vinahitaji vitendea kazi vya *laboratory*. Sasa kwa vyovyote hela hiyo ikienda itasaidia, maneno mengi hapa yaliyokuwa yamezungumzwa yataweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja sasa kuzungumzia mambo yanayohusu pango ambayo tunaita kodi ya nyumba. Utakuta Wizara nyingi za Serikali hazina ofisi za Serikali zinategemea kukodi na utakuta kodi inayotozwa ni kubwa na utaona kodi kila mwaka ikiwa inatoka basi bora ingekuwa hiyo kodi tukatafuta wafadhii wetu wakatujengea, tukalipa ile pesa iliyokuwa ya kodi, tukalipa kwamba kile kitu tulichojengewa ni chetu na ile pesa tukiipeleka kule tayari tunakwenda kulipa malipo ya kudhibiti kilichokuwa chetu. Lakini tunakwenda kutoa pango kila leo tunamfurahisha mtu mwingine, tunamuumiza mtoa kodi mwananchi, hilo ni tatizo na hapo ndiyo utapoona watu wanaona lazima pesa fulani zinaingia mifukoni, kumbe ni hali halisi, ni sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo lililojitokeza hapa tunapenda kukodi badala ya kujenga maofisi yetu. Tuchukulie mfano Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi wamekodi, tuchukulie ofisi

hizi ni nyeti, zina kazi muhimu ambapo zinategemewa na utakuta ofisi inakodi tuseme hii Tume ya Uchaguzi ya Taifa imepanga majengo ya Posta na Simu halafu utamkuta hapo hapo amekodi majengo mengine Wakala wa Manunuzi anaweka vifaa vyake vya uchaguzi, anaweka daftari la kudumu, sasa hapo tuseme udhibiti uko wapi, yeye mwenyewe ofisi yake iko sehemu nyingine, vifaa vyake vinakaa sehemu nyingine, lakini ndiyo hali halisi, tutafanya nini ina maana badala ya kujenga ofisi tunategemea kukodi na pesa za walalahoi au pesa za wananchi wetu tunazidi kuziangamizi. Sasa mimi naomba jambo hili Serikali iliangalie na tuweze kutafuta wafadhili wetu wa ndani, tuwaombe watujengee na tuwe na maofisi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia kuhusu mabasi tunayotumia Wabunge. Mheshimiwa, mabasi tunayotumia tunapokwenda ziara za kikazi ni mabovu na hayastahiki kupandwa na Waheshimiwa Wabunge, kwanza kutokana na hali yao kimaisha, basi lishakuwa bovu, ndani AC hamna, joto lililokuwepo Tanzania tunalijua, Mheshimiwa katia koti kwamba yeye ni Mbunge, inabidi ndani ya basi alivue, akisema nifungue madirisha vumbi la nje linamtawala. Sasa mimi nahisi kwa wakati huu tuliofikia na haya mabasi tuliyokuwa nayo muda wake umepita, kwa nini yasiuzwe yakanunuliwa mabasi mengine mapya. Jambo kubwa lililokuwa linafanywa na ofisi ya Bunge kukodi mabasi mengine Waheshimiwa Wabunge wapande waende kwenye ziara ya kikazi Mkoani, gharama ni kubwa, hela inapotea nyingi, basi nahisi ikiwa haiwezekani, Waheshimiwa Wabunge magari

yao wanayo, mnapotaka kuwapa kazi watilieni mafuta wafanye kazi zao, warejee kuliko kuwapatia mabasi ya kukodi au kuwapatia mabasi ambayo yamekuwa hayastahiki kutumika. Sasa hilo pia nilikuwa nataka kuliongelea na Mheshimiwa ulione na muweze kufahamu kwamba hali ya mabasi yetu hayaridhishi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa nikuhakikishie Tume ya Huduma za Bunge imesikia hayo maoni yako, ahsante, endelea. (*Makofi*)

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nililotaka kulizungumza ni mabasi yaendayo kwa mwendo wa kasi. Hiki ni kitendawili na kitataka kuteguliwa kwa sababu muda umekuwa mrefu, mazungumza yamekuwa mengi kila siku tunaahidiwa, ukipita Dar es Salaam kunakuangalia, majengo yamekaa kama mzimu kwa sababu majengo yapo lakini hayamaliziki, sasa imekuwa kitu hiki kitamalizika lini? Ukipita kwenye barabara zinazotengenezwa utakuta uharibifu wa mazingira, kwa sababu badala ya kutengeneza mazingira mara barabara hii haipitiki kumechimbwa, sasa baada ya kutengeneza kitu kiwe kizuri bado tumo katika kutengeneza jambo hajui lini linamalizika. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hoja atuambie kwa uhakika kwamba yale mabasi yanayokwenda kwa mwendo wa kasi tunategemea tarehe kadhaa yatamalizika na yale majengo yanahudumiwa tarehe kadhaa yatamalizika na tunategemea kwamba wananchi wataweza kutumia

wakati utakaokuwa muafaka utakuwa umemalizika.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka nitoe pongezi kwa ofisi yetu ya Bunge, maana naona tayari mko katika mchakato kututayarishia Wabunge Bima ya Afya. Bima ya Afya ni nzuri kwa wakati huu na tena naomba hili Bunge kabla hatujamaliza muda wetu tuanze kuitumia Bima ya Afya kwa sababu inatusaidia sisi wenyewe na watoto wetu wakati tunapokuwa nyumbani au mitaani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Naunga mkono hoja kwa asilimia mia. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, anayefuata ni Mheshimiwa Ester Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Vicky Kamata na Mheshimiwa Abdul Jabil Marombwa ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nitakwenda kuongelea sehemu kama nne hivi itategemea muda utakavyoniruhusu, nitazungumzia sekta ya elimu, afya, kilimo na mauaji ya raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza, napenda kuomba au kushauri, juzi tulipitisha bajeti ya Serikali na

kwa sababu tumesema *Financial Bill* tutai-*discuss* mwishoni, napenda kuomba kama tulivyoamua kuwalegezea maisha wafanyabiashara na kuamua kukata kodi kuanzia kiwango cha shilingi milioni nne kwa mwaka ambapo ni sawasawa kama shilingi 333,000 kwa mwezi, napendekeza pia na kwa wafanyakazi tuangalie, Serikali ilisema imetoa kodi kutoka shilingi 135,000 mpaka shilingi 170,000 basi na hawa wafanyakazi nao tuwafanyia hivyohivyo kwa sababu kwa shilingi 170,000 ni kama shilingi milioni 2,040,000. Tuwaangalie nao waanzie kukatwa kodi kuanzia shilingi 333,000 kwa mwezi. Vilevile tuangalie na vile viwango vingine kama ilivyopendekezwa kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani na namwomba sana Waziri wa Fedha na wataalam wengine waliangalie ili kuweza kuwapunguzia wafanyakazi makali ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikizungumzia sana suala la Nyamongo hadi watu wananiita Miss Nyamongo. Mimi ni Mbunge wa Mkoa wa Mara na ni Mbunge pia ambaye anatakiwa kuliwakilisha Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ifike sasa ione ni vyema kutatua mgogoro uliopo Nyamongo. Tunawakubali wawekezaji lakini hatutafurahia na sidhani kama Serikali inafurahia kuona wananchi wanaendelea kuuwawa kwamba tunapata mapato katika ule mgodi na wala sidhani kama hata mwekezaji anafurahia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na wimbi la mauaji Nyamongo kwa wale vijana ambao wanaenda

kuokota mawe, kama jana Mbunge wa Geita alivyosema, kule kwetu vijana wanaenda usiku au alfajiri kuokota zile *reject*, wanapigwa risasi maeneo ya vifuani, shingoni. Sasa utaangalia huyu anayempiga *intruder* risasi shingoni au kifuani, ni dhahiri amedhamiria kumua. Naomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Waziri alitamka ataunda Tume kuchunguza mauaji yanaendaje mengine yanafanywa na Walinzi wa mgodi wenyewe, wananchi wa Tarime Wakurya, tutasema mnatuona kama wanyama lakini tunastahili kuishi, tunastahili heshima, hatuwezi kulalia migodi, dhahabu, ardhi yetu yote ya Nyamongo pale ni dhahabu lakini kila siku tunazika nambaya zaidi Jeshi la Polisi baada ya mauaji linashinikiza ndugu wa marehemu wachukue maiti kwenda kuzika, wanatoa magari, wanatoa kifuta jasho, hiyo ni *contradiction*. Tunaomba sanasana zichukuliwe hatua thabiti mwisho wa siku isiwe kila siku ni wimbo wa Nyamongo, wananchi wetu wanafariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikibaki hapo hapo Nyamongo, nimekuwa siku zote naongelea suala zima la kuwahamisha wananchi ambao wako kwenye maeneo ambao wanaathirika na mazingira. Mwaka jana nilimuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna ma-*intruder* walienda, Askari wa Jeshi la Polisi katika kuwafukuza wakapiga mabomu watoto wa chekechea, wakawajeruhi na nikaomba, tena Naibu Spika uliniunga mkono, Naibu Waziri wa Nishati wa Madini akaahidi kwamba anaenda kuhakikisha kwamba zile shule zinahamishwa. Hivi ninavyoongea na wewe leo hii bado watoto wako pale licha ya

kwamba usikivu na uelewa haupo kwenye kufuatilia masomo yao, bado wanapata madhara ya kiafya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sanasana wananchi wa Nyamongo wangependa kufaidika na ule mgodi wasingependa kupoteza vizazi kwa mgodi wa Nyamongo kuwa pale. Tunapenda Shule ya Nyamatale, Matongo na Nyabigina zihamishwe na wananchi wahamishwe, tena wananchi kuhamishwa wanatakiwa walipwe stahili zinazostahiki. Naibu Waziri wa Nishati na Madini akijibu swali langu alisema wanalipa dola 22,000 kwa hekta na hicho ndicho kiwango cha chini kabisa, lakini kwa masikitiko makubwa unakuta mwananchi ana uwanja mkubwa karibia hiyo hekta, ana nyumba amejenga za kudumu na siyo zisizo za kudumu lakini unashangaa amepewa cheki ya shilingi milioni saba au milioni nne. Napenda ufafanuzi pia, yale majibu niliyojibiwa hapa yalikuwa ni ya ukweli au ilikuwa ni kujibu tu ili ipite.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna wananchi wa Ronsoti wamekuwa na mgogoro na viwanja vyao au maeneo yao ambayo yamechukuliwa na JWTZ mwaka jana. Kabla ya bajeti niliuliza na Waziri wa Ardhi akasema wameshayashughulikia na wamepanga bajeti wanawahamisha haraka sana iwezekanavyo lakini mpaka leo hii wananchi wa Ronsoti bado hawajiendelezi maana wamebaki tu pale wameambiwa wasiendeleze maeneo yao, hawajalipwa wala hawafanyi kazi ya kimaendeleo wala kiuchumi. Naomba sana wananchi wa Ronsoti Tarime nao wahamishwe au kama hamuwahamishi basi muwaruhusu wafanye shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka nizungumzie suala la afya. Pamoja na sera ya kwamba kila kijiji kiwe na Zahanati, maeneo mengi ya Mkoa wa Mara tuna zahanati na sehemu nyingine hazina Zahanati lakini hakuna dawa, hakuna wahudumu, miundombinu ni mibaya kutoka vijijini kwetu kufuata huduma ya afya mjini na mbaya zaidi hata hospitali ya Wilaya hazina *X-ray*, hawana huduma ya *Ultra Sound*. Mwezi wa tano nilipokuwa Tarime kuna mama mjamzito alikuja akitaka kujifungua lakini alikuja Jumatano yule mama alifariki Jumapili, alikuwa na mapacha lakini hakuna dalili za kwamba amepata uchungu sasa sijui kama ni uzembe wa Madaktari au ni ukosefu wa *Ultra Sound* ambao ungeweza kuchunguza na kugundua yule mama ana matatizo gani. Tunapenda sana tuzidishe wahudumu na vifaa vya afya katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie sekta ya elimu. Kama nilivyosema awali, kama sitamaliza basi nitaandika kwa maandishi, tumekuwa tukiona Serikali inasema ambapo ni kitu cha kweli kwamba wamejenga majengo mengi na wanafunzi wengi wanajiunga na shule lakini tunataka kuona kuna majengo mengi *output* yaani wanafunzi wetu wanaomaliza wanapata elimu gani?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko na sasa naomba nimwite Mheshimiwa Vicky Kamata atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul Marombwa.

MHE. VICKY P. KAMATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Waziri Mkuu, hoja ambayo imejaa majibu tele ya maswali mengi ya Watanzania walio wengi na mimi hoja hii naiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nakwenda Mkoani kwangu Geita na nitazungumzia suala la maji. Mwaka 2010, Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Kikwete alivyokuja Geita alikuta tatizo letu la maji ni sugu, ni tatizo la muda mrefu sana na kulikuwa na programu ya shilingi bilioni 15.3 ambapo Mgodini wa *GGM* ulikuwa unatoa shilingi bilioni 6.99 halafu Serikali ilikuwa inatakiwa itoe shilingi bilioni 9.3. Mradi huu ulikuwa ukamilike mwaka jana Novemba lakini mpaka ninavyoongea bado mradi huu haujaanza lakini kwa upande wa *GGM* shilingi 6.99 bilioni wameshazitoa na kwa hatua za mwanzo, wataalam wameshaanza kazi kwa ajili ya kutoa maji Ziwa Victoria kuyaleta Geita Mjini ambapo Serikali sasa inatakiwa itoe shilingi bilioni 9 ili iweze kufanya *distribution* kwa Geita Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie namna yoyote inavyoweze kama maji yapatikane Geita kwa sababu imekuwa ni kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Geita, akina mama wanalia na wanahangaika na sisi tunaamini chochote kile

anachoahidi Rais anakitekeleza kwa sababu Rais wetu huwa hadanganyi. Kwa hiyo, naomba sana Waziri wa Maji na Naibu wako nadhani mko hapa mnanisikia, naomba sana kwa namna ya pekee na kwa unyenyekevu mkubwa tatizo la maji Geita mliangalie na mtusaidie kwa sababu limekuwa ni tatizo la muda mrefu sana. Tunaishukuru Serikali imetupa Mkoa, imetupa Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya wazuri sana ambao watausukuma Mkoa wa Geita kufikia kule tunakotaka, tunashukuru sana kwa hilo. Lakini tatizo la maji jamani ni tatizo kubwa na tunaumia na tunateseka sana. Mapenzi siku zote yanaimarishwa na kujali, kama hii Serikali inatujali watu wa Geita basi tunaomba itupatie maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la madini. Nampongeza sana Prof. Muhongo, nawapongeza Manaibu wake na ninampongeza Katibu Mkuu wa Nishati na Madini kwa kuonyesha dhamira ya dhati ya kusaidia watu wa Geita lakini bado kuna tatizo. Kuna barua moja ambayo iliandaliwa na Mtaalamu Mwanasheria wa TAMISEMI, barua hii ilikuwa inaelekeza makampuni yote yalipe *Service Levy* Makao Makuu kule yalikutoka. Makampuni mengine Makao Makuu yako Johannersburg, mengine Dar es Salaam lakini yanachimba dhahabu Geita, magari yanazunguka usiku na mchana yanatimua vumbi Geita, wanavyopiga baruti kupata hiyo dhahabu mitikisiko inapasua nyumba, watu wanapata *pressure*, nyumba zinapata ufa lakini eti *Service Levy* inakwenda kulipwa Kinondoni, *Service Levy* inakwenda kulipwa Johannesburg, hii siyo haki! Mimi nadhani huyu

Mwanasheria kama binadamu wengine naye alipotoka wakati anaandaa hiyo barua. Mimi naomba ichaniliwe mbali hiyo barua ili *Service Levy* ilipwe mahali ambapo *service* imetolewa ili Halmashauri ya Geita iweze kupata manufaa na iweze kunufaika na mgodi wa Geita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kilio kikubwa sana pia kinachohusu Magwangala, jana Kaka yangu Donald Marx pia amezungumzia jambo hilo. Magwangala ni mawetaka ambayo hawa watu wa *GGM* wakishatoa dhahabu yao yanabaki, yanakuwa hayana kazi, wanayarundika lakini kwa imani ya watu wa Geita wanaamini kwamba yale wakiyachukua wanakwenda kusaga wanapata dhahabu kwenye yale mawe. Kwa hiyo, wanayanyatia, wanayaiba lakini wanapigwa risasi, wanakufa na hata kuvunjika miguu yaani ni balaa na matatizo makubwa. Naiomba Serikali ikae na hawa *GGM* waweze kuweka utaratibu mzuri kama ni vikundi viundwe ili vijana waweze kupewa yale mawe, wanaamini kwamba wanapata fedha mle kwa nini wasisaidiwe? Kama ni akina mama waunde vikundi na uwekwe utaratibu mzuri basi wayapate kwa sababu tayari wameshaamini kwamba yanawatengenezea pesa kuliko kuacha hivi watu wanakufa kila siku, kwa kweli tumechoka kulilia waume zetu wanakufa na tunachoka kulilia watoto wetu wanakufa basi tunaomba Serikali isikae kimya ili angalie suala hili la Magwangala Geita kwani ni tatizo ambalo limeshakuwa sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iliahidi kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo

lakini mpaka hivi sasa ninavyozungumza bado, watu wanagundua maeneo ambayo yana mali baada ya muda mfupi wanaambiwa toka kwenye eneo hili kuna kampuni fulani inakuja kuchimba, wanakaa kama yatima na wanakuwa wanyonge, kwa kweli mimi ninasikitika sana. Naomba Serikali kwani ni Serikali sikivu na kwa kuwa tayari Serikali ilishaahidi kwamba itatenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo ifanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana kuna kampuni moja tangu mwaka 1992 imehodhi karibu Kata nzima ya Nyarugusu, hawaifanyii kazi yoyote, hachimbi, ametunza, sijui amepanga kuja kuuza kwenye makampuni makubwa lakini leseni yake inaonekana kama ni mchimbaji mdogo lakini amehodhi karibu Kata nzima. Ukiangalia *PML* moja inaweza ikaajiri watu zaidi ya 1000 sasa kwenye Kata hii nzima zingetoka Leseni ngapi? Vijana wangapi wangeajiriwa pale? Naomba kwa unyenyekevu mkubwa suala hili liangaliwe ili wachimbaji wadogo watengewe maeneo waweze kuchimba na hawa wanaohodhi maeneo bila kuyafanyia kazi yoyote wanyang'anywe ili zigawiwe leseni nyingi na watu wengi waweze kunufaika na dhahabu iliyopo Geita maana tumebarikiwa dhahabu basi tuishi maisha kama vile kweli sisi tumetoka kwenye Mkoa wa dhahabu, tusiishi kama maskini bila sababu yoyote ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mengi sana lakini nitaomba nichangie kwa maandishi kwa sababu nina

wasiwasi na muda wangu. Ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Vicky Kamata, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa atafuatiwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa na mimi nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana nianze kusema kwamba siungi mkono hotuba ya Waziri Mkuu na nina sababu mbili ambazo pengine mara baada ya kushawishiwa na majibu ambayo yatatolewa na Waziri Mkuu, nitaweza kuiunga mkono hapo baadaye tutakapokuwa tunapitia vifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kwa kuangalia Kitabu cha Hotuba ya Kiongozi wa Upinzani kwenye ukurasa wa saba, pale chini, alikuwa anazungumzia kuhusiana na suala zima la uchaguzi wa Serikali za Mitaa/Vijiji na Vitongoji. Yeye ali-*generalise* kwamba Serikali imeamua kufuta chaguzi hizo kwa nchi yetu yote, hili jambo si la kweli. Mkoa wa Pwani chaguzi zote za CCM zimesimamishwa na tunafanya chaguzi za Serikali, chaguzi za Chama zitakuja baadaye. Kwa hiyo, asiuchukulie Mkoa moja ndiyo aka-*generalise* kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imesimamisha chaguzi zake katika ngazi za viongozi wa Serikali za Vijiji eti wanachaguzi za viongozi wa CCM, siyo kweli. Hilo la kwanza ambalo ningetaka kulizungumza kwani sisi Mkoa wa Pwani chaguzi za Vijiji

zitafanyika kwanza halafu hizo chaguzi za CCM zitakuja baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme ni kitu gani ambacho kimenisababisha mpaka leo nikatae hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jambo kubwa ambalo limenisababisha mpaka mimi nisiunge mkono hotuba ya Waziri Mkuu, ni suala zima la Serikali kuthamini sana wafugaji na kuwadharau wakulima. Wafugaji katika nchi yetu hii wana sauti kubwa sana kuliko wakulima ambao ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu. Taifa hili haliwezi kuendelea kwa kuwatumia wafugaji, uti wa mgongo wa Taifa letu ni kilimo. Sasa kama unadharau kilimo na unakwenda kuwafuata wafugaji wachache, kwa kweli tunalipeleka pabaya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rufiji ni Wilaya ambaya hakuna mtu asiyejua kwamba hakuna bonde kubwa na lenye rutuba nyingi katika nchi yetu ya Tanzania kama bonde la mto Rufiji, hakuna asiyejua hilo. Lakini kwa bahati mbaya, Rufiji tumevamiwa na wafugaji wamehamishwa kutoka lhefu kwenye bonde lile ambalo Serikali imeamua kulilinda na Serikali hiyo ikawaleta Rufiji na Rufiji wakaingia kwenye bonde la Mto Rufiji ambalo limeharibika sana kuliko ilivyokuwa lhefu. Rufiji kabla ya kuingia ng'ombe hao tulikaa kwenye RCC na tuliomba Serikali kwamba uwezo wa Rufiji siyo ngo'ombe zaidi ya 50,000 lakini tuliomba Serikali kwamba mnapotaka kuwapeleka ng'ombe katika Wilaya ya Rufiji basi nendeni mkazungumze na wananchi wa Rufiji kwa sababu wao hawajui ng'ombe ni ninin sisi ng'ombe kwetu ni wadudun tunawaogopa, nendeni mkatoe elimu ya namna ya kuishi vizuri baina

ya wakulima na wafugaji. Kilichojitokeza, Serikali bila ya kuwashauri wananchi wa Wilaya ya Rufiji, imeamua kupeleka ng'ombe na baada ya kupeleka ng'ombe wale hawakuwekewa miundombinu mizuri, kwa kutowekewa miundombinu, ng'ombe wale wamehama katika maeneo ambayo sisi tuliwapangia wamewapeleka kwenye bonde la Mto Rufiji ambalo sasa hivi kuna ng'ombe zaidi ya 300,000 ndani ya bonde la Mto Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikueleze ukweli kwamba kilimo Rufiji kimepungua kwa zaidi ya 80%, maeneo yote ambayo yalikuwa ya kilimo sasa hivi yamevamiwa na wafugaji na matokeo yake ni nini? Matokeo yake yanasababisha mpaka haya mauaji yanatokea ambapo mauaji haya yanawaandama wakulima mwenyeji wa Wilaya Rufiji wale wafugaji wako katika maisha yao ya usalama. Ule usemi wa 'mgeni njoo mwenyeji apone', Rufiji umegeuka umekuwa 'mgeni njoo mwenyeji afe', ndicho kinachotendeka katika Wilaya ya Rufiji. Sasa kitendo hiki cha kudharau kilimo mwaka huu naomba niarifu Serikali vizuri, Wilaya ya Rufiji ina njaa kubwa sana na ninaomba mpeleke wataalamu waende wakaangalie, sisi tumeshaanza na hii inatokana na kilimo kutozingatiwa, mnathamini sana mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mitano iliyopita, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Rufiji, Mheshimiwa Profesa Mtulia alizungumza Bungeni mambo haya vizuri mno na namna gani suala hili linaweza kuwa bomu hapo baadaye lakini Serikali ikadharau. Mwaka jana aliyekuwa Mbunge wa Rufiji Daktari Seif ambaye sasa

hivi ni Naibu Waziri alizungumza hapa Bungeni kwenye kuchangia hotuba ya Waziri, alielezea ni namna gani athari kubwa zinazopatikana kutoka na wafugaji hawa. Wafugaji hawa wengi ni watu ambao hawathamini kabisa mazingira. Sasa hivi Rufiji mazingira yameharibiwa. Ukimuweka mfugaji mahali anafyeka misitu yote na matokeo yake sasa hivi Rufiji ni jangwa, hakuna chakula, mvua hazipatikani. Alizungumza vizuri na akamuandikia mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu ni namna gani aweze kulitatua tatizo hili lakini kwa bahati mbaya toka iandikwe hiyo barua mpaka sasa hivi utekelezaji wake haujulikani. Sasa tunaiomba Serikali kama Serikali Kuu imeshindwa mturuhusu sisi, sisi Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji tuna sheria zetu ambazo tumeziunda twende tukawatoe wale ng'ombe kwani hatuwezi kukaa na njaa wakati ardhi tunayo. Tutawatoa ng'ombe wote kama Serikali Kuu imeshindwa kuwatoa basi Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ina uwezo tutawatoa wote. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la malipo ya korosho. Mkoa wa Pwani mpaka sasa hivi yale malipo ya pili ya korosho bado hayajapatikana. Waziri Mkuu alieleza kwamba kuna pesa zimetengwa kwa ajili ya kulipia malipo ya pili kwa nchi nzima lakini malipo haya sijui kwa nini Mkoa wa Pwani yanacheleweshwa, sielewi sababu zake ni zipi. Wenzetu wa Tandahimba walipochoma kituo cha Polisi na maduka siku ya pili wakulima wote na Mkoa mzima wa Mtwara na Lindi wamelipwa. Sisi Mkoa wa Pwani jambo hilo bado ni tata, wakulima hawa wanahitaji fedha kwa ajili ya pembejeo, kwa ajili ya kuwapeleka watoto wao shule

na kwa ajili ya matumizi yao ya kawaida lakini inachukua muda mnataka na sisi Rufiji tuchome moto majengo ya Serikali ndipo ninyi muweze kulipa fedha hizi? Mnataka tufanye kama walivyofanya Wamakonde na sisi ndiyo tuwaige wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni uchungu mkubwa! Mimi nilikuwa nafikiri, ni vizuri kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu atuambie Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Tunduru ni sababu gani zinazosababisha mpaka malipo ya korosho yasiweze kupatikana? Tumechoka! Watu wanatuma meseji wanasema sasa hivi badala ya kuchoma majengo ya kawaida wanasema Mheshimiwa Mbunge jengo lako lile ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Abdul Marombwa!

MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono, nashukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake, Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Manaibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi zao wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana hotuba ya Waziri Mkuu kwani imekusanya mengi na kama itatekelezwa ipasavyo, basi tutaweza kupiga hatua kubwa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usioplingika kwamba mabadiliko ya kiuchumi kama ilivyosema Serikali kwamba sekta ya kilimo inachangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa na Serikali inafahamu kwamba katika kipindi hiki sekta ya kilimo imeshuka kwa kiasi kikubwa kutokana na hali mbaya ya ukame iliyokumba baadhi ya maeneo nchini. Je, Serikali sasa naiuliza pamoja na kuimba kwa nini isielekeze fedha zaidi katika *schemes* za umwagiliaji nchini ili kuweza kuendeleza kilimo chenye tija? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Serikali imetueleza yenyewe kwamba pato la Taifa limeshuka kutokana na ukame ulioikumba nchi yetu na tumeona kwamba, baadhi ya wakulima wakubwa katika maeneo mbalimbali wamelima maeneo makubwa lakini mazao yamekumbwa na ukame na matokeo yake hawakupata mavuno. Naiomba sana Serikali kutenga fedha zaidi na hata hizi zilizotengwa basi kuzielekeza zaidi katika skimu za umwagiliaji kwa lengo la kuziendeleza zile zilizokwama na kuanzisha nyingine ili nchi yetu iweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika suala la Benki ya Rasilimali. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametueleza katika hotuba yake kwamba mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Raslimali unaendelea. Utakumbuka katika kipindi cha Bunge lililopita tulielezwa hivyohivyo kwamba, Benki ya Rasilimali mchakato unaendelea, yaani uanzishwaji wa Benki ya Wakulima na tukaelezwa kwamba Serikali imetenga fedha kutoka katika mfuko wa EPA shilingi bilioni mbili (2) ili kuwapatia mikopo wakulima kupitia dirisha la mikopo. Napenda kuiuliza Serikali katika kipindi kile ni wakulima gani na wa kutoka Mikoa gani walifaidika na hizi shilingi bilioni mbili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu baadhi ya wakulima walio wengi hawapati mikopo au ikiwa wanapewa mikopo ni wakulima wa namna ipi na sisi tuliekezwa jamani wanawake wapewe mikopo, wakulima wadogo na wakubwa wapewe mikopo. Kwa hiyo, napenda nijue ni wakulima wa namna gani na wa kutoka Mikoa gani? Nataka pia kujua hii benki hasa itakamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu suala la Muungano. Katika hotuba yake amefafanua vizuri na ameeleza kwamba, maoni 13 yameshughulikiwa na baadhi yanaendelea kushughulikiwa. Miongoni mwa maoni hayo akaelekeza kwamba ni ongezeko la ankara za malipo ya umeme. Pamoja na kuwa maoni haya yanashughulikiwa katika Tume Maalum ambayo imeundwa kutoka Bara na Visiwani, naomba nilete masikitiko yangu kwamba ongezeko la bei za umeme

limekuwa kwa kiasi kikubwa kule Zanzibar. Sijui huku lakini kwa kule Zanzibar bei ya umeme imekuwa kwa kiasi kikubwa na wananchi wanalalamika. Imefikia hatua mpaka wananchi wanashindwa kuwasha taa za umeme ndani kutokana na kuogopa deni. Naomba nieleze kwa kifupi kuhusu ongezeko la bei kwa *units* za umeme. Aliyekuwa ananunua *units* 50 kwa sasa amepandishiwa hadi kufikia asilimia 300. Aliyekuwa ananunua *units* 80 kwa sasa amepandishiwa hadi kufikia *units* 200, aliyekuwa ananunua *units* 120 sasa imepanda hadi kufikia *units* 134. Kwa kweli hili ongezeko ni kubwa sana, wananchi hawawezi kulivumilia. Tunaipongeza sana Serikali kwa kutuvushia umeme kutoka Tanga kuja Pemba, lakini nasema tena Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wanaoshughulika na masuala ya nishati, naomba sana ongezeko la bei ya umeme lipungue, wananchi wataashindwa kutumia umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nimegusia suala la Muungano, nataka kuwaelimisha Wazanzibari wenzangu kuhusu suala la mchakato wa Katiba. Kama tunavyofahamu kwamba sasa hivi baadhi ya wananchi wa Zanzibar wanaendelea kuwapotosha Wazanzibari kwa kufanya maandamano na fujo mbalimbali kwa ajili ya kuukataa Muungano. Tukumbuke kwamba Bunge hili ndilo lililopitisha kuhusu mchakato wa Katiba na tukumbuke kwamba sheria ile kabla ya kupitishwa hapa Bungeni ilikwenda Zanzibar na Wazanzibari pale Bwawani Hotel walichana mapendekezo ya sheria ile. Wakatoa maoni kwamba imekuja kwa lugha ya Kingereza sasa tunaitaka kwa Kiswahili. Wakashindwa kutoa maoni yao kwa hiyo

wale wasiofahamu Kingereza wakashindwa kutoa maoni. Matokeo yake sheria ile ikaja kwa Lugha ya Kiswahili na sisi kwa juhudi zote tukaenda kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria ile na hivyo pia hawakutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna malalamiko wanasema hawakushirikishwa katika sheria ile na wanaendelea kupotosha Wazanzibari kwa kuwaambia kwamba kataeni sheria ile haikubaliki. Sasa ninachowaambia ni kwamba, sheria ile tuliipitisha Bungeni, tunakumbuka kwamba wenzetu wa upande wa pili walitoka lakini Mheshimiwa Rais akatoa kauli kwamba, jamani njooni Ikulu mlete marekebisho. Vyama mbalimbali vilikwenda Ikulu na wakatoa marekebisho yao, kwa nini wao wasiende? Walikwenda baadhi na marekebisho yakaletwa tena Bungeni tukayapitisha, sheria ile ikaundwa. Kwa hiyo, kama kuna maoni ya wananchi kuhusu suala la Katiba au suala lolote linalohusiana na Muungano wasubiri Tume tayari imeshaundwa, waisubiri waje kutoa mawazo yao kwenye hiyo Tume. Kama ikiwa ni kuhusu suala la Mahakama ya Kadhi kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge mwenzangu, kama ni kuhusu sijui fedha 4.5, kama ni kuhusu sijui kitu gani, chochote kile waje wazungumze kwenye Katiba na maoni baadaye tutapitisha kwenye Bunge la Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba Wazanzibari wenzangu msiendeleo kuwapotosha Wazanzibari. Waacheni Wazanzibari wazisome Katiba na wakishafanya hivyo wataweza kujua nini cha kufanya na nini watolee maoni yao. Waacheni Wazanzibari wasome Katiba. Mkifanya fujo

hawatakata muda wa kuzisoma. Naishukuru sana Ofisi ya Katiba na Sheria iliyopita, iliyokuwa inaongozwa na Mheshimiwa Celina Kombani, alinipatia Katiba na nilikwenda kuzisambaza Kaskazini Pemba na sasa hivi wananchi wanaendelea kuzisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa na mimi naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kuongea jioni hii ya leo. Pongezi zangu kubwa sana nimpungeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote ambazo zimewasilisha bajeti zao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru wafuatao; kwanza Mkuu wa Mkoa wangu wa Iringa, RAS wa Mkoa wa Iringa ambao kwa kweli wameweza kunipa ofisi nzuri sana inaniwezesha kufanya kazi vizuri na wananchi wa Mkoa mzima wa Iringa na wa Jimbo la Iringa pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa Mkoa wa Iringa lakini naingia katika Halmashauri ya Manispaa ambapo kuna Jimbo la Iringa. Napenda sana kuleta changamoto zilizopo katika Mkoa wangu lakini nipenda kutoa changamoto zilizopo katika Jimbo la Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Iringa Mjini najua tuna Baraza la Mawaziri wa Serikali lakini tuna Wabunge

Vivuli na nafikiri Vivuli huwa wanaona zaidi kuliko Mawaziri wenyewe. Kwa hiyo, nasema Jimbo lile mimi ni Mbunge Kivuli na nisiposema wananchi wa Jimbo lile hawatanielewa kwa sababu yapo matatizo mengi, zipo changamoto nyingi sana ambazo zinakabili Jimbo lile. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Sema!

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze na shukrani. Hospitali yetu ya Mkoa wa Iringa ilikuwa na msongamano mkubwa sana, nimshukuru sana Mheshimiwa Mwanri nilipouliza swali alikuja Iringa tukaweza kufungua hospitali ya Wilaya. Lakini hospitali ile kuna mambo madogo madogo ambayo ningepomba kwanza yachukuliwe na yaangaliwe ili sasa ule msongamano uweze kuondoka na hospitali iweze kwenda vizuri. Kuna upungufu wa Madaktari, vifaa vya hospitali, vilevile barabara inayotoka katika ile hospitali kwenye barabara ya Mkoa ni mbovu sana, ina ma-*corrugations* mengi kiasi kwamba mgonjwa akitoka kwenye ile hospitali anaweza akafia hata njiani. Ni kama kilomita mbili (2) tu, naomba tusaidiwe katika Halmashauri ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningenda labda Serikali ilichukue, kumekuwepo na tatizo kubwa sana la ucheleweshaji wa fedha za maendeleo katika Halmashauri zetu likiwemo Jimbo la Iringa. Ipo miradi mingi ambayo ilikuwa imetengewa fedha kutoka mwaka jana, lakini mpaka mwaka huu fedha zile bado hazijaletwa. Nafikiri nchi hii itakwenda kama tutazingatia kilimo cha umwagiliaji. Katika Kata

ya Isakalilo kuna mradi wa Mkoga. Ule mradi muda mrefu sana umekuwa ukitengewa fedha lakini hazifiki. Halmashauri imetenga fedha, kuna nguvu za wananchi ambazo ziko pale lakini mpaka leo hii zinatakiwa shilingi milioni 380 ambazo bado hazijawafikia wananchi. Naomba suala hili lichukuliwe. Nakumbuka mwaka jana pia niliwasilisha na aliyekuwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula analitambua vizuri kwa sababu nilimletea hata *documents* za mradi huu. Namshukuru Mungu sasa hivi amekuwa Waziri kamili. Kwanza nimpongeze lakini namuomba sana sasa hivi alishughulikie kwa umakini kwa sababu wananchi hawatuelewi, wanatuona kama vile hatasukumi mambo yao. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Kilimo aangalie hii miradi ya umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna mradi mwingine wa umwagiliaji uliopo katika Kata ya Kitwiru, *Kitwiru Irrigation Scheme* na wenyewe unahitaji kama shilingi milioni 335. Naomba miradi hii iangaliwe kwa umakini wake ili wananchi wa Iringa, hatupendi kuomba sana chakula kwa sababu tunao uwezo wa kilimo na kama hii miradi kweli itatengewa fedha hizo basi tuna imani kwamba hata Majimbo mengine ambayo yatakuwa na njaa yanaweza yakasaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uko mradi mwingine ambao kwa kweli unasikitisha sana, mradi wa machinjio uliopo katika Kata hiyo hiyo ya Isakalilo. Mradi huu zinahitajika shilingi milioni 200 na mwaka jana niliomba. Wananchi tunategemea kwamba huu mradi utakapokamilika utasaidia hata ajira. Wananchi watajiajiri kupitia machinjio hii ya kisasa. Tayari mradi

huu umeshapata wafadhili kutoka *UNIDO*, mwaka huu wanakuja kuleta vifaa vyote vipya na wamesema kwamba wanataka waje wakute jengo liko tayari. Makamu wa Rais alikuja kuweka jiwe la msingi, Mheshimiwa Mwanri nafikiri anaweza akashuhudia kwa sababu alikuja kukagua na akakuta kwamba ule mradi uko vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba sana ujaribu kusukuma tupate hizo fedha ili mradi huu uanze kufanya kazi katika mwaka huuhuu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo lingine katika Jimbo hilo hilo la Iringa Mjini. Katika Kata ya Kihesa kuna hifadhi ya msitu inayoitwa Kihesa Kilolo. Kwa kweli ile hifadhi imekuwa ni kichaka cha majambazi. Pale jirani kuna chuo sasa hivi tunaomba ile hifadhi ibadilishwe ili tuweze kupima viwanja kwa sababu imezungukwa na majengo ya watu. Siyo siri, tuna vyuo vingi sana pale Iringa, vijana wanapata matatizo makubwa sana ya hosteli. Tuna imani kwamba kama ule msitu watauhawilisha basi tutapata viwanja na tutaweza kufanya maendeleo makubwa sana katika Jimbo letu la Iringa Mjini. Nitaomba Wizara ya Maliasili itupatie majibu ni lini kwa sababu toka mwaka 2010 tumekuwa tukipeleka barua lakini hazina majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisipowasemea Wamachinga nitakuwa sijawatendea haki. Najua Waziri Mkuu ni mtoto wa mkulima, lakini vilevile na mimi ni mtoto wa mkulima na mtoto wa Mmachinga. Nafikiri wengi ni mashahidi. Naomba sasa Halmashauri zianze kuwatengea vijana maeneo kwa ajili ya biashara ndogondogo. Nasikia uchungu sana ninapoona vijana

wananyanyasika, wanapigwa, wanafanyiwa yote hayo bila kutengewa maeneo, tunakuwa hatuwatendei haki.

MBUNGE FULANI: Usilie bwana.

MHE. RITTA E. KABATI: Kwa kweli ninaweza nikalia.

MBUNGE FULANI: Aah, usilie bwana. (*Kicheko*)

MHE. RITTA E. KABATI: Niungane pia na Mheshimiwa Neema aliyesema kwamba ipo haja hawa vijana wa bodaboda nao tuwaangalie. Kama tunasamehe kodi kwenye makampuni mengine, kwa nini na wao wasisamehewe? Pale Iringa kuna vijana kama 4000 wamejajiri kwa ajili ya bodaboda na vijana wengine wanajisomesha kutokana na hizi bodaboda. Sasa kama kweli tutawaangalia vijana hawa, najua kuna kodi nyingi sana ambazo kama tutaziangalia Serikali hii tutakusanya fedha nyingi sana. Pengine labda tu kuna ile kodi za leseni sijui zimefikia wapi. Labda niulize Wizara ya Fedha, Halmashauri nyingi sana zinasubiri, hii kodi imeishia wapi? Maana yake tunajua kwamba ni chanzo kimojawapo cha fedha katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nimshukuru sana Waziri Mkuu kwa majibu yake ya Alhamis. Huwa anatoa majibu mazuri sana yenye uhakika. Nakumbuka nilipochangia mwaka jana nilikuwa nimesema ningeleta Hoja Binafsi, lakini nikishukuru sana Kiti siku ya Alhamis wanapoongoza sasa hivi wamekuwa wakiangalia yale maswali

kwamba ni yale ambayo yanatakiwa kuulizwa, yanakuwa hayana *data*, lakini wakati ule nilipochangia mwaka jana yale maswali mara nyingi yalikuwa yanalenga kumdhalilisha Waziri Mkuu wetu. Kwa hiyo, niwashukuru pia hata Wabunge kwamba sasa hivi angalau mmeweza kuona ni maswali gani ya kumuuliza Waziri Mkuu maana haji hapa kwa ajili ya kudharaulika, anakuja hapa kwa ajili ya kujibu maswali ili wananchi waweze kuona umakini alio nao kwani vipo vitu vingi ambavyo wanapenda kuvisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba niunge mkono na nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, niseme kwamba jimbo la Iringa Mjini ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati. Waheshimiwa Wabunge, tutakubaliana kwamba Mheshimiwa Ritta Kabati amewasemea vizuri sana wananchi wa Iringa Mjini. *(Makofi/Kicheko)*

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Kuhusu mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mwongozo Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo kupitia Kanuni ya 68(7) ambayo inasema:-

" Halikadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niombe Mwongozo kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi za hotuba tunazoziweka kwenye *Hansard* za Bunge. Nilisemea hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye Wizara ya Fedha baada ya kugundua upungufu mkubwa na wao wakarekebisha lakini nimekuja kuona kwenye *addendum* ambayo ilikuwa imesainiwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, nadhani ilikuwa bahati mbaya alisaini bila kusoma. Nikamwambia kijana mwenzangu arekebishe na wakawa wamerekebisha. Pamoja na kurekebisha hii imeendelea pia, ukisoma ukurasa wa nne (4) kwenye hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwenye tarakimu juu kabisa pale...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Nitakupa nafasi kwa sababu ni suala la utaratibu tumuache Mheshimiwa amalize, ingekuwa taarifa ningekupa nafasi moja kwa moja. Mheshimiwa malizia halafu nitampa nafasi Mheshimwia Lissu.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Kwa mujibu wa utaratibu wa kuandika tarakimu jinsi nilivyofundishwa darasa la pili, unapozitaja tarakimu zikiwa zinamaanisha bilioni tarakimu peke yake zinajitosheleza au maneno, lakini wao walivyoandika ukurasa wa nne wameandika bilioni, bilioni 91 hiyo ni sehemu mojawapo. Sehemu ya pili wameandika bilioni, bilioni 24, ukurasa wa tano (5) wameandika bilioni, bilioni 134. Kwa ajili ya kumbukumbu zako na kwa ajili ya kumbukumbu za Watanzania bilioni, bilioni 134 haijawahi kutokea kwenye bajeti ya nchi yoyote ya Afrika Mashariki na Kati. (*Makofi*)

Lakini pia ukienda ukurasa wa 15 wa Kitabu kilekile cha Kiongozi wa Upinzani Bungeni, walichukua ile hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama kupitia swali lake kuhusu Pansheni kwa Wazee, lakini nadhani kwa ajili ya kutaka umaarufu wa harakaharaka wakabandika namba hapa, lakini hii namba walipobandika, imebandikwa kama ya posho ya wanafunzi ambao wanasajiliwa kwa mwaka wa masomo. Lakini ukienda kwa kanuni na utaratibu wa ku-*calculate pension* kwa *pensioners*, utaratibu uliotolewa na akina Barry, Aron, Robert na James Capreta unatakiwa u-*gross* namba ya wale *pensioners* unaowa-*target* kwa takribani mara robo tatu ili ku-*accommodate* namba ya wale watakaokuwa wanafikisha umri mwezi hadi mwezi. Wao

wamebandika tu kama ya wanafunzi wanaodahiliwa mwaka hadi mwaka na kupata *figure* ambayo ukiipigia hesabu kimsingi baada ya mwezi mmoja tu *pensioners* wengine watakuokuwa wanatimiza mwaka kuanzia mwezi utakaofuatia na miezi mingine kumi (10) katika mwaka, hawatakuwa wametengewa bajeti yao. Sasa kwa makosa haya na mengine mengi kutokana na muda sitayasema, niliona niombe mwongozo kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi kwenye *Hansard* kama inaruhusiwa kuleta vitu ambavyo vimeandaliwa, sijajua walikuwa na *hangover* ya nini maana yake makosa ni mengi mno.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Kama utaona hairuhusiwi, uwaagize *either* warekebishe ama waiandike upya hotuba hii kabla hatujamaliza kujadili hotuba ya Waziri Mkuu. Ahsante sana, Mheshimiwa naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimwona Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba nitoe utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(b) na vilevile Kanuni ya 68 (7) inayohusu Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Tusomee hiyo 64.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1)(b) inazungumzia Mbunge

kutokuzungumzia suala ambalo haliko kwenye mjadala.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala ulioko mbele ya Bunge lako Tukufu ni hoja ya Waziri Mkuu. Huo ndiyo mjadala ulioko mbele ya Bunge hili tangu siku ya Jumatatu, hilo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) Mwongozo unaombwa kwa jambo ambalo limetokea mapema, siyo kwa jambo ambalo limetokea juzi au wiki iliyopita.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Sasa ufundi wa kuzomea siyo ufundi wa kujua, ni ufundi wa kuzomea.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tumsikilize Mheshimiwa Tundu Lissu. Kwa muda wangu uliobakia ukiangalia saa yangu pale, nakuomba ufupishe sana.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nitafupisha. Anachokifanya huyu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba anataka kuleta kwa njia ya Mwongozo mambo ambayo hayatakiwi kwa wakati huu. Kama alikuwa makini kama anavyojifanya, kama ni makini hivyo alitakiwa alione hili siku ambayo hotuba ya Kiongozi wa Upinzani ilitolewa, siyo siku tatu baadaye, huo ni ushahidi wa kukosa...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wangu kwa kweli hauko upande wangu. Naomba maelekezo ya Mwongozo huu nitayatoa siku zijazo lakini nikumbushie mambo madogo mawili ya ushauri wa jumla.

La kwanza, Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu inasema kwamba, Bunge likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2012/2013. Hapa hajadiliwi Rais, hajadiliwi Waziri Mkuu, hiyo ndiyo hoja. Nataka kuwakumbusha tu Waheshimiwa Wabunge kila anayesimama kila wakati kukumbuka na kujua hoja ni ipi.

La pili la ushauri wa jumla, katika mfumo wa Vyama vingi, katika Mabunge ambayo yana Vyama vingi kama vya kwetu, tuna kambi ya Chama Tawala na Kambi ya Upinzani. Katika Mabunge ya Vyama Vingi, Mbunge wa Chama Tawala hana uhuru sana kama anavyofikiri kupinga bajeti ya Serikali yake kwa sababu ile bajeti ni ya kwake, wajibu wake Kikatiba ni kuishauri kwanza Serikali na kama kweli haisikii basi kuiadhibu lakini Mbunge wa Chama Tawala kuanza kutoa adhabu tu jumla jumla, hapo inabidi kuangalia vizuri kidogo. Ushauri wa jumla.

Waheshimiwa Wabunge, hoja za siku ya leo zimekamilika, naomba kuahirisha Bunge hadi kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 1.49 Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi,
Tarehe 28 Juni, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*